# Nipashe

Ijumaa Oktoba 4, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580040

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Kikundi vijana chafungua mlango wa ajira kupitia utotoaji kuku

Faru Mweusi anavyochochea upekee Hifadhi Ngorongoro

Habari katika picha

EU katika changamoto Uingereza na Marekani

Ukurasa 15

UKURASA 13



**Mwanamke mmoja kati ya watatu atatizwa na kiribatumbo, kitambi**

UKURASA 3

# DPP ashtukia janja ya mawakili msamaha JPM

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**UTEKELEZAJI MIRADI MABILIONI WASITISHWA**

SIKU nne baada ya Rais John Magufuli kukerwa na baadhi ya viongozi ambao hawasimamii na kuchukua...

**UKURASA WA 4**

**MUSIBA AKWAMISHA KESI DHIDI YA FATMA**

MAHAKAMA Kuu Zanzibar imehairisha shauri la kesi ya Mwanasheria Fatma Karume dhidi ya...

**UKURASA WA 21**

**SERIKALI KULIPA FIDIA WALIOJENGA HIFADHINI**

SERIKALI itawalipa fidia wananchi tisa ambao hawakulipwa kupisha ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha...


## Wachimba mchanga wajeruhi polisi jamii

UKURASA 9



UKURASA 2



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akiwacharaza viboko wanafunzi wa Shule ya Chalangwa, wilayani Chunya, mkoani humo jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mjadala kila kona RC kupiga viboko watoto

**MICHEZO** **STARS, RWANDA KUPIMANA NGUVU** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# PP ashtukia janja ya mawakili msamaha JPM

Na Waandishi Wetu

MKURUGENZI wa Mashtaka (DDP), Biswalo Mganga, amesema amebaini baadhi ya mawakili wanaofanya utapeli kwa kwenda kwa washtakiwa wa kesi za uhujumu uchumi kuchukua fedha, kwa madai wanakwenda kuwalipia katika ofisi yake.

Kadhalika, DPP amesema wanaotaka kurejesha fedha walizopewa na Mkurugenzi Mtendaji wa VIP Engineering, James Rugemalira, zinapokelewa na waliogawiwa wakati huo kuwa, haoni sababu ya kuzikataa.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, DPP Mganga alisema katika mchakato unaendelea wa urejeshaji wa fedha kwa washtakiwa wa kesi za uhujumu uchumi, wamewabaini baadhi ya mawakili kufanya utapeli.

"Tunapokuwa tunafanya kazi hizi kuna wajanja wanajitokeza, kuna mambo ambayo nimeweza kuyaona nikaona sio vyema nikayaacha yaendelea," alisema.

Aliongezea: "Tumekuwa tukiendelea na zoezi la watu kutubu mahakamani, kuomba msamaha na kuamuliwa kulipa fedha kwa kiwango alichoamuliwa," alisema.

Mganga alisema wakati zoezi hilo linaendelea, kuna baadhi ya watu wakiwamo mawakili wanatumika kukwamisha mchakato huo.

"Leo (jana) tumepata taarifa kuna baadhi ya mawakili wanachukua fedha kwa baadhi ya washtakiwa, wanasema wanazileta Ofisi ya DPP. Naomba niwakanye na niwaonye wanaofanya hivyo wanatafuta ugomvi na tayari nimeshaanza kufanya uchunguzi," alisema.

Aliwataka kufanya shughuli zao za uwakili bila kuathiri heshima ya ofisi yake la sivyo wasije kulaumiana.

Alisema utaratibu wa mshtakiwa kukiri upo pale pale kwa kufuata taratibu za sheria mahakamani.

Kwa mujibu wa Mganga, taratibu za kulipa malipo zipo mahakamani na sio wakili ama mtu yoyote kutoka na kwenda gerezani au kumfuata ndugu na kumuambia awapatie fedha.

"Huo utaratibu haupo katika mchakato kama huo, kuna wajanja wajanja wanajitokeza wanaotaka kufanya uhalifu katika zoezi hili wajiandae tutapambana hatutawavumilia," alisema.

Mganga alisema kwa kuliangalia hilo, ni kwamba waligundua kuna mambo yanaweza kujitokeza, hivyo serikali imefungua akaunti maalum itakayotumika kuweka fedha zote zitakazokuwa zimepatikana katika mchakato huo zitawekwa humo.

"Hii sio akaunti ya mahakama ni akaunti maalumu imefunguliwa Benki ya Kuu (BoT) kwa amri ya serikali viongozi wakuu wa mahakama watajulishwa, hivyo hakuna fedha itakayolipwa katika akaunti ya Mahakama, DPP ama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)," alisema.

Alisema ambaye atalipa sehemu nyingine wasilaumiane na kwamba ofisi yake haitamvumilia mla rushwa.

**SERIKALI KUPOKEA ZA RUGEMARILA**

Alipoulizwa kuhusiana na urejeshwaji wa fedha za mtuhumiwa katika kesi ya Uhujumu uchumi, James Rugemalira, DPP Mganga alisema hawezi kuzuia watu kurejesha, na kwamba fedha hizo zitaingia kwenyea akaunti hiyo maalum.

"Sasa kama mtu anajua alifanya na anaona hawezi kuendelea kuwa na uchafu rohoni unamzuiaje asirejeshe pamoja na kwamba anaona hajafika huko, lakini anaona haya ni matatizo, anaona bora nijisafishe pengine Mungu aendelee kumrehemu vizuri," alisema

**WENGINE WALIPA MIL. 100/-**

Katika hatua nyingine, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya Arusha, Rose Ngoka, jana aliwahukumu washtakiwa kumi ambao ni raia wa kigeni, kulipa Sh. milioni 100 au kwenda jela miezi 12, kwa kosa kufanya kazi Kampuni ya Uwindaji ya Oterlo Businness Coperation (OBC) bila kuwa na kibali cha kufanya kazi nchini.

Watu hao ni Darweshi Jumma,

INAENDELEA UK.26




Wakazi wa Butiama, wakifanya usafi na kulipaka rangi jengo lilimo kaburi la Hayati Baba wa Taifa, Mwl. Julius Kambarage Nyerere, katika eneo la Mwitongo, mkoani Mara jana, ikiwa ni maandalizi ya maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 20 ya kifo chake yatakayofanyika Oktoba 14. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Utekelezaji miradi ya mabilioni wasitishwa

Na Romana Mallya

SIKU nne baada ya Rais John Magufuli kukerwa na baadhi ya viongozi ambao hawasimamii na kuchukua uamuzi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Fedha na Mipango, imeisitisha 20 yenye thamani ya Sh. bilioni 161. 6.

Miongoni mwa miradi hiyo ambayo Septemba 16, mwaka huu, Rais Magufuli alionyesha kukwera nayo ni pamoja na uboreshaji wa ufukwe wa Coco Beach ulioko Oysterbay jijini Dar es Salaam na mradi wa ujenzi wa machinjio ya kisasa Vingunguti ambayo katika orodha ya wizara, utekelezaji wake umesitishwa.

Barua ya wizara iliyoandikwa Septemba 19 na Katibu Mkuu wake, James Doto, kwenda kwa watendaji ngazi ya mikoa, majiji na wilaya, imeitaja miradi hiyo iliyositishwa na mingine 18 itakayoendelea yenye thamani Sh. bilioni 126.4 ambayo utekelezaji wake uko kwenye ujenzi.

Kwa mujibu wa barua hiyo, watendaji walioandikiwa ni makatibu tawala wa mikoa, wakurugenzi wa majiji, manispaa na miji, na wakurugenzi watendaji wa halmashauri za wilaya zote Tanzania Bara.

Msemaji wa wizara hiyo, Ben Mwaipaja, alilithibitishia gazeti hili jana kuwa barua hiyo ambayo ilisambaa mtandaoni ni yao lakini wizara hiyo imesikitishwa na kitendo hicho kwa sababu haikuwa kwa ajili ya umma bali viongozi walioainishwa ndani yake.

"Ni kweli baadhi ya miradi imezuiwa hadi maelekezo mengine yatakapotolewa. Tunatumia fedha za walipakodi, halmashauri zijitegemee kimapato na kuboresha huduma za wananchi. Unapoona watu wanakaa na fedha muda mrefu hawatendi haki, ndiyo maana tumezuia utoaji

INAENDELEA UK.26

# Mjadala kila kona RC kuchapa viboko

Na Waandishi Wetu

WADAU mbalimbali nchini wamepinga vikali uamuzi wa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuwachapa viboko vitatu kila mmoja wanafunzi 14 wa Shule ya Sekondari Kiwanja wilayani Chunya.

Wanafunzi hao wanadaiwa kuchoma mabweni mawili ya shule hiyo yaliyoungua Oktoba Mosi, mwaka huu, kwa kile kinachoelezwa ni mawasiliano yao ya simu kuonyesha kuwa walipanga kutenda kosa hilo.

Mjadala uliibuka kwenye mitandao ya kijamii baada ya picha ya video ikimwonyesha kiongozi huyo akiwaadhibu wanafunzi hao mbele ya wanafunzi wengine, viongozi wa shule na viongozi wengine.

Mjadala mkubwa ulijikita kwenye Waraka wa Elimu Na. 24 kuhusu adhabu ya viboko ambao umeweka bayana kuwa ni mwalimu mkuu wa shule husika au mwalimu mwingine atakayeteuliwa na mwalimu mkuu kwa maandishi kila mara kosa linalostahili adhabu hiyo.

Waraka huo unaonya kuwa mwanafunzi wa kike anapaswa kupewa adhabu ya viboko na mwalimu wa kike tu isipokuwa kama shule haina mwalimu wa kike.

Pia waraka huo umeweka wazi kuwa kila mara adhabu ya viboko inapotolewa, sharti iorodheshwe katika kitabu kilichotengwa kwa kusudi la kujaza taarifa zihusuzo adhabu husika, ikiwa ni pamoja na jina la mwanafunzi anayeadhibiwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, katika ukurasa wake wa twitter, aliandika: "Nakemea kitendo hiki cha kikatili. Adhabu ya viboko ni

INAENDELEA UK.26

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
03/10/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI tarehe 5/10/2019** kampuni ya **CHINA SICHUAN INTERNATIONAL COOPERATION (SIETCO)** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka SONGEA kuelekea MAFINGA. Gari yenye namba za usajili

   **T 586 DMF / T 369 DNW**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 19 |
| Upana | - | mita | 3.1 |
| Kimo | - | mita | 4.5 |

3. Njia itakayotumika: SONGEA hadi MAFINGA kupitia NJOMBE.

   Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

115444102

# Mwanamke mmoja kati ya watatu atatizwa na kiribatumbo, kitambi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema viwango vya utapiamlo ikiwamo uzito uliozidi kwa wanawake wenye umri wa kuzaa vimeongezeka nchini na havikubaliki kimataifa.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua mkutano wa sita wa mwaka wa tathmini ya lishe nchini.

Alisema pamoja na utafiti kuonesha kupungua kwa viwango vya udumavu na upungufu wa damu, bado viwango vyake havikubaliki kimataifa na viwango vya utapiamlo vimezidi kuongezeka na pia havikubaliki kimataifa hususan uzito ulioziḍi kwa wanawake wenye umri wa kuzaa.

"Tuzingatie taratibu za kula, watu wanayo lugha ya kujivunia wanapokula kujichana, lakini kujichana huko kuna madhara, asubuhi unajaza vitu vyote mayai badala ya moja unaweka matatu, viazi, mihogo mwingine chips tena asubuhi anasema anashushia, lazima tujadili tupeane utaratibu na kuelimisha jamii ulaji wa vyakula," alisema.

Aliwataka watoa ushauri nasaha pia kutoa elimu kwa wanawake wenye umri huo ili kupunguza matatizo yanayoweza kujitokeza na ni hatari kubwa kwa nchi kutokana na kukabiliwa na aina nyingine ya utapiamlo.

Aidha, alisema Tanzania mambo yamebadilika mtu akiwa na kitambi ndio heshima na kuonekana mtu ambaye hana afya yake ni mbaya kumbe ni kinyume.

"Wale wenzangu wa vitambi kama mpo lazima mfanye mazoezi ili muweze kuondokana na vitambi kwa kuwa vina madhara yake." "Udumavu, utapiamlo mkali na wakadiri una athari kubwa kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, tunatakiwa kuongeza jitihada mbalimbali katika kupambana na aina zote za utapiamlo ili kufikia viwango vinavyokubalika kimataifa," alisema.

"Wadau waeleze vigezo vya kimataifa ambavyo vinapaswa kufikiwa. Matokeo ya utafiti yatupe chachu ya kukabiliana na tatizo la utapiamlo," alisema.

Majaliwa alitaka Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) kuendelea kuweka mazingira mazuri ya lishe na kushauri masuala hiyo.

Aliwaagiza wataalamu wabuni mbinu na mikakati ya kupunguza tatizo la utapiamlo na kuainisha rasilimali zinazohitajika ili kuleta ufanisi.

Naye, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema suala la vitambi na viribatumbo kwa wanawake nchini ni tishio kwasasa ambapo takwimu zinaonesha thelusi moja ya wanawake wana tatizo hilo.

"Kubwa na la kutisha bado thelusi moja ya wanawake katika nchi yetu wanakabiliwa na tatizo la vitambi na viribatumbo na hili eneo linazidi kuongezeka," alisema.

Alisema Tanzania imepiga hatua katika kupunguza udumavu kutoka asilimia 34.4 kwa mwaka 2015 na kufikia asilimia 31.8.

"Ukondefu nao umepungua kutoka asilimia 4.3 na kufikia asilimia 3.5, upungufu wa damu kwa akina mama nao umepungua kutoka asilimia 45 na kufikia asilimia 29," alisema.

## Risiti EFD mfupa mgumu kwa mapambano ya rushwa

**Na Salome Kitomari**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imeeleza vikwazo inavyokumbana navyo katika kukabiliana na rushwa kwenye utoaji wa stakabadhi kwa mashine za kielektroniki (EFD).

Akijibu maswali ya wakuu na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam juzi, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema Takukuru inayo makosa 24 yaliyotajwa kwenye Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Alisema waliwahi kufanya operesheni ndogo ya kujua namna mashine za EFD zinavyofanya kazi.

"Upo udanganyifu mkubwa sana katika kutumia mashine hizo. Unakuta mafanyabiashara anazalisha risiti anampa aliyenunua bidhaa lakini haandiki thamani ya fedha aliyonunua dukani," alisema Mkurugenzi huyo.

Kwa mujibu wa Jenerali Mbungo, waliwahi kulizungumza suala hilo na waliibuka watu na kusema Takukuru inaingilia majukumu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Wakati mwingine wananchi hawaelewi haraka na wanaona tunaingilia maeneo ya watu wengine," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema ndani ya sheria ya kuzuia na kupambana na arushwa kuna kipengele kinachosema kutumia stakabadhi kuidanganya mamlaka.

"Ukitumia kudanganya mamlaka ni kosa la rushwa chini ya kifungu cha 22. mwenye duka akiandika amepepokea Sh. 20,000 wakati amepokea

INAENDELEA UK.26

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

TRA

## TAARIFA KWA UMMA

Mnamo tarehe 14 Juni, 2018, Waziri wa Fedha na Mipango alitangaza msamaha maalum wa riba na adhabu kwa Walipakodi wenye malimbikizo ya madeni, na wale ambao wako tayari kuweka wazi madeni ya nyuma kwa hiari yao wenyewe na kulipa kodi ya msingi kwa utaratibu ulioanishwa katika (Amri Na. 282A ya Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018.

Mpango maalum wa msamaha wa riba na adhabu ni fursa maalumu ya muda mfupi iliyotolewa. Utaratibu huu ulianza 01 Julai, 2018 hadi Juni 30, 2019 na ilihusisha malimbikizo ya madeni ya kodi yaliyokuwepo.

Hata hivyo, Serikali kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu), (Nyongeza ya muda wa kulipa)2019 , iliongeza muda wa malipo ya kodi ya msingi kufikia tarehe 31 Disemba 2019 kwa walipakodi ambao;

a) waliomba msamaha wa riba na adhabu za kodi kwa Kamishna Mkuu;
b) waliopatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi;
c) waliingia makubaliano na Kamishna Mkuu ya kusamehewa riba na adhabu za kodi kama ilivyoanishwa katika Amri Na. 282A ya Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018;
d) walianza kulipa kodi ya msingi kwa mkupuo au kwa awamu; na
e) mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2019 walishindwa kulipa kiasi cha kodi ya msingi kilichokubaliwa kwa ukamilifu.

Hivyo, wastahiki wote wa msamaha waliopatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi mnakumbushwa kulipa kodi ya msingi kama ilivyoainishwa kwenye mikataba ya makubaliano wa malipo kabla au kufikia tarehe 31 Disemba, 2019 na kwamba hakuna nyongeza zaidi ya muda itakayotolewa.

Izingatiwe kwamba, pindi mstahiki wa msamaha aliyepatiwa msamaha wa riba na adhabu za kodi kupitia Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu), 2018 atashindwa kutekeleza sehemu ya masharti ya mkataba wa makubaliano wa malipo, Kamishna Mkuu atabatilisha mkataba wa makubaliano wa malipo na kudai kiasi cha kodi kilichosalia kama vile hakukuwa na msamaha alioutoa. Aidha, hatua za ukusanyaji zitachukuliwa kuanzia tarehe 2/1/2020 bila taarifa nyingine.

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

**Dr. Edwin P. Mhede Ph.D**
**KAMISHNA MKUU**

215445702

## Askari polisi kortini kwa tuhuma rushwa mil 60/-

**Na Hellen Mwango**

WATU watano wakiwamo Askari wa Jeshi la Polisi wanne wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na mashtaka ya kuomba na kupokea rushwa ya zaidi ya Sh. milioni 60.

Washtakiwa hao ni Mfanyabiashara Patrick Kumburu (40), askari Erick Kumburu (39), Jonas Lwezimula (36), Mohammed (33) na Sajenti Swedy Hamisi Swedy (34).

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya mahakimu wawili, Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustine Rwizile na Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi.

Katika kesi ya kwanza, Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon aliwasomea mashtaka yao mbele ya Hakimu Shaidi kwa madai kwamba washtakiwa hao walikula njama ya kupata fedha kati ya Julai 3 na Julai 7, mwaka huu, maeneo ya Mtaa wa

INAENDELEA UK. 26



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akizungumza na wazazi wa baadhi ya watoto kati ya 20 wanaotarajiwa kufanyiwa upasuaji wa moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Msako nyumba kwa nyumba wazazi wanaoficha watoto

**Na Ibrahim Joseph,** BAHI

UONGOZI wa wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, umetangaza kuanza msako wa nyumba kwa nyumba kuwakamata wazazi wanaoficha watoto nyumbani badala ya kuwapeleka shuleni.

Msako huo ulitangazwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mukunda, alipokuwa akizungumza na wazazi na walimu wa Shule ya Msingi Mpalanga katika ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo na miradi elimu.

Alisema kwenye wilaya hiyo bado kuna watu wanaficha watoto wao nyumbani hawataki kuwapeleka shuleni ili wapate elimu.

"Kuna watu katika wilaya yetu bado wanawaficha watoto wao nyumbani hawataki kuwapeleka shuleni huku wakichunga mifugo. Nawaambia msako mkubwa unakuja, tutakapokuta mzazi hutaki kumpeleka mtoto shuleni tutakupeleka mahakamani kwa kumkosesha mtoto haki yake ya kupata elimu," alisema.

Aidha, alisema msako huo utahusisha kuwakamata wazazi wa watoto ambao ni watoro shuleni na ambao wameacha shule huku wakibaki kuchunga mifugo.

Alibainisha kuwa lengo la msako huo ni kuhakikisha kila mtoto wa wilaya hiyo anapata haki yake kikatiba ya kupata elimu ili kutokomeza ujinga.

Aidha alisema katika mikakati yake ni kuhakikisha kila mtoto anapata haki hiyo ya elimu.

Sambamba na hilo, alisema wanafunzi 450 wa kidato cha kwanza wanaotoka kwenye mazingira magumu walilipiwa gharama za masomo na mahitaji yao ya shule.

"Watoto hao walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza lakini walishindwa na halmashauri yetu ilichukua jukumu hilo la kulipia gharama za mahitaji yao ya shule na sasa wapo wanaendelea na masomo," alisema.

Alisema serikali ilipotangaza elimu bila malipo, ilikuwa na lengo la kuwasaidia familia zote ziweze kupata haki hiyo muhimu katika maisha.

Naye mdau wa elimu wa wilaya hiyo, Mathias Njoji, alisema kwa kushirikiana na uongozi wa wilaya hiyo, wamekuwa wakichangia madawati katika shule mbalimbali.

Njoji alisema wamekuwa wakiwawezesha vifaa ya shule kama madaftari na kalamu wanafunzi wanaotoka kwenye mazingira magumu ili kupata haki hiyo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mpalanga, Hussein Ngozi, alisema shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa walimu na kwamba waliopo ni 13 huku wanafunzi wakiwa 1,285.

Ngozi aliitaja changamoto nyingine ni upungufu wa nyumba za walimu kwa kuwa mahitaji ni 13 wakati zilizopo ni mbili.

"Pia upungufu wa madawati 162 ambapo mahitaji ni madawati 428 na yaliyopo ni 266," alisema.






# Korti yapiga kalenda kesi ya Fatma dhidi ya Musiba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAHAKAMA Kuu Zanzibar imehairisha shauri la kesi ya Mwanasheria Fatma Karume dhidi ya mwanaharakati, Cyprian Musiba hadi Oktoba 28, mwaka huu .

Naibu Mrajisi wa Mahakama hiyo, Salum Hassan, alisema amelazimika kuahirisha shauri hilo kutokana na upande wa mlalamikiwa kutokamilisha utetezi wake aliotakiwa kuupeleka.

Alisema ameamua kutoa nafasi ya kutosha kwa mwanasheria huyo kuandaa na kupeleka utetezi wa mteja wake.

Musiba uliwakilishwa na wakili Ruben Mandara kutoka Zanzibar kutokana na upande wa mawakili wa mlalamikiwa kutofika mahakamani hapo.

Wakili Mandara aliyomba Mahakama kusogeza mbele kusikilizwa kwa shauri hilo ili kumpa nafasi mteja wake kupeleka utetezi wake.

Upande wa mlalamikaji Fatma Karume ulikubaliana na mamuzi ya Mrajisi huyo na kuomba mlalamikiwa ahakikishe kuwa anapeleka utetezi wake mapema.

Fatma Karume aliiambia Mahakama kwamba muda wa kutoa maelezo ulishapita wiki mbili, hivyo ipo haja ya shauri hilo kupangiwa kusikilizwa kwa kuwa wadaiwa wamepewa muda wa kutosha.

Kesi hiyo ilifunguliwa September 28, mwaka huu na Fatma dhidi ya Musiba akidai kumdhalilisha kupitia taarifa zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii na magazeti.

# Utafutaji wa mwili ajali boti hifadhini wakwama

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

KAZI ya kuopoa mwili wa muongoza watalii, Samuel Mhina aliyezama kwenye Ziwa Momela katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha, baada ya upepo kupindua mtumbwi waliokuwa wanafanyia utalii imekuwa ngumu baada kushindwa kuupata.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, aliiambia Nipashe kuwa kazi ya kuutafuta mwili wa imekuwa ngumu baada ya kushindwa kuupata na kuuopoa.

"Tulitegemea baada ya saa 24 ungeelea na kuopolewa, lakini haikuwa hivyo, badala yake tumeshindwa kujua uko upande gani ndani ya ziwa," alisema jana.

Muro alisema ameshafanya mawasiliano na Jeshi la Polisi Kitengo ya uokoaji na anasubiri wapigambizi kuzamia na kuuopoa mwili huo.

Alisema wapiga mbizi wapatao watano watafika muda wowote wakitokea Dar es Salaam kuungana na wa wenzao wa Arusha na wenzetu wa Hifadhi ya Taifa ya Arusha ili kuutafuta mwili wa na kuuopoa.

"Nipo Hapa uwanjani KIA nawasubiri wazamiaji wafike ili niwapeleke Momela moja kwa moja, tutahakikisha tunampata samuel akiwa hai au amekufa, zoezi hili nina imani litafanikiwa, maana wapigambizi hao wana mitungi ya oxygen, kwa hiyo watazama ndani ya maji kuopoa huo mwili.

Ajali hiyo ilitokea juzi mchana wakati Mhina kutoka Kampuni ya Kitalii ya Africa tours akiwa na mtalii raia wa Ujerumani wakitalii kwa mtumbwi na ghafla kimbunga kikaibuka kupindua mtumbwi na kuzama.

Baada ya kupinduka mtumbwi Mhina alidaiwa kuzama , huku mtalii huyo, RoseBever Heike, alijiokoa.

# Viashiria wakurugenzi wengi kutumbiliwa hivi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI, Selemani Jafo, ametaja viashiria vitatu vinavyosababisha wakurugenzi wengi wa Halmashauri nchini kutumbuliwa.

Viashiria hivyo ni pamoja na kushindwa kusimamia uwapo wa mahusiano mazuri, kushindwa kukusanya mapato na kutosimamia fedha za miradi zinazopelekwa katika maeneo yao ili zifanye kazi iliyokusudiwa.

Jafo alitoa kauli hiyo jana katika kikao kazi kwa wakurugenzi wapya 10 walioteuliwa hivi karibuni na Rais John Magufuli.

Waziri huyo alisema viashiria hivyo pamoja na vingine ndivyo vinasababisha wakurugenzi kuondolewa.

"Wakurugenzi ambao hawana uwezo wa kukusanya mapato ni miongoni mwa indicator (viashiria) vikubwa vya wakurugenzi kuondoka, jambo la pili kushindwa kusimamia miradi ya maendeleo serikali inayopeleka na jambo la tatu ni mahusiano. Wakurugenzi mkisikia kila siku boti inapakua inajaza hizi ndio indicator tatu, kwa hiyo hizi parameters tatu nendeni mkazifanyie kazi."

"Siku zote huwa nasema chombo cha Tamisemi ni tofauti na miaka mingine, hii ni safari kama umechoka kushika bomba utaachia bomba, na ukiachia bomba ina maana wengine watatamani kushika bomba," alisema na kuongeza:

"Nyinyi wakurugenzi kakamateni vizuri bomba, maeneo yote mnakokwenda mnaenda kufanya replacement kwa sababu maalum, kafenyi kazi."

Jafo alieleza baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri wamekuwa hawatekelezi wajibu wao ipasavyo.

"Inashangaza mtu anakuwa na dokezo mezani miezi sita, watu wamepewa fedha za kujenga vituo vya afya, lakini havikamiliki, tunataka watu wanaofanya kazi kwa usahihi na kwa haraka zaidi.. naomba niwaambie wakurugenzi ambao mapato yao hayatoshi, hawana uwezo wa kukusanya mapato hii ni ishara kubwa sana kwa wakurugenzi kuondoka," alisema.

Jafo alikumbusha katika ziara yake ya Malinyi ambapo kulikuwa na tatizo kubwa la mahusiano.

"Unayeenda Morogoro vijijini, pale hata fedha Sh. milioni 500 tulizozipeleka ukienda kuzigoogle huzioni, nimeenda pale na kubaini Sh. milioni 66 zimekwenda kununua dawa ya mchwa, hivyo nenda ukafanye wajibu wako, maana eneo lako kuna shinda kubwa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo," alisisitiza.

Kadhalika, alisema kwa Halmashauri Rombo na Siha kuna tatizo la mahusiano, hivyo wakafanye wajibu ili halmashauri ziweze kusonga mbele.

Kuhusu wakurugenzi wapya kutokuwa Mungu-mtu, Jafo aliwataka wakawatumikie wananchi na kuhakikisha wanasimamia fedha za miradi na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa weledi na kasi kubwa.

Aliwasisitiza kujiamini vya kutosha katika nafasi zao wakijua Mungu amewapa nafasi. "Nendeni mkawatumike watu wake, kumbukeni mmeteuliwa kutokana na uwezo wenu ili mkamsaidie Rais aliyewateua, jambo kubwa ambalo mnatakiwa kwenda kusimamia mahusiano, wengi wanafeli katika siku ya kwanza kwa sababu wanashindwa kusimamia mahusiano," alisema.

Aliongeza "Unapokuwa kiongozi sio kila kitu unakijua, hapana mwende mkaunganishe mawazo ya wataalamu katika halmashauri zenu ili ziweze kusonga mbele, mnakokwenda mtakuta magomvi makubwa, msiende kununua ugomvi wa watu."

"Pia kuna watu wengine katika halmashauri nyingine ni mabingwa wa kujipendekeza pindi wakurugenzi wapya wanapofika, anakuwa mtu wa kwanza kuepeleka umbeya lengo ni kuwa umtambue kuwa yeye ndiye anayefaa ili ukiitwa Tamisemi aweze kukaimu."

Waziri Jafo aliwahimiza wakurugenzi hao kufuata itifaki za viongozi wengine katika maeneo yao.

**ewura**

Energy and Water Utilities Regulatory Authority

ISO 9001:2015 Certified

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole

S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz

*Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni Taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea iliyoundwa na Sheria ya EWURA Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA inawajibu wa kuzidhibiti sekta hizi kiufundi na kiuchumi. Mamlaka ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida ya halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.*

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/No | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 35 | ET & T's Investment Ltd – Samanga Marangu Petrol Station S.L.P 31165 Dar es salaam | Kijiji cha Samanga, Kata ya Marangu, Wilaya ya Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro | Eliawony Towo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 36 | Nasser Gas Distribution S.L.P 1249 Dodoma | Kiwanja Namba 122, Kitalu "U", Eneo la Maisaka B, Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara | Menyiwe Christian Gama (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya LPG |
| 37 | Pirson Investment Ltd Dara es salaam | Eneo la Mbezi Juu, Wilaya ya Kinondoni, Jiji la Da es salaam | Ayub Mbowe (Mtanzania) | Leseni ya kusambaza gesi ya kupikia |
| 38 | Nyambi Service Station – Newala S.L.P 190 Newala | Eneo la Luchingu, Wilaya ya Newala, Mkoa wa Mtwara | Nurdini Nyambi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 39 | Sinohydro Corporation Limited S.L.P 70589 Dar es salaam | Eneo la Upanga Mashariki, Wilaya ya Ilala, Jiji la Dar es salaam | Guo Xinming (Raia wa China) | Leseni ya jumla ya vilainishi |
| 40 | Oryx Oil Company Ltd S.L.P 9540 Dar es salaam | Kiwanja Na.523, Kitalu 46, Eneo la Kijitonyama, Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es salaam | Christopher Paul Swart (Raia wa Afrika Kusini) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 41 | Tanzania Zambia Railway Authority S.L.P 2834 Dar es salaam | Kiwanja Na.210, Eneo la Tazara, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es salaam | Nelson Kaserwa (Raia wa Tanzania) | Leseni ya jumla ya vilainishi |
| 42 | Projestus Rutinwa – Kyebitembe S.L.P 49 Muleba | Mtaa Kisana, Eneo Kyebitembe Wilaya ya Muleba Mkoa Kagera | Projestus Rutinwa(Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 43 | Abel Isaya Filling Station S.L.P 475 Kasulu | Viwanja Na. 21,22 & 23 Eneo la Mwilamvya, Barabara ya Kibondo, Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma . | Abel Isaya (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 44 | Lake Oil Bomba Mbili Geita S.L.P 5055 Dar es salaam | Kiwanja Na 99/1 Kitalu 'D' Eneo la Bombambili Wilaya ya Geita Mkoa wa Geita | Stephen Mtemi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 45 | GBP Tanzania Limited S.L.P 3728 Dar es Salaam | Kiwanja Na. 319, Kitalu 'D', Eneo la Nyankumbu, Wilaya ya Geita, Mkoa wa Geita | Rashid Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 46 | Calvary Filling Station Pwani | Eneo la Bokomnemela, Wilaya ya Kibaha Vijijini, Mkoa wa Pwani | Bildard Rogathe Lema (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa juu.

215444702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kama viroba viliondoka mataputapu ni ya nini?

**KATIKA** moja ya taarifa zetu za jana kulikuwa na habari ya kuiomba serikali kudhibiti utengenezaji wa pombe za kienyeji ambazo kwa hakika ni chanzo cha matatizo ya kiafya.

Pombe kama kama gongo, mbege, ulanzi, boha na chimpumu zimekuwa zikizalishwa Dar es Salaam na kwenye miji mingine mikubwa licha ya kwamba ziko kwa wingi vijijini na ndiyo maeneo yenye wanywaji wengi.

Aidha, kwa kuona kilio hicho nasi tunaungana na wadau hao wanaojali afya za walaji kuiomba serikali kupinga matumizi ya vinywaji hivyo ambavyo si kwamba tu ni hatari kwa binadamu bali pia ni mwanzo wa udhalilishaji watoto na wanawake vilabuni.

Tuanze na suala la afya, pombe hizo hutengenezwa katika mazingira duni, hutumia maji machafu na uandaaji wake wakati mwingine hufanyika porini na vyombo vinavyotumiwa ni vichafu na wapo wanaotumia au kuchanganya pombe hizo na sumu.

Suala la sumu lilijitokeza miaka ya karibuni wakati watu zaidi ya 15 walipofariki Kimara jijini Dar es Salaam baada ya kunywa gongo iliyochanganywa na sarafu za senti tano, dawa ya madoa ya jiki na pia iliwekwa kwenye matangi ambayo huenda yalikuwa na sumu ya sulphonic acid' ambayo hayakusafishwa kikamilifu.

Kuna wanaosema kuwa hata taka za chooni hutumiwa kupika gongo, pumba na taka nyingine au hata unga wa kiwango duni uliovunda nao hutumiwa kupika komoni ambayo hadi kuchachuka hupitia hatua mbalimbali kama vile kuvunda na kuwa na wadudu kama sumu kuvu.

Wasimamizi wa afya watakubaliana nasi kuwa pombe hizo huandaliwa kwenye mazingira ya ajabu ikiwa ni pamoja na ulezi au mtama kuanika na vimea vyake kutandazwa kwenye mikeka kwenye mazingira machafu.

Mikeka yenye vimelea hivyo huwekwa pembeni ya barabara na kwenye viwanja au maeneo ya wazi ambayo huchafuliwa na vumbi, vinyesi vya wanyama na ndege na wakati mwingine vumbi la injini za magari.

Maji yanayotumiwa kuzichuja ni machafu ya mtoni au mabwawani na hata uchujaji wake ni wa kiwango duni unaotumia mashuka au viroba.

Aidha, uuzaji wa pombe hizo hufanyika katika maeneo ya giza na watoto hasa mabinti hutumiwa kuuza pombe hizo zinazonywewa maeneo yasiyo na vyoo wala huduma muhimu za kijamii na wakati mwingine nyumbani kwa wafanyabiashara wanaohusika.

Ni sehemu ambazo mabinti wanaweza kubakwa, watoto kudhalilishwa na wakati mwingine hata kufanyiwa mambo mabaya.

Suala la afya ni jambo muhimu na ni lazima kulipa kipaumbele kwani linamaliza rasilimali nyingi za taifa kutibu taifodi, kipindupindu, amiba, kuhara damu na maradhi mengi yanayotokana na ulevi kama ini na figo.


Tunaungana na wadau kuitaka serikali kumaliza tatizo hilo kwani kama pombe za viroba na mifuko ya nailoni lilimalizika pombe za mataputapu zinangoja nini?

Watu wanaokunywa mataputapu wakati mwingine hutumia vijiwe au vilabu hivyo kwa ajili ya kufanya uhalifu kama wizi na uhalifu hasa unaofanyika usiku wa manane kwa kuwa sehemu hizo mara nyingi hazina ufuatiliaji wa karibu wa vyombo vya dola.

Shime elimu itolewe kwa wanaoandaa pombe hizo na kukumbushwa kuwa ni mwanzo wa maradhi ili kukomesha madhara yanayotokana na pombe za kienyeji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






**Na Sabato Kasika**

## Muungwana Lazima Nilonge

# Enyi wauza mkaa, elimu hii ya TFS inawahusu

**MATUMIZI** ya nishati ya mkaa, hasa katika maeneo ya mijini yana nafasi kubwa na yamekuwa yakiongezeka na kufikia kiwango cha juu sana. Sababu kubwa ni kutokuwapo nishati mbadala yenye bei nafuu.

Kuongezeka matumizi ya nishati hiyo, kunaelezwa kuchangia ongezeko la ukataji na ufyekaji miti, pia mkaa unatengenezwa bila ya kuwapo mpango endelevu wa matumizi ya rasilimali miti, ili isiteketee.

Pia, kingine kinachotajwa kuchangia katika ongezeko la matumizi ya rasilimali miti hiyo kwenye mkaa, ni utengenezaji wake kwa njia isiyoboreshwa, hivyo kutumia miti mingi kutengeneza mkaa kidogo.

Hiyo ni kwa mujibu wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) Kanda ya Kusini, ambao wanasema mkaa hutengenezwa kwa matanuru, lakini kunatakiwa kuwapo utengenezaji bora wa nishati hiyo.

Ofisa Ugani na Uenezi wa TFS Kanda ya Kusini, David Namwaga, anasisitiza umuhimu wa elimu kwa wananchi, kujua jinsi ya kutengeneza matanuru bora ya mkaa.

Anasema, TFS imekuwa ikijitahidi kuwajengea uwezo wananchi kwa ajili ya uelewa wa masuala ya mkaa na kusimamia utengenezaji bora wa mkaa katika maeneo yao ili kupunguza ukataji wa miti ovyo.

"Jambo lingine ni kujenga uwezo wa kupigana na uzalishaji na utengenezaji mbovu wa mkaa pale unapotokea na kusababisha uharibifu wa ubora wa mkaa au soko la mkaa," anasema Namwaga.

Pia, anafafanua kwamba, wakala huo wa kitaifa unafanya harakati za kudhibiti uzalishaji mkaa usiozingatia taratibu, kwa ajili ya kuokoa mapato ya serikali yanayopotea kwa kutoroshwa na kutunza mazingira.

Kwa mujibu wa TFS, kuna matanuru bora ya mkaa yanayotakiwa kutumika kwa ajili ya uzalishaji bora wa mkaa, pia usajili na ukataji leseni ya biashara uzingatie taratibu na sheria ya uvunaji wa mazao ya misitu.

Tanuru linalofaa kutumika kwa hapa nchini, ni lile la asili la kichuguu-udongo lililofanyiwa maboresho ya kina, baada ya kuingizwa kwa vipengele vikuu viwili vya tanuru la aina ya 'CASAMANCE' au Tanuru la Senegal.

Namwaga anaeleza kwa kutaja vifaa vinavyohitajika, ili kutengeneza tanuru lililoboreshwa kuwa jembe kwa ajili ya kusafishia eneo na kuchimba udongo, chepe la kuchota udongo wa kulifunika.

Kingine kinachohitajika katika tanuru hilo, kinatajwa kuwa ni 'futi kamba' ya kupima ukubwa wa tanuru, bati la futi 6.8 au 10 ili kutengenezea pa kutoa moshi, tupa, nyundo, tindo, viatu-bati na kofia.

Mjadala huu unaunga mkono juhudi za TFS kulinda misitu hasa wakati huu ambao bado hakuna nishati mbadala wa uhakika, ingawa ukataji miti kwa ajili ya mkaa umekuwa ukipigiwa kelele kwamba unaharibu mazingira.

Biashara ya mkaa ina soko kubwa. Katika wakati huu ambao hakuna nishati mbadala, ni vyema wafanyabiashara wakazingatia uvunaji na hata uchomaji, ili kutokata miti mingi kama TFS inavyoelekeza.

Katika kukabiliana na uharibifu wa mazao ya misitu, serikali ilitangaza kanuni mpya kwa ajili ya kuongeza usimamizi wa sheria kwa wanunuzi na wauzaji mazao hayo, ikiwamo mkaa na samani mbalimbali.

Hiyo ni tangu mwezi Mei mwaka huu, ilipotangaza kupitia tangazo la serikali, adhabu kwa atakayekuka kanuni hizo ni faini ya Sh. 500,000 hadi Sh. milioni 12 au kifungo kati ya miezi sita hadi miaka mitano.

Juhudi hizo zote ni kwa ajili ya kuokoa misitu na hata kama inakatwa, basi iwe ni kwa kufuata utaratibu uliowekwa, ili kulinda mazingira, badala ya kuyaharibu kama ambavyo inatokea kwenye baadhi ya maeneo.

Kimsingi, elimu inayotolewa na TFS kama itazingatiwa kuanzia kwenye uvunaji misitu hadi kuchoma mkaa, kutakuwapo uhakika mkubwa katika utunzaji misitu nchini.

Huko nyuma, taarifa iliyowahi kutolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, jijini Dar es Salaam, ni kwamba mkoa Dar es Salaam unaongoza kwa matumizi ya nishati ya mkaa, ikimaliza tani 500,000 kwa mwaka.

Hivyo, wakati mkaa ukiendelea kuwa na nafasi kubwa katika matumizi ya kila siku, ni vyema kuzingatia hatua zinazosaidia kupunguza changamoto za uharibifu wa mazingira na ukataji ovyo wa miti.

HABARI KITAIFA

# Waonywa utoroshaji mbolea nje

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imewaonya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao wanadaiwa kutorosha mbolea kwenda nchi jirani kutokana na bei ya pembejeo hiyo kuwa na bei kubwa katika nchi hizo.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitoa onyo hilo jijini Dar es Salaam alipokuwa akitangaza bei mpya ya mbolea za kupandia za DAP na Urea ambazo zimeshushwa kati ya asilimia sita na 17.

Alisema kushuka kwa bei hiyo kunatokana na ushindani wa zabuni za mfumo wa ununuzi wa pamoja (BPS) iliyofunguliwa Juni 21, mwaka huu.

Alisema tangu kuanza kwa BPS mwaka 2017, huu ni msimu wa tatu wa kilimo wa utekelezaji wake kwa mbole kuingizwa nchini.

Mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja (BPS) umechangia kushusha bei za mbolea kwenye chanzo na usafirishaji baharini, hivyo kumfanya mkulima kunufaika na hali hiyo.

BPS imefanya gharama za usafirishaji wa mbolea baharini kushuka kwa kiasi kikubwa kutoka Sh. 23,000 hadi Sh. 3,500 kwa mfuko wa kilo 50.

"Pamoja na kwamba hii ni neema kwa wakulima wetu, hali hii inahatarisha utoshelevu wa mbolea kwa wakulima wetu. Licha ya uelimishaji ambao wizara yangu inaendelea kuufanya katika mikoa ya mipakani, natoa onyo kali kwa wafanyabiashara wachache wenye tabia hiyo.

"Endapo kutakuwa na haja ya wafanyabiashara kuuza mbolea nje ya nchi, basi wafanye hivyo kwa kuzingatia sheria za nchi, "alisema Waziri Hasunga huku akisema bei elekezi za mbolea hutegemea umbali wa sehemu inakopelekwa kutokea bandarini.

"Kwa wastani, gharama ya kusafirisha mfuko mmoja wa mbolea wa kilo 50 kwa barabara kutoka Bandari ya Dar es salaam hadi makao makuu ya halmashauri ni Sh. 5,500 kwa kilometa 1,000," alisema Waziri Hasunga.

Hata hivyo, alisema gharama hizo hupanda na kushuka kutegemeana na hali ya barabara na hali ya hewa (masika au kiangazi).

Aidha, alisema usafiri kwa njia ya reli ni nafuu zaidi kwa sababu gharama za kusafirisha mbolea kwa kilometa 1,000 kwa mfuko wa kilo 50 ni Sh. 4,160 (TRC) au Sh. 4,600 kwa Tazara.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea, Dk. Steven Ngairo aliwataka wakulima kuona umuhimu wa kutumia fursa iliyotangazwa kuhusu punguzo la bei.

Mwishoni mwa Agosti, mwaka huu, serikali ilitangaza bei elekezi za mbolea ya kupandia (DAP) katika soko la ndani ambayo ilishuka kwa Sh. 8,000 hadi Sh. 10,000 sawa na asilimia 13 hadi 17.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi (aliyepiga magoti), akiongoza maombi kabla ya kuanza mkutano wa kuwaelimisha wananchi tafsiri sahihi ya mpaka kati ya Tabora na Singida, katika Kitongoji cha Matagata, wilayani Manyoni hivi karibuni. Mkutano huo, ulifanikiwa kumaliza mgogoro wa mpaka baina ya Wilaya ya Manyoni na Sikonge, uliodumu kwa zaidi ya miaka 25 na kusababisha wananchi kutojua wanawajibika wapi kiutawala. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri. **PICHA: TIGANYA VINCENT**

# Wafurahia mafunzo umeme jua India

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI watatu wa fani ya uhandisi waliokwenda India kusomea fani hiyo kwa ufadhili wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph, wamejivunia kupata utaalamu wa kutengeneza umeme wa bei nafuu kwa kutumia upepo na jua.

Wanafunzi hao waliwasili nchini jana na kupokewa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam na ndugu, jamaa na marafiki na viongozi wa chuo hicho.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Penina Angolo alisema India imepiga hatua kubwa kiteknolojia, hivyo wana mambo mengi ya kujivunia kuhusu masomo yao ya uhandisi waliyoyapata nchini humo.

Tanzania inapoelekea kwenye uchumi wa viwanda, alisema inahitaji umeme mwingi wa uhakika na wa bei nafuu, hivyo utaalamu walioupata unaweza kuisaidia nchi kusogea kutoka ilipo.

Alisema wamejifunza kwa vitendo mambo mengi hasa kozi hiyo ya umeme wa upepo na jua ambayo nchi hiyo imekuwa ikitumia kuzalisha umeme na kuwapatia wananchi wake wengi mijini na vijijini.

Kwa mujibu wa mwanafunzi huyo, uzalishaji wa umeme wa njia hizo mbili unahitaji mtaji wa kawaida lakini baada ya hapo faida zake ni nyingi kwa kuwa husaidia kuzalisha umeme wa uhakika. Alisema kwa sasa umeme wa sasa wa kutegemea maji bado haujawa wa uhakika.

"Wenzetu wako mbele sana katika teknolojia ya ujenzi na sisi tulifanikiwa kwenda kwenye taasisi za umma zinazotoa fani mbalimbali fupi ambazo zitatusaidia katika mambo ambayo tumesomea kama wahandisi," alisema na kuwataja wenzake kuwa ni Modester Ndelwa na Sonia Sillas.

Naye Mlezi wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph, Mathew Ngulugulu, alisema chuo hicho kimekuwa na kawaida ya kuwapeleka wanafunzi nje ya nchi kwa ajili ya kujifunza zaidi kwenye fani zao.

"Tulianza miaka 10 iliyopita na tulipoanza tuliwapeleka 56 kwa mkupuo mmoja lakini safari hii wamekwenda watatu wote wakisomea fani ya uhandisi.

Tunashukuru wamerudi wakiwa salama na wakiwa na ujuzi tunarajia wana kitu kipya cha kujivunia," alisema

Aidha, alisema nchi hiyo imepiga hatua kubwa kiteknolojia na ndiyo sababu chuo hicho kila kinapopata fursa kinawapeleka wanafunzi wake ili wakapate utaalamu zaidi ambao utasaidia maendeleo ya nchi.

## Waziri amsimamisha mhandisi wa umeme

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amemsimamisha kazi Mhandisi Samson Mwangulume wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) baada ya umeme kukatika kutokana na hitilafu iliyotokea katika kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Ubungo, Dar es Salaam.

Umeme huo ulikatika usiku wa Oktoba 03 na kusababisha Mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar kukosa huduma hiyo kwa muda.

Dk. Kalemani alichukua hatua hiyo baada ya kufanya ziara ya kutaka kujua tatizo lililosababisha umeme kukatika.

Baada kutembelea kituo hicho na kuona mfumo mzima wa kusafirisha umeme kwa njia ya kieletroniki (Scader) na kupata maelezo kutoka kwa wataalam, alibaini kuwa chanzo cha hitilafu hiyo ni uchafu katika vikombe katika transifoma kubwa namba sita inayozalisha umeme wa Megawati 120.

Kutokana na kubaini hilo, alisema huo ni uzembe uliofanywa na msimamizi aliyekuwa zamu siku hiyo pia kutofanya kazi yake kwa ufanisi, ikiwamo kutofanyika kwa ukaguzi na matengenezo ya mitambo mara kwa mara.

"Wataalamu wangu wamenambia kuwa kuna fyuzi ilikatika, lakini nimetaka kujiridhisha...sababu kubwa waliyonieleza ni uchafu, sasa hili suala la uchafu ni uzembe uliofanywa na aliyekuwa zamu kushindwa kubadilisha na kufanya usafi katika vikombe hivyo.

"Nimetoa maelekezo huyu Samson aliyekuwa zamu namsimamisha kazi kutokana na uzembe wake. Atupishe watasimamia wengine," alisema.

# Waliochota mil. 78/- za wanafunzi Chuo cha Ualimu Moshi warejesha

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WATU waliotajwa kuhusika katika kashfa ya upotevu wa fedha za wanafunzi 400 wa Chuo cha Ualimu Moshi, zamani Mong'are wamezitapika, baada ya kubanwa na serikali na kisha kurejesha Sh. milioni 54.876 kati ya Sh. milioni 76.9 zinazotakiwa kurejeshwa.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, alithibitisha kuwa kiasi hicho cha fedha kilikuwa kimerejeshwa katika akaunti ya Chuo cha Ualimu Moshi, hadi kufikia Oktoba 2, mwaka huu.

"Tumekuja kuwataarifu, kwa heshima ya Mwenyezi Mungu na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa nchi hii (Dk. John Magufuli), mpaka kufikia tarehe ya leo (jana), tunao ushahidi na stakabadhi za benki za Meleckezeck Mchau, ameshalipa Sh. milioni 20 na nimetoa maelekezo, nilisema na nikaagiza Mkuu wa Chuo na DAS (Katibu Tawala wa Wilaya) waende wakajiridhishe benki kama fedha zimewekwa.

"Mtu wa pili ni ELCT Saccos, wamelipa kiasi walichotakiwa kulipa katika mgawo wao wa Sh. milioni 12.313 ninayo stakabadhi hii hapa. Mtu wa tatu ni chuo, wao wamelipa Sh. milioni 12.313, mtu wa nne ni Sarafina Mbwambo, yeye amelipa Sh. milioni 10 na risiti hii hapa, na ameomba kwamba ndani ya kipindi cha wiki tatu atakuwa amelipa Sh. milioni 10 iliyobaki," alisema Ole Sabaya na kuongeza:

"Mtu wa mwisho ni Benki ya CRDB ambao wao wamekuja ofisini wameomba waandikiane 'deed of settlement' kwa sababu wana utaratibu wao, wamekuja kusaini kwa hawa, wameenda kusaini kwa wale wengine na wameniambia Ijumaa wiki hii, fedha hizo zitakuwa zimeingia. Tunafungia mjadala hapa, wazazi na wanafunzi, hamtalipa ada tena kwa sababu serikali inayoongozwa na Rais Magufuli imerejesha fedha zenu za watoto wenu zilizokuwa zimechukuliwa." Awali, Mkurugenzi na Mmiliki wa Chuo cha Ualimu Moshi, Joseph Msaki, akizungumza mbele ya wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama pamoja na wazazi na wanafunzi wa chuo hicho, alisema tayari fedha hizo zimerejeshwa kwa asilimia 80.

Kutokana na mafanikio hayo, Msaki alitangaza ahueni kwa wanafunzi wapya wa daraja la tatu A (Grade IIIA) na Diploma kwamba hawatalazimika kulipa gharama za hosteli kwa mwaka mzima kwa sababu ya heshima hiyo ya Rais Magufuli.

Vile vile, Msaki alitangaza ofa maalum kwa walimu waliowahi kusoma chuoni hapo na kushindwa kuchukua vyeti vyao vya taaluma, kulipa asilimia 50 ya madai yao ndani ya siku 30 ili wakabidhiwe shahada zao.

Mwezi uliopita, wanafunzi hao waligoma kuingia katika vyumba vya mitihani ya kumaliza kozi na wengine mitihani ya muhula na kufanya maandamano, wakitaka kujua hatima ya fedha zao za malipo ya ada.

Wanafunzi hao waligomea kuingia katika vyumba vya mitihani ya kuhitimu masomo yao na wengine ambao walikuwa wanafanya mitihani ya muhula iliyokuwa ianze kati ya Septemba 9 hadi Septemba 12, mwaka huu.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Wenye Ulemavu), Stella Ikupa (kushoto), akisalimiana na baadhi ya watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga wakati wa ziara yake kukagua utekelezaji wa masuala ya Ukimwi juzi. **PICHA: OWM**

# Jalada tuhuma za mwalimu rushwa ngono latua kwa DPP

**Na Allan Isack,** ARUSHA

UCHUNGUZI wa kesi ya rushwa ya ngono inayomkabili mwalimu wa Chuo cha Ufundi Arusha(ATC), umekamilika na jalada la mashtaka limepelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Akizungumza na wanahabari wakati wa kusoma taarifa ya utendaji kazi kwa kipindi cha miezi mitatu, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Arusha, Frida Wikesi, alisema shauri hilo limekamilika, na jalada limeshapelekwa kwa DPP.

"Baada ya kupokea taarifa tulijiridhisha nayo na tuliandaa mtego kwa mtuhumiwa na tulifanikiwa kumkamata," alisema Wekesi.

Hata hivyo, alisema hajafikishwa mahakamani kwa sababu kesi ya rushwa ya ngono ni mojawapo ya mashauri ambayo lazima yapite kwanza kwa DPP.

"Mtuhumiwa hajafikishwa mahakamani kutokana na aina ya shauri lake, lazima lipite kwanza katika ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka," alieleza Wekesi.

"Kama DPP akipitia jalada hilo, huenda akaturudishia kwa maelezo kama mtuhumiwa afikishwe mahakamani au hasifikishwe,"alisema.

Agosti 2, mtuhumiwa huyo, Lusato Kanyika, alikamatwa na Takukuru kwa madai ya kukutwa na mwanafunzi wa chuo hicho katika nyumba ya kulala wageni, akidaiwa kuomba rushwa ya ngono.

Awali, Ofisa Habari wa (ATC), Gasto Leseiyo, alikiri mwalimu huyo alituhumiwa kuomba rushwa ya ngono kwa lengo la kumsaidia mwanafunzi kufaulu somo la mafunzo viwandani (IPT).

Alisema chuo hicho kilishtushwa na taarifa hiyo ya rushwa ya ngono na endapo mamlaka husika wakihitaji chochote wapo tayari kutoa ushirikiano.

# Vyama 200 Saccos kukutana Arusha

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ZAIDI ya vyama 200 vya ushirika wa akiba na mikopo nchini, vitakutana jijini Arusha kuanzia Oktoba 8 hadi 10 mwaka huu, kutafakari na kushirikishana namna bora ya kufanikisha adhima ya utoaji wa huduma rafiki na jumuishi za kifedha kwa Watanzania.

Vyama hivyo vinavyoendelea kubadilisha maisha ya watu na kufanikisha ndoto za wananchi hasa wenye kipato cha chini, vinalenga kuwainua kiuchumi, kwa kuwahakikishia kipato endelevu kitakachowawezesha kumudu gharama za maisha.

Jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT Ltd-1992), Dk. Gervas Machimu, alisema vyama hivyo vitakutana katika maadhimisho ya siku ya kimataifa ya ushirika wa akiba na mikopo (Saccos) ambayo mwaka huu, yanafanyika, jijini Arusha.

"Kupitia siku hii, Saccos zote Tanzania zinatafakari namna iliyo bora pia ya kufikisha huduma za fedha vijijini na kutatua changamoto za mitaji kwa wananchi. Maadhimisho ya siku ya kimataifa ya ushirika wa akiba na mikopo yanaitwa International Credit Union Day (ICUD) ambayo hufanyika kila Alhamisi ya tatu ya mwezi Oktoba.

Utamaduni huo ulianza tangu mwaka 1948 huko Marekani kupitia U.S Credit Union National Association na baadaye kusambaa kwenye nchi nyingine kuanzia mwaka 1971, lakini kwa Tanzania tunaadhimisha kwa mara ya 10 sasa."

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo ya kitaifa ni Kaimu Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Tito Haule na yatafungwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga.

Katika taarifa yake, Mwenyekiti huyo wa Sccult Tanzania, maadhimisho hayo kwa Tanzania yametangulia kufanyika ili kutoa fursa kwa Saccos za Tanzania kungana na Saccos nyingine za Afrika katika maadhimisho yatakayofanyika Mombasa, nchini Kenya.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Huduma kwa kijamii, kuufikia ulimwengu'.

# Polisi jamii yawakuta kukamata watuhumiwa

**Na Mwandishi Wetu**

POLISI Jamii wanne wa Kikundi cha Ulinzi Shirikishi Mtaa wa Saranga Kata ya Saranga, wilayani Ubungo jijini Dar es Salaam, wamenusurika kuuawa kwa mapanga na chepe wakati wakiwakamata watu wanaodaiwa kuchimba mchanga mtoni.

Tukio hilo linatajwa kutokea Jumatatu mchana katika eneo la Mto Ruhanga kwa Nguogani lililopo mpakani kati ya Mtaa wa Saranga na Msingwa wilayani Ilala. Kamanda Mkuu wa Kikundi hicho, Mdoe Kissu, alisema walipokea taarifa kuna gari limeegeshwa katika eneo hilo linajazwa mchanga.

Kissu alisema kuwa aliongozana na wenzake Karim Tarimo, Thadei Simba na Alfani Miho, walipofika walikuta watu kadhaa wakiwa na chepe wakikusanya mchanga.

"Tulifanikiwa kumnasa mmoja na kumfunga pingu, lakini waliitana wakajikusanya na kuzusha purukushani tulipoanza kuondoka, mtuhumiwa akakimbia na pingu kuelekea Mtaa wa Msingwa ambapo tulianza kumkimbiza," alisema.

Alisema kutokana na mazingira hayo, walijikuta wamevuka mto ambao ndiyo mpaka.

Alisema ghafla Miho alivamiwa na watu wenye mapanga na chembe na kuanza kumshambulia, ndipo akamfuata ili kumnusuru, lakini akajikuta naye anashambuliwa na kujeruhiwa.

"Hapo ndipo tukagutuka kuwa tumeingia kwenye hatari, maana tulijikuta tunashambuliwa, mara polisi mmoja aliyevalia kiraia alifika, akawaamuru waache, kisha akataka tumwonyeshe vitambulisho vyetu, tukamuonesha, lakini katika hali ya kushangaza, akaanza kutufokea," alisema Kissu.

"Alituambia sisi tunavunja amani, tukamjulisha kilichotokea, mtuhumiwa wetu akaletwa tukaamliwa tumfungue zile pingu kisha polisi yule akachukua na kuwafunga wenzetu wawili, huku akimwachia mtuhumiwa, jambo hilo lilitufedhehesha," alisema. Alibainisha wakati huo alikuwa anavuja damu kutokana na jeraha usoni mwake, polisi huyo aliwachukua na kuwapeleka Kituo cha Polisi Stakshari, ambako Mkuu wa upelelezi aliwasikiliza kisha kuwaruhusu kuondoka.

"Kutokana na tukio hilo, tumebaini kwamba kuna mtandao wa aina yake wa uharibifu wa mazingira kwa uchimbaji wa mchanga ambao unahusisha baadhi ya polisi wasio waaminifu, tunaomba Takukuru wamulike ili kusaidia kujua ukweli, " alisema Kissu.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Saranga, Godwin Muro, alisema alifika eneo la tukio ambapo alishuhudia baadhi ya wakazi wa eneo hilo wakishabikia kushambuliwa kwa polisi jamii hao.

Muro ambaye ndiye Mwenyekiti wa Ulinzi wa Mtaa, alisema amewashauri Polisi Jamii kutoa taarifa polisi ili kupata RB itakayowezesha taratibu nyingine za kisheria kufuatwa ikiwamo kutibiwa.

"Uchimbaji wa mchanga kwenye mito ni jambo ambalo linakatazwa kwa kuwa linasababisha madhara, lakini wengine wamegeuza kuwa ni biashara ya kuwaingizia kipato, nimeamua kujipanga kwenda kumuona na kuzungumza mwenyekiti mwenzangu wa mtaa huo ili kuona jinsi ya kukomesha hayo," alisema Muro.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alipoulizwa kuhusu tukio hilo, alisema hana taarifa. Kamanda wa Mkoa wa Polisi Kinondoni, Mussa Taibu, hakupatikana, ikielezwa yupo kwenye semina.



Mkufunzi wa mafunzo ya ujasiriamali, Richard Kiyoba, akitoa maelekezo ya umuhimu wa kujiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali kwa wananchi wa Kijiji cha Mpanyani, wilayani Masasi, mkoani Mtwara jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Mkurugenzi Dar aipa changamoto NMB

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Jiji la Dar es Salaam, Zipora Liana, ameitaka Benki ya NMB kuchangamkia fursa kwa kufungua tawi katika stendi mpya ya mabasi yaendayo mikoani inayoendelea na ujenzi eneo la Mbezi Luis.

Liana aliyasema hayo jana wakati akifungua wiki ya huduma kwa wateja wa NMB katika tawi la benki hiyo lililopo Mlimani City.

Aliipongeza benki hiyo kwa kazi ambayo inaendelea kuifanya.

"Ifikapo Julai mwakani stendi hii itakuwa imekamilika, hii ni fursa nzuri kwenu kufungua tawi kwa kuwa itakuwa inahudumia watu wengi wa ndani na nje ya nchi," alisema.

Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema kauli mbiu ya mwaka huu kwa wiki ya huduma kwa wateja ni 'Magic of service'.

Alisema NMB imeendelea kufanya maboresho ikiwamo kuongeza idadi ya matawi hadi kufikia 230 ambayo yameenea kila wilaya nchini.

"Maboresho mengine tuliyoyafanya ni kufungua ATM 8,000 na tuna mawakala 6,000. Ili kuwafikia wateja wetu wakati wote, tunatarajia kuongeza muda wa kufanya kazi hadi kufikia saa moja usiku kwa matawi ya Kariakoo, Mlimani City na kwa tawi lililopo Kahama mkoani Shinyanga," alisema.

Alisema wameongeza wateja kutoka 6,000 mwaka 2005 hadi kufikia watu milioni 3.5.

Alisema wiki kwa mteja ni fursa ya muhimu kwao kwa ajili ya kumjali mteja na kumhudumia kwa sababu wanapata muda wa kuzungumza nao wale wanaowahudumia.

# Jela kuvamia shamba la kijiji

**Na Happy Severine,** MASWA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wilayani Maswa, mkoani Simiyu, imemuhukumu mtu mmoja kifungo cha miezi 6 jela kwa kosa la kuingia kwenye shamba la kijiji na kuanza kuweka makazi na kufanya shughuli kilimo.

Aliyehukumu ni Tija Kacheli, mkulima mkazi wa kijiji cha Isagenh'e Kata ya Sukuma wilayani Maswa.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Maswa, Fredrick Lukuna, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, alimuhukumu kwenda kutumikia kifungo cha miezi sita jela au faini sambamba na kurudisha shamba hilo kwa wanakijiji.

Awali Mwendesha Mashtaka, Rashidi Achimtole, aliiambia mahakama mtuhumiwa alitenda kosa hilo Septemba 8, 2018, majira ya asubuhi katika kijiji cha Isagenh'e.

# Wajengewa bwalo chakula kwa mil. 66/-

**Na Alipius Mchucha,** NJOMBE

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Madunda, iliyopo Kata ya Mawengi wilayani Ludewa Mkoa wa Njombe, wameondokana na adha ya kukosa sehemu ya kulia chakula baada ya kujengewa bwalo.

Bwalo hilo la chakula lenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 66, lilijengwa na Shirika lisilo la kiserikali la Southern Highlands Participatory Organization (SHIPO) na kukabidhiwa kwa uongozi wa shule mwishoni mwa wiki iliyopita.

Akikabidhi jengo hilo, Mratibu wa mradi wa Mawengi, Mlangali, Milo, Intergrated Education (MAMMIE) toka Shipo, Nemes Temba, alisema, kuimarishwa kwa miundombinu ya majengo shuleni kutachochea kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu.

"Kabla ya utekelezaji wa mradi huu, hali ya ufaulu ilikuwa asilimia 61 kwa mwaka 2017, lakini baada ya uboreshwaji wa miundombinu katika shule 20 zilizopo katika kata nne za Mawengi, Milo, Mlangali na Lubonde hali ya ufaulu kwa mwaka 2018 imepanda na kufikia asilimia 74," alisema Temba.

Mratibu huyo alisema, shirika lenye makao makuu yake mkoani Njombe, linatekeleza mradi huo katika shule 20 zilizopo kwenye vijiji 15 na kata nne wilayani Ludewa.

Alisema serikali imeamua kutoa elimu bure kwa shule za msingi na sekondari, hiyo na wao wanaunga mkono ili kuhakikisha changamoto za upungufu wa vyumba vya madarasa, vyoo, nyumba za walimu, majiko na mabwalo ya chakula mkoani Njombe zinatatuliwa.

Akipokea jengo hilo, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Ditram Chaula, aliwaomba wadau wengine wa elimu kuunga mkono juhudi za Shipo ili kutatua changamoto zilizopo kwenye shule za msingi na sekondari.

## Watoto 37,000 kuchanjwa polio

**Na Sabato Kasika**

WATOTO 37,120 wanatarajia kupatiwa chanjo ya surua-rubella na polio wilayani Nachingwea mkoani Lindi, kwenye kampeni ya siku tano ya kutoa chanjo, inayotarajiwa kuanza wiki ijayo.

Hayo yalisemwa jana na Mganga Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Dk. Joseph Mtabho, katika kikao maalum cha kuwatambulisha wajumbe wa kampeni hiyo kwa mkuu wa wilaya hiyo, Rukia Muwango.

"Kampeni hii itafanyika kwa siku tano kuanzia Oktoba 15 hadi 19 mwaka huu na tunatarajia watoto 22, 957 wenye miezi mitano hadi 59 watapata chanjo ya surua-rubella," Dk. Mtabho alisema. Pia aliwataja watoto wengine kuwa ni 14, 163 wenye umri wa miezi 18 hadi 42, ambao wanatarajiwa kupewa chanjo ya polio, huku akiwaondoa hofu wajumbe kuwa chanjo hiyo haina madhara makubwa.

"Yapo madhara madogo, ambayo hayana athari na yanadumu kwa muda wa saa 24 na kama yataendelea, mhusika atatoa taarifa kwenye kituo cha kutolea huduma ili kupata msaada zaidi ya kitabibu," alisema. Akizungumza katika kikao hicho baada ya kukaribishwa, Mkuu wa wilaya hiyo, Rukia Muwango, aliwataka wajumbe wa kamati za afya ya msingi kuhamasisha wananchi kupeleka watoto katika vituo vya kutolea huduma ya chanjo.

"Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imeandaa kampeni ya kitaifa, hivyo wajumbe hamasisheni wananchi," alisema Muwango.

## Wito kusoma masomo sayansi

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

KATIKA kuhakikisha kuwa serikali inafikia katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, wanafunzi wametakiwa kuhakikisha wanasoma masomo ya sayansi ili kuepuka kuagiza wataalamu wa viwanda kutoka nje.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa, aliyasema hayo jkatika mahafali ya 10 ya Shule ya Sekondari ya Sister Irene Halmashauri ya Mji wa Kahama na kuongeza kuwa kama watu wataajiriwa kutoka nje ya nchi, serikali haitakuwa na faida yoyote.

Kwandikwa ambaye pia ni Mbunge wa Ushetu, alisema kama Tanzania itafikia uchumi wa kati kwa kutumia wataalamu kutoka nchini basi, itakuwa ni nafuu kwa serikali, huku ikitumia gharama ndogo hata katika kuwalipa mishahara watumishi wake.




Mfanyausafi akisukuma toroli lililojaa takataka baada ya kusafisha katika Barabara ya Shaaban Robert, Kata ya Kivukoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Tanzania, Uingereza zajadili mazito kilimo

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara, imemhukumu kunyongwa hadi kufa Mohamedi Omari (45), iliyompata na hatia ya kumuua kwa kukusudia Andrew Ndemba, kwa madai ya kumnyima supu ya kuku.

Omari maarufu Mang'oro ni mkazi wa Kata ya Chikonji katika Manispaa ya Lindi, alihukumiwa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Paul Ngwembe, baada ya ushahidi uliotolewa dhidi yake kuthibitishwa bila shaka kuwa alitenda kosa hilo.

Baada ya Jaji Ngwembe, kumtia hatiani, mshtakiwa aliulizwa kama ana neno litakaloishawishi mahakama isimpe adhabu kali kutokana na kutiwa hatiani.

Aidha, alijitetea kwa kuiomba isimpe adhabu kali akisema ni mkosaji wa mara ya kwanza, lakini pia anayo familia inayomtegemea akiwamo mke na mtoto na alifanya hivyo kutokana na kupitiwa na shetani.

Wakili wa Serikali, Emmanuel John, aliiomba mahakama impe adhabu kali ili iwe fundisho kwake mshtakiwa na watu wengine walio na moyo usio wa kibinadamu dhidi ya wenzao.

Jaji Ngwembe akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 48/2016, alimhukumu kunyongwa hadi kufa licha ya utetezi wake.

Mwanzoni ilielezwa mahakamani hapo na wakili wa serikali, Emmanuel John, kuwa Mang'oro alifanya mauaji hayo Aprili 07 mwaka 2016 usiku, baada ya Ndemba, aliyekuwa akiitwa kwa jina la utani Mtanzania kukataa kumnunulia supu ya kuku.

Alisema siku hiyo ya tukio, Mang'oro akiwa ameongozana na mpenzi wake walifika nyumbani eneo inapouzwa supu ya kuku na kumkuta Mtanzania na rafiki yake aitwaye Barnaba wakiendelea kunywa supu hiyo.

Mfungwa huyo alimwomba amnunulie supu lakini alimjibu kuwa hana fedha.

John alisema majibu hayo yalimchukiza mshtakiwa Mang'oro, ndipo mzozo ulipoanza huku akimpa kauli za vitisho kuwa atamwonyesha.

Mtanzania alilipiga teke sufuria la supu, kisha kuondoka eneo lile akiwa na rafiki yake mwingine Issa Abdallah, kuelekea nyumbani kwao wakitumia baiskeli.

Alisema wakiwa wanaelekea nyumbani kwao, Mang'oro alichukuwa panga na kwenda kuwavizia njiani akijificha eneo ambalo walikuwa wanapita mara kwa mara na walipokaribia aliwasimamisha.

Hata hivyo walipomtambua waliongeza mwendo lakini katika kukimbia huko Ndemba au Mtanzania alidondoka.

Wakili wa serikali alisema kitendo cha Mtanzania kudondoka kulitoa nafasi kwa mshtakiwa kumshambulia kwa kumkatakata na panga maeneo mbalimbali ya mwili wake, ikiwamo kichwani na kupoteza damu nyingi na mwisho kufariki maisha yake.

Alisema mshtakiwa aliacha kumshambulia baada ya kuona watu akiwamo Issa Abdallah kufika eneo la tukio na kuanza kumkaripia.

Aliangusha panga kukimbilia nyumbani kwake, lakini usiku huo alikamatwa na polisi na taratibu za kumfikisha mbele ya sherria zilianza hadi alipohukumiwa jana.

## Mtuhumiwa rushwa akamatwa msibani

**Na Romana Mallya**

OFISA Afya Mkuu na Mratibu wa mradi wa Belgian Fund for Food Security (BFFS), Emmanuel Mziwanda wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, aliyekuwa akisakwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) tangu Julai 2017, amekamatwa msibani.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema mtuhumiwa Mziwanda alikuwa akitafutwa kwa makosa ya kutumia nyaraka kumdanganya mwajiri na kuisababishia hasara Serikali ya Sh. Milioni 15 ambazo alizipata kwa njia ya udanganyifu.

Alisema baada ya kufanya uchunguzi wao na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kutoa kibali cha kumfikisha mahakamani Mziwanda, alitoweka hadi mwezi huu alipokamatwa wilayani Mpwapwa akiwa msibani.

Alisema taasisi hiyo inawashukuru wananchi na wadau kwa ushirikiano hadi kufanikisha kukamatwa kwake.

Alisema Mziwanda atafikishwa mahakamani muda wowote baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Hata hivyo, alisema katika robo ya Julai hadi Septemba 2019, ofisi yake imeendelea kutoa elimu ya rushwa kwa wananchi na kwamba imefuatilia miradi 39 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. Bilioni 46 katika sekta za ujenzi wa miundombinu, elimu, afya, maji na kilimo.

"Tumegundua viashiria vya uwepo wa uvunjaji wa taratibu kwenye utekelezaji wa miradi minne yenye thamani ya Sh. Bilioni 1.9," alisema.

Aidha, alisema kutokana na hali hiyo wameanzisha uchunguzi ili kuona iwapo kuna vitendo vya rushwa katika miradi hiyo.

Alisema katika eneo la kupambana na rushwa kwa kipindi tajwa, wamepokea jumla ya tuhuma 155.

"Makosa yahusianayo ambapo uwiano wa tuhuma hizo kisekta ni kwa asilimia ni kama ifuatavyo, kata, mitaa na vijiji 39, Ardhi 13.5, Elimu 12.3, Mahamama 7.7, Wizara 5.8, Polisi 5.2, sekta binafsi 5.2, Maji 4.5, ambapo tuhuma zilizobakia zinahusu sekta ya afya, Uhamiaji, Tarura na vyama vya siasa," alisema.

# Wakamatwa na tani kadhaa za vinyago

Na Friday Simbaya, KILOLO

MWENYEKITI wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah, ameongoza ukamataji wa zaidi ya tani mbili za vinyago zilizokuwa zimefichwa kwenye msitu wa Ruaha mkoa wa Iringa.

Mkuu wa Wilaya, Ofisa Misitu Wilaya Tullah Abong'o na Mkuu wa kituo cha polisi Ruaha Mbuyuni Prosper Ng'oro walishiriki msako na ukamataji huo.

Alisema vinyago hivyo vinaendelea kufanyiwa tathimini ili kujua thamani yake na watuhumiwa kadhaa wanashikiliwa na polisi. Mkuu wa Wilaya, alisema vinyago hivyo vimetengenezwa na mpingo unaotakiwa kulindwa. Alisema watuhumiwa, hawakuwa na vibali vya umiliki vya kusafirishia tena hawakuwa na cheti cha kuonyesha vinyago hivyo zinazotoka nchi gani wala hawajasajiliwa.

Aidha, hawakulipia tozo za serikali, hawakuwa na nyaraka zinazothibitisha chanzo cha shehena hiyo imevunwa wapi.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji (kushoto), akiwasikiliza walipakodi waliokuwa wakisubiri kupatiwa huduma katika Ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: WFM**

# Mwanjelwa awataka kuboresha utumishi

Na Neema Emmanuel, MWANZA

SERIKALI imewataka watumishi wa umma kuwa watiifu, wabunifu, wavumilivu na wanaozingatia uzalendo wanapowahudumia wananchi.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Dk.Mary Mwanjelwa, ametoa agizo hilo, wakati akizungumza na watendaji wa taasisi za umma.

Alisema licha ya kuwa changamoto zipo, wanatakiwa kutumia utaalamu na weledi kuleta mabadiliko chanya mfano, eneo lisilo na mapato yaongezeke, penye utovu wa nidhamu kuwe na maadili na heshima iwepo.

Dk.Mwanjelwa, alisema kitendo cha mamlaka za nidhamu kutozingatia sheria, kanuni na taratibu wakati wa kushughulikia masuala ya nidhamu kinaisababishia serikali hasara.

Alifafanua kuwa inatokea pale serikali inapolazimika kuwalipa watumishi mishahara ambayo hawakifanyia kazi ikiwa pamoja na kuanzishwa upya kwa mashauri hayo na watumishi kurejeshwa kazini.

"Kutokana na kitendo hicho nawaagiza watendaji wakuu wa taasisi zote za umma kuhakikusha kwamba mashauri ya nidhamu yanaendeshwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma,hivyo wale ambao watakiuka, Tume ya Utumishi wa Umma, izijulishe mamlaka zao za nidhamu ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi yao mara moja," alisema.

Naibu Waziri aliyasema hayo kwenye mkutano na watendaji wa taasisi za umma mkoani Mwanza na kusema wananchi wote wanahitaji huduma mbalimbali kutoka serikalini na watumishi wa umma ndiyo wahusika.

Alisema ili kufanikiwa kutekeleza hilo wanapaswa kufanya kazi kwa utii na kuzingatia sheria na si mazoea.

Aidha aliwaagiza waajiri kuwaelimisha wafanyakazi kuhusu mfumo wa kujitathimini kazini wa OPRAS ili waweze kuielewa na kutekeleza kikamilifu.

Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Christopher Kadio, alisema, manufaa ya mkutano huo ni kufumbuliwa macho kwa kuwajengea uelewa.

# Wananchi walilia elimu ya uchaguzi

Na Jumbe Ismailly, MANYONI

KUKOSEKANA kwa elimu ya mpiga kura pamoja na uhamasishaji duni wa wanawake kugombea nafasi za uongozi wilayani Manyoni Mkoa wa Singida, ni changamoto inayowarudisha nyuma wagombea wanawake.

Hali, hiyo ndiyo inayotishia kuwepo kwa wagombea wanawake wachache kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Mmoja wa wajasiriamali wadogo katika mji mdogo wa Manyoni, Sarah Mdoma alisema hayo kufuatia taarifa ya Ofisa Uchaguzi wa Wilaya ya Manyoni, Edina Palla, ikitaja idadi ya wapiga kura. Palla aliwaeleza wajumbe wa mkutano wa kawaida wa robo ya nne wa Baraza la Madiwani kwamba Wilaya ya Manyoni inatarajia kuandikisha wapiga kura 84,637 wanaume 39,892 na wanawake 44,745 waliopo katika vitongoji 279 na vijiji 58.

Mdoma alisema idadi kubwa ya wanawake inaridhisha, lakini wanapopatiwa elimu huwavusha kutoka sehemu moja kwenda nyingine ikilinganishwa na wanaume. Hata hivyo alilalama kuwa mpaka sasa serikali ya wilaya hiyo haijawapatia elimu hiyo. "Na unavyojua kwamba wanawake tukipata elimu ya kutosha siku zote tunavuka tunaweza hata kuwapita hata wanaume, lakini elimu ni bado hatujapatiwa kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa bado ni kimya kwa hiyo wanawake huenda wasihamasike,"alisisitiza Mdoma. Aliwatahadharisha wanaume wanaotarajia kuingia katika kinyang'anyiro cha uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji hata ule mkuu wa mwaka 2020, kuwa wajipange kwani kuna wanawake wenye elimu ya kutosha na wana uchungu wa kuongoza wananchi na wenye uchungu wa kuwatetea wanawake na wahitaji wengine.

# Waazimia kuuza chaki nchi nzima

Na Hamis Nasiri, LINDI

WAJASIRIAMALI wadogo wa Kijiji cha Mpanyani wilayani Masasi mkoani Mtwara, wameanza kutengeneza chaki kupitia mradi wa kiwanda kidogo.

Lengo la ujasiriamali huo ni kuzifikia shule zote za umma za wilayani hiyo na nyingine za Tanzania nzima ili zitumie chaki zinazotoka kwenye kiwanda chao.

Aidha, wajasiriamali hao wameamua pia kuanzisha kampuni yao ya Mpanyani ambayo itafanya shughuli mbalimbali za uchakataji wa mazao ya kilimo ikiwemo ukamuaji wa mafuta ya alizeti na kusindika muhogo

Hayo yalibainishwa jana wilayani Masasi na Katibu Mtendaji wa Mpanyani, Abilahi Nampali, wakati alipokuwa akizungumza na wanachama wa kikundi hicho kwenye hafla ya kumaliza mafunzo ya ujasiriamali,yaliyofanyika katika kijiji cha Mpanyani Masasi.

Alisema kama wajasiriamali wadogo wameamua kuanzisha kiwanda kidogo cha kutengeneza chaki ambazo wataziuza kwa bei nafuu ili waweza kujipatia kipato na kwamba kazi hiyo imeshaanza.

Nampali alisema mashine waliyonayo inatengeneza chaki zaidi ya 400 kwa mkupuo mmoja hivyo kwa mwezi wana uwezo wa kuzalisha chaki zaidi ya boks 20 hadi 30. "Changamoto kubwa kwetu ni mtaji pamoja na malighafi hivyo tunawaomba wadau watuunge mkono hasa taasisi za kifedha kutupatia mikopo ili tuweze kutimiza azma yetu," aliomba Nampali

Alisema lengo la kutengeneza chaki hizo kwa kutumia kiwanda chao kidogo ni kuweza kusaidia kuondokana na changamoto ya kifaa hicho cha kufundishia shuleni.

"Hizi boksi za chaki tulizotengeneza tunaanza kutafuta soko katika shule zetu hapa kijijini ili zikisifiwa ubora wake hapo tutatafuta masoko Tanzania nzima- nje ya wilaya yetu," alisema Nampali Akisoma risala ya kikundi hicho mmoja wanachama hao, Amina Hamisi alisema changamoto waliyonayo kwa sasa ni mahitaji ya chaki ni makubwa lakini mashine wanayotumia kutengeneza chaki ni hizo ni ndogo "Mashine yetu ni ndogo hivyo chaki tunazotengeneza haziwezi kukidhi mahitaji ya soko tulilonalo tunaomba wadau watusaidie ili tuweze kufikia malengo yetu," alisema Hamisi

Alisema kwa tafiti walioifanya wamegundua kuwa kumekuwa na uhaba mkubwa wa viwanda vya chaki nchini hivyo kutokana na hilo wao wameamua kubuni kiwanda cha kutengeneza chaki hizo. Mkufunzi wa mafunzo hayo ya ujasiriamali kutoka Dar es Salaam,Richard Kiyabo, aliwaomba wananchi wa Mpanyani kujiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali ili waweze kutimiza ndoto zao za kuondokana na umaskini.

# Mkulima bora atoa ya moyoni

**Na Restuta Damian**, KYERWA

BAADHI ya wadau wa kahawa akiwamo mkulima bora wa kahawa wilayani Kyerwa mkoani Kagera, wameiomba serikali kuwapatia elimu ya kisasa ya kulima kahawa.

Waliyasema hayo kwenye maadhimisho ya siku ya kahawa duniani, ambayo kitaifa yamefanyika wilayani humo. Kyerwa inaongoza katika uzalishaji wa kahawa ya robusta na arabika zinazouzwa katika soko la dunia. Albert Katagira, mkulima bora kitaifa kutoka Kata ya Isingiro wilayami humo alisema kuna umuhimu wa wakulima kuelimishwa ili waachane na umazoea.

Alisema ni muhimu kwani mataifa mengine yanatumia mifumo ya kiteknolojia kujipatia tija na ongezeko la mavuno tena yenye ubora.

Katagira alisema wakulima wamekuwa wakilima kwa kufuata mazoea na kufanya vile wanavyoona hali inyosababisha kukosa mazao yenye tija na ufanisi yanayoshindana kibiashara. Aidha, Katagira alisema mkulima anatakiwa kupatiwa namna bora ya kilimo kuanzia kwenye uandaaji wa shamba, upandaaji, uvunaji na uhifadhi wa mavuno, mambo hayo yatamsaidia kuondoa ushushwaji wa bei hiholela unaotokea sokoni.

"Sisi wakulima bado hatujaweza kusimama pekee yetu ndiyo maana tunashindwa kwani tunatumia mazoea ya kiurithi, tukijua hayo yatatusaidia," Juma Paschal mkulima wa kata Chonyonyo alisema, ili waweze kufanikiwa na kuwa kama wakulima wengine wa mikoa ya Ruvuma, Kilimanjaro, Songwe na Mbeya wanahitaji utaalamu.

Alisema mashamba yamekuwa na upungufu na kuna magonjwa na wadudu waharibifu kwani mkulima anaonyesha kila jitihada za kuweka mbolea ya kukuzia na hufanikiwa kwa kutumia uzoefu usio na elimu ya wataalamu licha ya kahawa kuwa na ubora wa ushindani.

Mwonjaji wa kahawa Kanda ya Ziwa, Jimmy Mchau, alisema ili kupata mafanikio lazima mkulima atumie hatua za uandaaji ,uvunaji, uanikaji na uchambuaji.

Mchau alisema , kahawa ina umuhimu wake katika matumizi ya binadamu hasa mwilini huzuia magonjwa ya sukari na kuweka akili vizuri, hutibu figo, endapo itaandaliwa vyema kuanzia kwa mkulima hadi sokoni iwe kitaifa na kimataifa.

Kwa upande wake Meneja wa Bodi ya Kahawa Kanda ya Kagera Merickyod Massawe, alisema ,changamoto iliyopo kwa sasa ni uzalishaji kwani uwekezaji wa mkulima ni mdogo na usiotosheleza.

# Wanaodhalilisha watoto mitandaoni kukomeshwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

OFISI ya Ustawi wa Jamii, Halmashauri ya Mji wa Kahama, ametangaza nia ya kuwachukulia hatua za kisheria watakaobainika kurusha picha za kumdhalilisha mtoto kwenye mitandao.

Abrahamani Nuru, Ofisa Ustawi, alionya kuwa sheria zinakataza kuwaonyesha hadharani watoto waliofanyiwa vitendo vya ukatili kwenye mitandao ya kijamii.

Nuru aliyabainisha hayo jana katika warsha ya siku mbili ya kuzijengea uwezo, kamati za mipango wa kitaifa ya kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA).

Mafunzo hayo yanazijumuisha kata tano na kugharamiwa na The Foundation for Civil Society na kutekelezwa na shirika la Uheso Foundation la mjini hapa.

Alisema kitendo cha kurusha picha ya mtoto au mwanamke aliyefanyiwa vitendo vya kikatili sio njia ya kumsaidia bali ni kuendelea kumdhalilisha tena kwa kasi kupitia mitandao.

Alionya kuwa ili kukomesha jambo hilo atawachukulia hatua za kisheria watuhumiwa.

Aidha Nuru alisema, Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 kifungu cha 158 (i)kinamkataza mtu yoyote kurusha picha za mtoto aliyefanyiwa vitendo vya kikatili kwenye mitandao ya kijamii na akibainika atatozwa faini isiyopungua 500,000 au kwenda jela miezi sita au vyote kwa pamoja.

"Kwasasa kila mwananchi anajifanya ni mwandishi wa habari wa kurusha kila jambo analoliona mbele yake. Halikubaliki tutachukua hatua za kisheria ujumbe utakaorushwa wenye picha ya mtoto au mwanamke aliyefanyiwa ukatili kwenye mitandao," alisema Nuru.

Hata hivyo, alionya kuwa, njia ya kumsaidia mtoto au mwanamke aliyefanyiwa vitendo vya kikatili ni kutoa taarifa kwenye ofisi za ustawi wa jamii ama dawati la jinsia lililopo kituo cha polisi na sio kumpiga picha za mitandaoni.

Kwa upande wake Ofisa Maendeleo wa Kata ya Kagongwa, Witiness Mlayi, alisema kata yake inaongoza kwa ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na wanawake na kwa siku hupokea mashauri nane hadi 10 ya ukatili.

Alisema wamekuwa wakiwapiga faini ya mfuko mmoja wa saruji wazazi ambao wanabainika kuwa na watoto mitaani na huku umri wao ukiwahitaji kuwa shuleni.



Mbunge wa Viti Maalumu (CCM) Mkoa wa Singida, Aysharose Mattembe (katikati), akikabidhi msaada wa vifaa vya ofisini vyenye thamani ya Sh. milioni 7.3 kwa Mwenyekiti wa chama hicho (CCM) Mkoa wa Singida, Alhaji Juma Killimba juzi, kwa ajili ya kusaidia kurahisisha utendaji wa kazi wa Jumuiya za chama hicho. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# Madiwani wamchimbia mkwala Mkurugenzi

**Na Happy Severine,** BARIADI.

MADIWANI wa Halmashauri ya mji wa Bariadi mkoani Simiyu, wamemtaka Mkurugenzi wa Halmashauri, Merckzedec Humbe, kushughulikia mara moja huduma mbovu ndani ya hospitali ya wilaya.

Wametaja tatizo la huduma mbovu , lugha chafu za wahudumu na uzembe katika hospitali hiyo ya wilaya ya Somanda.

Malalamiko mengine yalikuwa ni lugha chafu kutoka kwa wauguzi, huduma mbovu kwa wagonjwa wanaolazwa, kutowaona madaktari wa zamu pamoja na kukosekana tiba.

Walitoa wito huo jana katika kikao cha Baraza la Madiwani, kilichofanyika mjini Bariadi.

Walieleza kuwa wananchi wanalalamikia kukosa haki za msingi ambazo ni huduma bora za afya. Akitoa tamko hilo Mwenyekiti wa Halmashauri, Robert Rweyo, alisema kutokana na hali hiyo Mkurugenzi wa Halmashauri anatakiwa kuwajibika.

Walimtaka kuchukua hatua kabla hawajaunda kamati maalum ya kuchunguza kero hizo kiundani. "Malalamiko yamekuwa mengi na wananchi wetu wanapata shida mno wanapokwenda hospitalini hapo. Hivyo kabla hatujaliingilia kati sisi madiwani ,tunamtaka mkurugenzi wetu aanze kulishughulikia suala hilo kwa kuchunguza kero zilizopo na kuziondoa maana zimekuwa sugu, " alisema Rweyo

"Kero hizo si tu nazisikia kwa watu...hapana hata mimi nimekutana nazo wakati tulipompeleka mwenzatu diwani alipopata ajali. Tulihangaika sana na kuzungushwa, huku madaktari wakitukwepa, hivyo hatua ilipofikia ni mbaya,"aliongeza.

Veronica Kinyemi, Katibu Tawala wa Wilaya ya Bariadi, alisema sio siri huduma zinazotolewa katika hospitali ya Wilaya ya Somanda ni mbaya mno.

Alisema wahudumu wana lugha mbaya zinazokatisha tamaa na kutibua wagonjwa waliolazwa hospitalini hapo.

Alisema walilifuatilia suala hilo kwenye x-ray ya ultra sound ilipoibiwa katika wodi ya kinamama lakini cha kushangaza waliambiwa wanaingilia masuala ya kitaaluma zaidi.

"Mkurugenzi wa Halmashauri anatakiwa kufanya kazi ya ziada kuhakikisha anasafisha na kuondoa kero lukuki zilizopo hospitalini hapo...la sivyo wananchi wengi wataendelea kuteseka na hata kupoteza maisha kwa uzembe."

Aidha, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri, Christopher Legonda, amelihakikishia baraza la madiwani kuwa atalishughulikia suala hilo na kuwapa mrejesho.



Ukurasa 20

Chuo Kikuu Nelson Mandela chakomboa wakulima, mifugo



Ukurasa 14

Ufadhili wa EU mpunga shambani wapaishwa kupitia 'Kilimo Shadidi'

BUFE

Ijumaa Oktoba 4, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 19

## Kikundi vijana chafungua mlango wa ajira kupitia utotoaji kuku

# Faru Mweusi anavyochochea upekee Hifadhi Ngorongoro



**Na Woinde Shizza,** Ngorongoro

MOJA ya maeneo yaliyomo kwenye orodha ya maajabu saba ya dunia ni Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, yenye vivutio vingi vya utalii, akiwamo Faru Mweusi.

Hifadhi hiyo ina mamlaka inayojitegemea kwa kuwa na majukumu tofauti yanayolenga kuhifadhi viumbe hai na makazi endelevu kwa ajili ya vilivyopo na vijavyo.

Upekee wa Ngorongoro, unatokana na jinsi lilivyo eneo lenye hifadhi mseto, ambavyo kuna viumbe hai vya aina tatu vinavyoishi kwa pamoja, yaani watu, mifugo na wanyamapori.

Hillary Mushim ni Naibu Kaimu Kamishna wa Uhifadhi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, anaeleza mambo yanayohusiana na mnyama huyo aina ya Faru Mweusi na tabia zake zinavyoonekana, sehemu anakopatikana mna hata thamani yake.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## EU katika changamoto Uingereza na Marekani

Ukurasa 15

UCHUMI

MAMBO YA KILOSA & MVOMERO

# Ufadhili wa EU mpunga sham wapaishwa kupitia 'Kilimo S

• Waliopata gunia nane sasa 40 • Hasara 40% yashuka hadi 25%
• Wakulima 15,000 katika vijiji 36



Wakulima na wanavikundi wanaolima mpunga katika kata ya Kilangali, Kilosa wakiangalia ghala la kuhifadhi mpunga, lililofanyiwa ukarabati kupitia mradi wa Ripoma, **PICH**

**Na Ashton Balaigwa,** Morogoro

SERA ya Taifa ya Kilimo inabainisha kuwa mpunga ni zao lenye fursa kubwa ya kuongeza pato kwa Taifa na takribani robo ya uzalishaji kitaifa, inatoka mkoni Morogoro, hasa katika wilaya zake za; Mvomero,Kilosa na mkoa Mbeya, huko wilaya za Kyela na Mbarali, ndizo zinang'ara.

Wakulima wa Kilosa na Mvomero, wamekuwa wazalishaji wakubwa wa mpunga, kuchangia upatikanaji na usalama wa chakula, ziada ikiuzwa nje ya mkoa.

**KILIO MOROGORO**

Katika wilaya za Kilosa na Mvomero, licha ya wakulima kuwa wazalishaji wakubwa wa mpunga kuliko mazao mengine ya nafaka, wamekuwa wanakabiliwa na changamoto, ikiwamo kukosa elimu bora ya kilimo na uelewa mzuri wa kutumia kanuni bora za kilimo cha mpunga, wakiegemea uduni wa njia za kienyeji.


Katibu wa Vikundi vya Wakulima Wadogo wa Mpunga katika kata ya

> **"Lengo ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema na wanaendelea kuendesha shughuli za kiuchumi.**



Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgoy (wa pili kutoka kushoto),akipata maelezo jinsi ya kuhifadhi mpung kuhifadhia mpunga, Kata ya Kilangali. **PICHA ZOTE: ASHTON BALAIGWA,MOROGORO**

# nbani hadidi'



IA ZOTE: ELIZABETH ZAYA



a kutoka kwa msimamizi wa ghala la

Hembeti Mvomero, Aliphonce Maziku,anaiambia Nipashe kwamba matumizi ya mbegu za kienyeji imechangia wakulima wengine kutumia mbegu nyingi na majim, huku wakiambulia kuvuna kidogo, wastani wa gunia nane mpaka 15 kwa ekari moja.

Anaeleza changamoto nyingine ni hifadhi ya mpunga, kwani ghala iliyokuwapo imechakaa, kuta zake zina nyufa, sakafu chakavu na paa ni fupi, hali inayosababisha kuwapo joto kali ghalani.

Pia, kasoro nyingine inahusu kutokuwapo vifaa kama mizani, kipimo cha unyevu,vifaa vya kuzimia moto na elimu kwa viongozi wa ghala bado iko chini.

Katibu huyo wa vikundi vya wakulima, anataja changamoto nyingine ni ukosefu wa fedha za kuendesha kilimo na wanalazimika kupata mkopo wenye riba kubwa, kutoka kwa wafanyabiashara.

Inaelezwa mpango uliopo ni kwamba mkulima anakopa Sh.30,000 na mwanzo wa msimu itamlazimu wakati wa mavuno kulipa gunia moja la mpunga la debe nane, bila ya kujali bei ya soko kwa wakati huo.

Changamoto nyingine iliyokuwa inawakabili wakulima wa mpunga ni pamoja na upotevu mkubwa wa zao la mpunga wakati wa kuvuna kutokana na elimu duni ya matumizi ya zana bora za kuvuna na kushindwa kuvuna kwa wakati sahihi hatua inayowafanya wakulima kupata hasara na kukata tama na kuendelea na kilimo.

**WAKULIMA KILOSA**

Kiongozi wa vikundi vya wakulima katika Wilaya ya Kilosa, Mohamed Issa,anasema wakulima hao wa mpunga wamekabiliwa na changamoto ya uzalishaji duni wa zao hilo, kwa sababu ya kukosa mbinu bora za kilimo cha kisasa .

Anasema pamoja na kuzalisha zao hilo kwa kutumia kilimo kisichokuwa na tija, lakini wanakabiliwa na changamoto ya uhakika wa soko unaotokana na wafanyabiashara anaowaita 'walanguzi' wanaotaka kununua mazao shambani kwa bei ya chini .

Issa anasema wanakabiliwa na matatizo ya kuhifadhi mpunga, kutokana na uchakavu wa maghala yanayokabiliwa na upugufu mbalimbali, hatua inayochangia kudhulumiwa na walanguzi wanaonunua mpunga kwa bei wanayotaka.

**MRADI RIPOMA?**

Kutokana na changamoto zinazowakabili wakulima wa wilaya hizo, mradi wa kupunguza upotevu wa zao la mpunga wakati na baada ya mavuno unaofahamika kama (Ripoma ) unaoendeshwa na shirika la Helvetas Tanzania, ulianza mkakati wa kuwasaidia walima mpunga wa wilaya hizo mbili za Kilosa na Mvomero.

Meneja Mradi wa Ripoma, Grayson Ferdinand, anasema baada ya kubaini changamoto zinazowakabili wakulima, waliamua kuanza kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga maarufu kama 'Kilimo shadidi' kupitia Chuo cha Wakulima Mkindo.

Hiyo inajumuisha mafunzo ya kuongeza thamani zao la mpunga (mchele joto), mafunzo ya kuzuia upotevu wakati na baada mavuno wa zao la mpunga

Ferdinand anataja mafunzo mengine yaliyotolewa kwa wakulima hao wa mpunga Kilosa na Mvomero ni pamoja na kuweka na kukopa na usimamizi wa mikopo, kuchagua na kupanga kusimamia miradi mbalimbali.

Pia anataja njia nyinginezo ni namna ya uendeshaji ghala kwa kamati zinazosimamia maghala na zimamoto wakati wa dharura na mazingira, masuala mtambuka na uongozi wa vikundi na kusuluhisha migogoro.

Meneja huyo wa mradi, anasema licha ya wakulima kupatiwa mafunzo wamenufaika na ukarabati wa maghala kwa kuongeza urefu wa paa, kuezeka kuweka sakafu, kurekebisha kuta na kupaka rangi, kuongeza ukubwa wa madirisha.

Mengine ni maboresho ya mizani ya kupima magunia ya mpunga, vifaa vya zimamoto na kupimia unyevu inayosaidia vikundi vya wakulima.

Anasema, kupitia mafunzo wakulima wamedhibiti upotevu wa mpunga kabla na baada ya mavuno na wanatambua wakati sahihi wa kuvuna na kutumia nyenzo za kisasa, kuzuia upotevu wa zao hilo inayohesabiwa inaongeza uzalishaji mpunga katika wilaya hizo mbili.

Meneja huyo wa Ripoma, anasema vikundi vyote vya wakulima vimeunganishwa na taasisi za fedha kuweka akiba zao na kuweza kupata huduma nyingine za kibenki kama mikopo, hali iliyochangia wakulima kukopeshana kwenye vikundi vyao kwa riba nafuu, tofauti na awali walikopa kwa watu binafsi kwa riba kubwa.

Mkurugenzi mwekezaji

Mkurugenzi Msaidizi wa shirika la Helvetas Tanzania, Daniel Kalimbiya, anasema zaidi ya wakulima 15,000 kutoka vijiji 36 katika wilaya za Mvomero na Kilosa, baada ya kuwaongezea uzalishaji wa zao hilo kupitia 'Kilimo Shadidi' cha mpunga.

Kalimbya anasema, mradi umesaidia kujenga na kukarabati maghala sita ya kuhifadhi nafaka katika kata Dihombo,Mkindo,Hembeti wilayani Mvomero na kata za Msowero na Kilangali, wilayani Kilosa kupitia ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU).

Anaeleza kuwa, ujenzi wa ma-

INAENDELEA UK.18

# EU katika changamoto Uingereza, Marekani




Ndege ya Air Bus, iliyoleta msuguano wa Marekani na Umoja wa Ulaya.



Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson.
**PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Mwandishi Wetu**

UINGEREZA imetoa wito kwa Umoja wa Ulaya (EU), kuwa wabunifu na utayari wa kufanya mabadiliko kuhusiana na suala la nchi hiyo kujiondoa katika Umoja huo, maarufu kwa msamiati wa Brexit.

Hiyo ni baada ya Waziri Mkuu Boris Johnson, kutoa pendekezo la mwisho la kuingia katika mkataba kuhusiana na mpaka wa Jamhuri ya Ireland.

Kwa mujibu wa waziri anayehusika na suala la Brexit, Stephen Barclay, ilichobaki sasa ni kwa EU kuonyesha kwamba inaweza kuwa na wepesi wa kufanya mabadiliko na ameongeza kuwa Uingereza haitaki kuongezwa kwa muda wa Brexit.

Imani yao ni kwamba, muda ulioko unatosha kuiondoa nchi hiyo kwenye Umoja wa Ulaya, kufikia tarehe mwisho wa mwezi huu, tarehe 31.

Wakati EU inapatiwa salamu hizo jana kutoka Uingereza, Marekani nayo imesema inajiandaa kuziwekea ushuru bidhaa zenye thamani ya Dola bilioni 7.5 zinazotoka EU, ikiwa ni hatua ya kulipiza kisasi ya ruzuku inayoitwa 'siyo halali' ya umoja huo kwa kampuni inayotengeneza ndege ya Airbus.

Tangazo hilo limetolewa saa chache baada ya Shirika la Biashara Duniani (WTO), kuamua mjadala uliodumu kwa miaka 15, kwamba Marekani inaweza kuziwekea ushuru bidhaa za Ulaya, ili kulipiza kisasi ruzuku hizo kwa Airbus, ambazo imekuwa na athari kwa mpinzani wake nchini humo, kampuni ya Boeing.

Inaelezwa kwamba, nchi hiyo inapanga kuweka ushuru wa asilimia 10 kwenye ndege zinazoingizwa kutoka Ulaya na asilimia 25 ya kodi za bidhaa za kilimo na viwanda zinazoingizwa nchini humo ifikapo tarehe 18 mwezi huu.

WTO ilipitisha kiwango cha ruzuku kwa asilimia 100, lakini Marekani iliamua kuweka ukomo.

**Habari na picha zote kwa mujibu wa mtandao.**

UCHUMI

# Faru Mweusi anavyochochea upekee Hifadhi Ngorongoro

• Miaka 4 hajauawa, ulinzi saa 24 • Watalii wanawapenda kupitiliza



Watalii walioko katika Hifadhi ya Ngorogoro wakimuangalia faru mweusi. **NA MPIGAPICHA WETU**

**INATOKA UK.13**

**FARU YUKOJE?**

Pamoja na kuwapo wanyamapori kwenye eneo hilo, Faru Mweusi yuko katika jamii ya wanyamapori wakubwa, kutika familia ya Rhino- Cerotidae.

Faru, anaakisi jina la Kiingereza Rhinoceros au Faru, na sio kifaru ilivyozoeleka kwa baadhi ya watu.

Mnyama huyo ni miongoni mwa wanyamapori watano, wakubwa barani Afrika. Wengine ni Chui, Simba, Mbogo na Tembo.

Nchini Tanzania, Ngorongoro inatajwa kuwa sehemu nzuri ya kuwaona Faru wakiwa kwenye eneo la bonde maarufu kwa jinala Crater.

Wanyamapori hao, wamekuwa wakiongezeka kutokana na ulinzi uliowekwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, huku serikali ikijitahidi kuwalinda wasipotezwe kupitia ujangili.

Hivi sasa serikali imeshawawekea ulinzi maalum wa saa 24 unaofanywa na askari wanyamapori.

> **“Wataalamu wa wanyamapori, wanaeleza kwamba kwa asili, faru ana uwezo wa kuishi miaka 35 hadi 50. Ni tofauti na faru mweusi, mwenye uwezo wa kuishi hadi miaka zaidi ya 55.**

Katika mustakabali wa dunia, Faru wako wa aina tano. Mbali na mweupe na mweusi, aina nyingine tatu, zilizobaki zipo Kusini mwa Bara Asia.

Kwa sehemu kubwa, Faru Mweupe na Faru Mweusi wanafanana na wote wana maumbile yanayovutia kuwatazama.

Ila, Faru Mweusi ni mdogo kimaumbile, kuliko Faru Mweupe na wana mdomo uliochongoka, unaomsaidia kukusanya majani kabla ya kula; Faru Mweusi ana mdomo uliochongoka kuliko Faru Mweupe.

Wataalamu wa wanyamapori, wanaeleza kwamba kwa asili, faru ana uwezo wa kuishi hadi miaka miaka 35 hadi 50. Ni tofauti na Faru Mweusi, mwenye uwezo wa kuishi hadi miaka zaidi ya 55.

Mfumo wa faru kuishi maisha ya kujitenga, huku dume na jike wakikutana katika msimu wa kujamiiana, tena kwa kutafutana kwa njia ya harufu, ambayo inatolewa na jike pale anapomhitaji dume.

Inapotokea hali hiyo, Faru anabeba mimba kwa kipindi cha siku 475 au miezi 16 (mwaka mmoja na robo), japokua kuna wakati hufikisha zaidi ya miezi 18. Kwa kawaida, faru anazaa ndama mmoja na mara chache anapata mapacha.



Faru mweupe na mtoto wake wakiwa mbugani. **PICHA: MTANDAO.**

**NDAMA WA FARU**

Ndama wa faru anapozaliwa mwili wake huwa umefunikwa na manyoya ya kahawia. Manyoya hayo humsaidia kumlinda asichomwe na jua wakati wa mchana na kumkinga dhidi ya baridi nyakati za usiku.

Ndama dume wa faru anapofikisha umri wa miaka miwili na ndama jike anapofikisha umri wa miaka minne huwatoroka wazazi na kwenda kujitegemea. Kitendo hicho kinatoa fursa kwa faru jike kwenda kutafuta dume na kubeba mimba nyingine.

Faru Mweusi anafahamika zaidi kwa umbo lake kubwa na ni miongoni mwa wanyama wanaokula nyasi, huku wakikaribia kuwa na uzito wa tani moja.

Uwezo wa Faru Mweusi kuanzisha himaya yake, inategemea uimara na nguvu za Faru Dume. Kama atakuwa dhaifu, atabaki kukimbizwa kila mahali na faru wanaomiliki eneo husika.

Faru dume huanza kupanda wakati akifikisha umri wa miaka saba, wakati jike anapandwa akiwa na umri wa miaka minne.

Baada ya kitendo hicho, wanyamapori hao huachana na faru dume, kwani anaweza kupanda majike mengi kadri ya idadi iliyopo.

Thamani ya Faru Mweusi ipo zaidi kwenye pembe zake zinazoelezwa kuwa na viinilishe vya protini, sawa na ile inayopatikana kwenye nywele na kucha.

Pia Faru Mweusi, kutokana na jinsi anavyovutia watalii wa ndani na nje, anachangia kuingiza pato la taifa linalotokana na sekta ya utalii.

Maadui wa Faru Mweusi, kama walivyo wanyamapori wengi hasa waliopo kundi la kutoweka, Faru

Mweusi, pia anakabiliwa na changamoto ya ujangili, sambamba na wanaowawinda watoto (ndama) wao kwa ajili ya kitoweo.

**ULINZI WAO**

Hillary Mushi, ni Naibu Kaimu Kamishna wa Uhifadhi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, anaendelea kusema katika kipindi cha miaka ya 1980, kulikuwapo tishio la kutoweka Faru Mweusi lakini ulinzi uliongezeka kiasi cha kutetea uwapo wao.

Anasema kumekuwapo dhana hasi inayoenezwa na majangili wa wanyamapori, kwamba viungo vya faru hasa pembe, vinahitajika sana katika nchi za Bara Asia kwa vile vinatumika kutengeneza dawa na mapambo na hivyo kulipiwa fedha nyingi kwa ununuzi wake.

Miongoni mwa hoja inayojengwa kuhusu viungo hivyo vya faru, ni kwamba zinatengeneza dawa, zikiwamo za kuongeza nguvu za kiume.

“Wanawaaminisha watu kuwa nguvu za kiume za faru zinazomfanya ama apande jike kwa takribani dakika 40 zinazopatikana kwenye pembe zake, jambo ambalo limethibitishwa na wataalamu kwamba si kweli,” anasema.

Mwandishi wa Nipashe aliyekuwapo nchini Thailand wiki kadhaa zilizopita, alithibitisha kuwapo dhana hizo na alishuhudia bidhaa zitokanazo na viungo vya wanyamapori hao zikiuzwa kwa bei kubwa kwenye masoko mbalimbali ndani ya imani hiyo.

Miongoni mwa bidha hizo ni kama vile shanga, pete na bangili zinazotengezwa kutokana na viungo kama vile pembe, kucha, kwato na ngozi za wanyama, wakiwamo faru watokao Afrika.

Ulinzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro unatambua umuhimu wa faru na unasema unajipanga kuweka mikakati ya ulinzi dhidi ya wanyamapori, waliopo kwenye hatari ya kutoweka.

Mkakati huo unahusu hamasa na elimu kwa jamii inayoishi ndani na maeneo ya kuzunguka eneo la mamlaka, ili washiriki kuwalinda wanyamapori dhidi ya majangili.

**MWANANCHI/ MWONGOZA WATALII**

Francis Ole Siapambuni, ni mfugaji kutoka jamii ya Kimasai, anayeishi ndani ya Mamlaka a Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Anasema, hifadhi hiyo ina mazingira mazuri ya mapito ya wanyamapori na malisho ya mifugo, pia ina sehemu maalumu kwa ajili ya wanyama aina ya pofu na nyani wanaozaliana pamoja na ndege wa aina tofauti.

Pia, anabainisha kuwapo viumbe wanaovutia watalii wanaopatikana ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro . Anafafanua:”Wageni wakija kuona faru hawa weusi, wanaingiza kipato, kwa hiyo tunafurahi.”

Anaendelea:“Maana tunanufaika sisi kutokana na mapato yanayotokana na ugeni huu. Tunajengewa shule, hospitali pamoja na zahanati, kwa hiyo tunajivunia bonde letu la ‘crater’ pamoja na wanyama tuliyo nao.”

Mwongoza utalii anayejitambulisha kwa jina la Bakari Uledi, anasema watalii wengi wanapenda kuwaona Faru Weusi, kwani wanawavutia sana na inaopotokea baadhi yao na hasa watalii hasa wazee wanaofika hifadhini na hawajabahatika kuwaona Faru Weusi, waangukia masikitiko makubwa, wanaondoka na huzuni.

Anasema, licha ya wengi kufika kuona wanyama wengine, hisia zao zaidi ni katika mnyama Faru Mweusi

**KAMISHNA UHIFADHI**

Kamishna wa Uhifadhi wa mamlaka hiyo, Freddy Manongi, anasema mafanikio katika kupambana na ujangili, kwani katika kipindi cha miaka minne iliyopita, hakuna tukio la ama tembo au faru aliyeuawa na majangili.

Anasema wanajivunia rekodi hiyo, kwani hivi sasa uhifadhi na ulinzi wa wanyamapori huo, umekuwa wenye tija na manufaa zaidi kitaifa.

“Hakuna mzoga wa faru au tembo ambao umeokotwa kwenye eneo la mamlaka au hata kuripotiwa kwenye hifadhi nyingine nchini, kwamba kuna mnyama kauawa na majangili,” anasema Manongi.

# Biashara katika picha



Wafanyakazi wa benki ya NMB, wakipozi kwa picha katika uzinduzi wa wiki ya huduma kwa wateja wa benki hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**



Machinga wakiwa wametandaza bidhaa zao kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Sayansi Kijitonyama, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**



Madereva wa bobaboda wakiwa wameziegesha kwenye stendi mpya ya mjini Nachingwea mkoani Lindi hivi karibuni, wakisubiri abiria wanaoshuka kwenye  mabasi ili kuwapeleka maeneo mbalimbali ya mji huo.  **NA MPIGAPICHA WETU**

UCHUMI

## MAMBO YA KILOSA & MVOMERO

# Ufadhili wa EU mpunga shambani wapaishwa kupitia 'Kilimo Shadidi'

• Waliopata gunia nane sasa 40 • Hasara 40% yashuka hadi 25% • Wakulima 15,000 katika vijiji 36




Mwakilishi wa Umoja wa Ulaya (EU), Anna Costantini (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgoy (wa kwanza kulia) wakizIndua ghala la kuhifadhi mpunga katika Kata ya Kilangali,lililojengwa kwa ufadhili wa EU. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

**INATOKA UK.15**

ghala hayo na ukarabati wake umegharimu jumla ya Sh. milioni 508, EU ikichangia asilimia 80 na Helvetas umechangia asilimia 20.

Lengo kwa mujibu wa Kalimbya, ni kuwasaidia wakulima waongeze thamani ya mpunga, baada ya kukidhi vigezo vya masoko na kusaidia kupunguza upotevu wa mazao hilo baada ya mavuno, inayowahakikishia usalama wa chakula.

Anasema mradi umekusudia kumaliza changamoto zinazowakabili walima mpunga katika wilaya hizo mbili, kama vile tija ndogo, upungufu wa mazao, upotevu kabla na baada ya mavuno.

Nyigine anazitaja kuwa ni uwezo mdogo wa utunzaji na usindikaji, vikwazo katika kupata huduma za kifedha na mikopo na kukosa soko la uhakika na uhusiano dhaifu katika mifumo ya masoko.

"Mradi huu umesaidia wakulima kupunguza upotevu wa zao la mpunga kutoka asilimia 40 mpaka 25 na hivyo kuwaongezea kipato na uhakika wa chakula pamoja na kufanya biashara ya mchele joto" anasema Kalimbya.

> **"Mradi uliopo sasa wakulima wa wilaya hizo mbili wataweza kuisadia serikali kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga.**

Anasema, wakulima wamepewa mafunzo ya kilimo bora cha 'Mpunga Shadidi' na wameongeza uzalishaji kutoka gunia nane mpaka 40 kwa ekari moja, inayowaongezea kipato, usimamizi wa mazao kabla na baada ya mavuno

Hiyo inatajwa umuhimu wa kongeza thamani ya zao la mpunga na kukidhi vigezo masoko.

### WANUFAIKA WA RIPOMA

Mkulima Bahati Dimoso, kutoka Kata ya Dihombo wilayani Mvomero, anasema kupitia mafunzo ya kilimo bora cha mpunga, ameongeza uzalishaji kutoka gunia 10 mpaka 45 kwa ekari.

Anasema hivyo anaweza kuhifadhi ghalani na kusubiri bei ipande na kuuza kwa bei ya faida, tofauti na mwanzo walivyolazimika kuuza shambani au walanguzi.

Anasema kuwa hivi sasa amesomesha watoto wake wawili na mwingine akitarajia kumaliza masomo yake ya sekondari, huku akifanikiwa kuwa na duka kwa ajili ya shughuli zake za kibiashara.

Mkulima Esther Kihondo kutoka Kata ya Kilangali wilayani Kilosa, anasema manufaa ya mradi huo kwake ni makubwa sana, kutokana na uhakika wa chakula na kuhifadhi ghalani na kuongeza thamani ya mpunga kuuza mchele joto kwa bei

"Tumeongeza thamani katika zao la mpunga kwa kutengeneza mchele joto ambayo bei yake iko juu kuanzia Sh. 2500 hadi Sh. 3000 kwa kilo moja, ukilinganisha na mchele wa kawaida ambao bei yake ni Sh.1200 hadi Sh.1800 kwa kilo hatua ambayo imekuwa ikitunufaisha na kututoa kimaisha" anasema Esther.

### WIZARA YA KILIMO

Ofisa kutoka Kitengo cha Uhifadhi, Usindikaji na Usalama wa Chakula, Wizara ya Kilimo, Sadati Makwaluzi, anasema wastani wa asilimia 30 hadi 40 ya mazao ya nafaka nchini yamekuwa yakipotea wakati wa uzalishaji na kuisababishia nchi hasara.

Anasema, mradi uliopo sasa wakulima wa wilaya hizo mbili wataweza kuisadia serikali kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga.

Anasema, serikali hivi sasa imeweka mikakati ya nchi kufikia uchumi wa kati, ifikapo mwaka 2025 kupitia sekta viwanda na kwamba, miongoni mwa mazao ya kimkakati yaliyopewa kipaumbele kwa ajili ya kuzalisha malighafi, ni pamoja na mpunga hivyo kuongezeka uzalishaji wake.

" Elimu iliyotolewa kwa wakulima wa wilaya hizi mbili za Kilosa na Mvomero kuhusu kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga na kuongeza thamani ya zao hilo pamoja na ujenzi wa maghala ya kuhifadhi nafaka, ikiwamo zao la mpunga ni nyenzo muhimu kwa wakazi wa mkoa wa Morogoro katika usalama wa chakula,kuongeza kipato na kuelekea Uchumi wa Viwanda " anasema Makwaluzi.

### MWAKILISHI EU

Mwakilishi wa EU, Anna Costantini, anasema mradi huo umeghalimiwa na fedha za wananchi wa EU na umelenga kukuza sekta ya mpunga mkoani Morogoro, wakati nchi ikielekea katika Uchumi wa Viwanda.

Anasema mradi wa Ripoma, umelenga kuwasaidia wakulima wadogo wa mpunga wakiwamo wanawake na vijana ili kuondokana na changamoto mbalimbali kama umasikini na kuongeza zao hilo lenye soko la uhakika.

Anasema ni mradi wenye thamani ya Euro milioni 4.5.

### DC KILOSA

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgoy, anasema kupitia mradi huo na ujenzi wa maghala katika wilaya mbili, yatasaidia kupunguza upotevu wa mpunga na kuuwa vituo vya kukusanya na kuuza mazao kwa bei nzuri na njia rahisi ya kupata mikopo.

Mkuu wa Wilaya Kilosa, anasema licha ya wakulima kunufaika kwa kupata elimu ya kilimo bora cha Mpunga Shadidi, pia itasaidia kuwaongezea kipato kutokana na kuongeza thamani ya zao hilo, baada ya mavuno na anaitaka EU kuongeza ufadhili katika maeneo mengine kunakolimwa mpunga.

Pia kitokana na mabadiliko ya tabianchi, Mkuu wa Wilaya huyo, anaitaka kuangalia uwezekano wa kuboreshea miundombinu ya umwagiliaji, mifereji na mabanio kwa wakulima wa mpunga ili wajihakikishie uzalishaji na uhakika katika maeneo yanayolimwa zao hilo.


BIASHARA

DODOMA MPYA...

# Kikundi vijana chafungua mlango wa ajira kupitia utotoaji kuku

Na Renatha Msungu, Dodoma

• Wakamata soko, waangaza nje ya mkoa




Mwenyekiti wa Tusumuke Group, Christopher Dioniz, akionyesha vifaranga vya kuku ambavyo vimetotolewa. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

UKOSEFU wa ajira ni moja ya tatizo kubwa linalowakabili vijana wengi hasa wasomi, ambao wamekuwa wakitumia muda mwingi kutafuta kazi katika ofisi mbalimbali bila mafanikio.

Mara nyingi hali hiyo imeibua lawama nyingi, lakini mkoani Dodoma, hoja hiyo ina lake. Kuna kundi la vijana wasomi walioamua kukabiliana na changamoto hiyo ya ukosefu wa ajira, kwa kuanzisha mradi wa uzalishaji vifaranga wa kuku kupitia mayai yanayoletwa na wateja.

Kikundi hicho kinachoitwa Tusumuke Group, kimenza mradi huo kwa mafanikio makubwa, kwa kuwa na soko la uhakika kuuza vifaranga vya kuku katika maeneo ya Dodoma na nje ya mipaka yake, lengo ni kujiinua kiuchumi kama ilivyo kwa wajasiriamali wengine.

Tusumuke Group, inaundwa na wahitimu wa vyuo mbalimbali vya elimu, waliohitimu na kuamua kujiajiri kupitia ufugaji na kilimo cha mboga wanachofanya katika eneo la Nanenane, jijini hapa, wakinuia kuongeza kipato cha kila siku, kulingana na ujasiriamali wanaofanya, ambao unaonekana kuleta tija mbele ya jamii.

### MWENYEKITI TUSUMUKE

Christopher Dioniz, ni mwenyekiti wa kikundi hicho anayesema, hakuna sababu ya vijana kukaa chini kufikiria ajira za serikalini, bali kinachotakiwa ni kubadilisha mtazamo kuhusu elimu waliopata na kuitumia kwa vitendo, ili ilete tija kwa jamii inayowazunguka.

Anasema, utaalamu waliopata wanaweza kuuweka kwa vitendo kwa kuanzisha vikundi vya ujasiriamali tofauti, ambao utawainua kiuchumi, kama ikiwamo katika kuendesha maisha yao ya kila siku.

Dioniz anaeleza haja ya vijana kuungana na kutumia fursa zilizopo kuanzisha mradi ambao utawainua kiuchumi.

Anasema, Tusumuke Group, hivi sasa imepanua wigo wa ununuzi wa mayai kutoka sehemu mbalimbali za jiji la Dodoma na kutotoa vifaranga vya kuku, wanavyoviuza katika maeneo tofauti jijini.

Anasema ni umoja uliowasaidia kwa kiasi kikubwa, kutokana na kila mmoja kwenye kikundi hicho, anamudu kuendesha maisha yake ya kila siku, wakijumuisha na familia zao.

"Nawashauri vijana wasomi kuchangamkia fursa za kujiajiri wao wenyewe. Kuna faida kubwa hasa ukizingatia wanafanya ujasiriamali wenye tija, iwe wa kilimo au ufugaji," anasema Dioniz.

> "Nawaomba vijana tuinuke, tuache fikra za kuajiriwa na badala yake kujiajiri wenyewe kupitia ujasiriamali mbalimbali.

Anafafanua kuwa vijana wengi wasomi wanapaswa kutumia elimu waliopata kwa vitendo vitakavyowasaidia kutengeneza fursa za ajira nyingi kwao, tofauti na maisha ya kusubiri kuajiriwa kutoka katika taasisi binafsi au serikalini.

Mwenyekiti anaenda mbali akisema, vijana wasomi hivi sasa wana fursa kubwa ya kujiendeleza kibiashara kutokana na uwazi uliopo, ikiwamo upatikanaji mikopo kutoka serikalini, kwa vikundi vya vijana, ili mradi kiwe kimesajiliwa na kina uhakika wa kile inachokifanya, kupitia mchanganuo inaowasilisha katika maombi yao.

"Nawaomba vijana tuinuke, tuache fikra za kuajiriwa na badala yake kujiajiri wenyewe kupitia ujasiriamali mbalimbali," anasema Dioniz.

### MAFANIKIO YAKOJE?

Sehemu ya mafanikio yao, anayataja ni pamoja na kuajiri vijana wengi katika kikundi hicho, ambacho kina wigo mkubwa hivi sasa wa kuielimisha jamii juu ya utotoaji vifaranga na ufugaji wa kuku.

Dioniz anasema, hivi sasa wako mstari wa mbele kuwavuta vijana wengine kuingia katika ujasiriamali, eneo wanaloamini 'itawatoa' kimaisha, ikiwamo kujiingizia kipato chao cha kila siku na familia zao.

Mwenyekiti huyo anasema, taifa hivi sasa linaelekea katika uchumi wa kati wa viwanda, hivyo ni vyema vijana wengi wanatumia fursa hizo kuanzisha vikundi, ambavyo vitawapa faida hivi sasa na baadaye.

Mwenyekiti anaeleza soko la uuzaji vifaranga vya kuku mjini Dodoma hivi sasa limekuwa kubwa sana na Tusumuke inafanya jitihada za kuhakikisha ikabidhi soko la wakazi wa Dodoma, ambao wengi wamekuwa wakifuata vifaranga vya kuku kikundi kililopo, eneo la Nanenane.

Dioniz anasema, lengo lao ni kuona soko linavuka nje ya jiji la Dodoma na wanahitaji kuona soko linakuwa kubwa zaidi ya lilivyokuwa awali, sababu ni kwamba wanajipanga kuongeza idadi ya utotoaji vifaranga vya kuku.

Anatamka matarajio yao ni kuwa na kikundi cha mfano jijini Dodoma, hata nje ili wapate wigo kutoa elimu kwa vijana wengine, wanaoendelea kubweteka kusubiri ajira badala yake wajikite kujiajiri.

"Tunahitaji kuwa na kikundi cha mfano kuona vijana wote hawabaki nyuma, badala yake wabadilishe mtazamo," anasema Dioniz.

Anasema lengo lao ni kuona wanafika mbali katika ufugaji kuku kuhakikisha wanasonga mbele na ufugaji kwa njia ya usambazaji.

### KATIBU KIKUNDI

Katibu wa Tusumuke, Erick Buberwa, anasema moja ya ushauri kwa vijana, ni kwamba wanatakiwa wasikate tamaa na badala yake, wachape kazi kuendesha maisha yao ya kila siku na familia.

Pia, Buberwa anasema wanapaswa kutumia mawazo walio nayo kichwani kwa malengo endelevu na si kubaki nayo bila ya kuyafanyia kazi kwa ufasaha.

"Maendeleo yanaanzia kichwani na baadaye huyafanyia kazi kwa vitendo anasema," anasema Buberwa, ambaye ni hodari wa utaalamu wa uandishi wa miradi.

Anasisitiza vijana wengi wanakuwa na mawazo mazuri lakini wanashindwa kuyafanyia kazi kwa sababu hawayatumii kwa kitendo.

Anashauri kwamba kinachotakiwa hivi sasa ni kufanya kazi kwa vitendo kupitia elimu mbalimbali waliopata, kwani itawasaidia kuwainua kiuchumi.

BIASHARA

UTAFITI WAINGIA SOKONI

# Chuo Kikuu Nelson Mandela chakomboa wakulima, mifugo

• Nyanya, mboga, nafaka sasa salama • Mdudu 'Kantagaze' aletewa 'Vuruga' • Rasmi sokoni nembo ya Chuo Mandela • Dk. Isakwisa; Anusuru mifugo porini



Nyanya zilizoathiriwa shambani na mdudu 'Kantangaze,' **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

CHUO Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (NM - AIST), kimekuja na majibu kwa wakulima, wanyamapori na wafugaji kwa kugundua tafiti za kudhibiti wadudu na wavamizi wanaoshambulia mboga, nafaka, nyanya na nyasi za malisho.

Ofisa Uhusiano na Mawasiliano wa chuo hicho, Peres Muhagaze, ameiambia Nipashe kwamba katika kumdhibiti mdudu huyo mharibifu, mtafiti Dk. Never Zekaya, amegundua kiuatilifu alichokiita 'Vuruga' kinachomdhiti mdudu anayefahamika kwa jina maarufu 'Kantangaze' au kitaaluma anaitwa 'Tuta Absoluta.'

Muhagaze anasema, mtafiti huyo aligundua, baada ya kutafiti kwa miaka minne, kupitia michakato mbalimbali ya kisayansi na hatimaye akapata matokeo ya dawa hiyo ya 'Vuruga' inayoleta ahueni kwa walima mboga na nafaka.

Anasema, baada ya hapo kwa kushirikiana na uongozi wa chuo, alianza taratibu za kuisajili na kikapewa haki miliki ya ugunduzi huo kabla ya kuwasilisha sokoni.

"Mdudu huyu kwa mfano kwenye zao la nyanya hujipenyeza wakati wa hatua ya kuzaa matunda na hapo huyafanya matunda kuoza na kuweka rangi nyeusi. Wakulima walikosa suluhisho la kumuangamiza mdudu huyu tishio, lakini sasa mwisho wake umefika ambao ni Vuruga," anasema.

Muhagaze anaongeza kuwa tayari Vuruga imeshafanyiwa majaribio yenye mafanikio kwenye mashamba ya wakulima wa Arusha, Morogoro na Mbeya na kumdhibiti mdudu huyo.

> **Baada ya hapo kwa kushirikiana na uongozi wa chuo, alianza taratibu za kukisajili na kikapewa haki miliki ya ugunduzi huo kabla ya kuwasilisha sokoni.**



**INAINGIA SOKONI**

Muhangaze anasema, Vuruga haijaanza rasmi kibiashara, lakini Dk. Zekaya ameshafanya mazungumzo na kufikia makubaliano na kampuni kadhaa mkoani Kilimanjaro, ili kuzalisha kwa wingi na kuuziwa wakulima.

Anamtaja mtafiti mwingine chuoni hapo, Dk. Isakwisa Ngondya, amegundua majani ya asili yenye uwezo wa kuangamiza gugu vamizi (invasive species), ambao husababisha kutoweka malisho ya wanyamapori na wafugwao. Ulifanyika katika Bonde la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Anasema mtafiti huyo alianza utafiti kwenye shamba la chuo mwaka 2017 na baadaye majaribio madogo kwenye Bonde la Ngorongoro, ikifanikiwa kuangamiza gugu vamizi kwa asilimia 70 na kustawi.

Ni utafiti huo uliopata nguvu baada ya Wizara ya Mazingira ya Tanzania, kuunda kikosi kazi kilichopewa jukumu la kutengeneza Mpango Mkakati wa Kudhibiti Viumbe Vamizi nchini, wa mwaka 2019 hadi 2029.

Muhagaze anasema, chuo kinaendelea na tafiti zingine zinazogusa jamii na viwanda nchini na barani Afrika kwa ujumla.

Anazitaja kuwa ni za maji salama, ambayo mtafiti Dk. Askwar Hilonga, alifanikiwa kugundua chujio la maji ya kunywa linalotumia teknolojia ya kuondoa kemikali za aina zote, wadudu na madini aina ya Floride, ambao umefanikishwa baada ya miaka mitano.

Kwa mujibu wa msemaji wa chuo, imemuwezesha Dk. Ilonga kupata tuzo ya kwanza mwaka 2015, baada ya kuibuka mshindi wa mashindano ya wahandisi - UK Royal Engineering Academy, Uingereza na Wizara ya Afya Tanzania; pia Shirika la Afya Duniani (WHO).

"Inasemekana chujio hili limekuwa msaada mkubwa kwa wakazi wa Arusha na maeneo ya jirani, tangu watu walipoanza kulitumia, anasema Muhagaze na kuongeza:

"Kabla ya hapo, Arusha ilikuwa ikikumbwa na ugonjwa wa kipindupindu mara kwa mara ila sasa umepungua kwa kiasi kikubwa, hivyo watu watakavyoendelea kutumia maji yaliyochujwa na chujio hili, madhara ya Floride yatapungua."

Anasema, chuo hicho kilitokana na mawazo ya aliyekuwa Rais wa Afrika ya Kusini, Nelson Mandela, alipohudhuria mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika, ambayo inalenga kutafiti kwa ajili ya maendeleo Afrika, hasa nyanja za Sayansi, Uhandisi na Teknolojia, kutatua changamoto za kimaendeleo zilizopo.

Muhagaze anaeleza mafanikio ya Chuo Kikuu Mandela ni kuhusu ushindi na kuwa mwenyeji wa vituo viwili vya umahiri katika ufundishaji na utafiti barani Afrika, vinavyofadhiliwa na Benki ya Dunia. Anaongeza kuwa, hivi sasa kati ya wanafunzi walio nao zaidi ya 500, wanaojigharamia ada ni chini ya asilimia 10, hata hivyo chuo kinaendelea kutafuta wadau kuweza kufanya mengi zaidi.o

Muhagaze anasema Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, kina mkakati wa kuendelea kutoa taaluma yenye ushindani kitaifa na kimataifa, kwa kuibua wataalamu wanaotatua changamoto za jamii na viwanda kupitia tafiti.

Kwa mujibu wa Muhagaze, wazo hilo la Nelson Mandela, pia limefanikisha kujengwa vyuo vya aina hiyo katika nchi za Bukinafaso; Chuo Kikuu cha Maji na Mazingira na Cha Nigeria, jijini Abuja; na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia nchini Afrika Kusini, ambacho bado hakijaanza.

**MTAFITI DK. ISAKWISA**

Naye Dk. Isakwisa Ngondya, aliyetafiti gugu vamizi, anasema mradi huo umeshaanza kustawisha majani hayo ya asili, katika maeneo mengi kunusuru malisho, kunusuru wanyama waathirika wasife.

Dk. Isakwisa anasema, gugu-vamizi linapoliwa na wanyamapori, ni hatari inayochangia vifo kwa kuvimba matumbo, kwani mmeng'enyo wa chakula tumboni haufanyiki vizuri kutokana na mapungufu katika mchakato huo wa chakula tumboni.

# TANROADS kuwafidia waliojenga hifadhini

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI itawalipa fidia wananchi tisa ambao hawakulipwa kupisha ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha cha Tanzania na Malawi kwenye mpaka wa Kasumulu ulioko Kyela, mkoani Mbeya, licha ya kujenga ndani ya hifadhi ya barabara.

Wananchi hao tisa hawakulipwa fidia baada ya Wakala wa Barabara (Tanroads), kuwagomea wakidai kuwa wamejenga ndani ya hifadhi ya barabara hivyo hawana haki ya kulipwa kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anayeshughulikia Ujenzi, Elius Mwakalinga, juzi alitembelea mpakani hapo na kuagiza wananchi hao walipwe fidia yao. Alisema wanalipwa kwa sababu wafadhili wa mradi wa Benki za Dunia (WB) na ile ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), wameagizwa walipwe kwani wameishi muda mrefu eneo hilo. Mwakalinga, alisema kuwa kwa mujibu wa sheria ni kweli wananchi hao wako ndani ya hifadhi ya barabara na hawana haki ya kisheria ya kulipwa, lakini wafadhili wa mradi wa ujenzi wa Kituo ambao ni Benki za Dunia (WB) na Maendeleo ya Afrika (AfDB), wameagiza walipwe.

"Kwa mujibu wa sheria zetu, wananchi hao tisa hawana haki ya kulipwa, lakini wafadhili wetu ambao ni WB na AfDB wamesema kama wameishi eneo hilo kwa muda mrefu wanastahili kulipwa. Hivyo serikali hatukuona sababu ya kukataa kuwalipa hivyo tumeamua wapate haki yao," alisema Mwakalinga.

Alisema kuwa tayari fedha kwa ajili ya fidia ya wananchi hao tisa waliosalia imeshatolewa na Rais John Magufuli na imekabidhiwa Tanroads Mkoa wa Mbeya ili kuwalipa.

Baadhi ya wananchi hao wameishukuru serikali kwa uamuzi huo na kusema kuwa kitendo hicho kimekuwa ni suluhisho la matatizo yao na mgogoro wa muda mrefu uliokuwepo baina yao na Serikali.

Magreth Thomas ni miongoni mwa wananchi hao ambaye alisema kukubaliwa kuwalipwa kunawafuta machozi ambayo walikuwa wakilia kwa muda mrefu.

"Tunaishukuru serikali kwa kukubali kutulipa, maana baada ya kuona wenzetu wamelipwa na sisi tumeachwa tulichanganyikiwa na hatukujua hatma yetu, lakini kwa kuwa wamekubali kutulipa tumefarijika sana," alisema Magreth.

Diwani wa Kata ya Njisi, Omary Mwinjuma, alisema kuwa baada ya mgogoro huo kumalizwa, wananchi wameupokea kwa mikono miwili mradi huo wa ujenzi wa kituo cha pamoja cha forodha kwenye mpaka huo.



Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah akikagua shehena ya vinyago vilivyokamatwa na Ofisi ya Misitu chini ya Meneja Misitu wa wilaya hiyo, mkoani Iringa hivi karibuni. Vinyago hivyo vimetengenezwa kwa kutumia miti iliyovunwa kinyume cha sheria. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Wasamaria waamka kuichangia Chalangwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI na wasamaria wema kutoka maeneo mbalimbali wameendelea kuchangia Sekondari Chalangwa wilayani Chunya Mbeya, iliyoungua hivi karibuni.

Fedha hizo zinatolewa kwa ajili ya ukarabati wa mabweni mawili ya yaliyoteketea hivi karibuni na chanzo cha moto hakijafahamika.

Mabweni hayo yaliteketea Septemba 30 mwaka huu, wakati wanafunzi wakiwa darasani na kusababisha vifaa vya wanafunzi na mali zote zilizokuwemo kuteketea.

Kufuatia hali hiyo wadau mbalimbali walianza kuwasilisha misaada yao shuleni hapo vikiwamo magodoro, daftari, sare za shule pamoja na vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kuyakarabati mabweni hayo.

Akizungumza wakati wa harambee iliyoitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi alisema wanafunzi walioathirika na ajali hiyo ni 150 na kwamba mpaka sasa misaada mbalimbali imetolewa na wadau.

Alitaja baadhi ya vifaa vilivyotolewa na wadau kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi hao kuendelea na masomo kuwa ni sare za shule, magodoro, mashuka, mablanketi na soksi huku wengine wakiendelea kujitokeza kuchangia.

"Kwenye hii harambee tumepata fedha taslimu Sh. 5,000,000, ahadi milioni 16.5 na tayari baadhi ya wadau wametuchangia saruji mifuko 110 na bati mabando 19, tunawashukuru wadau wote wanaoendelea kuchangia ili tuwasaidie vijana wetu," alisema Mahundi.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha elimu katika shule hiyo haitetereki kutokana na ajali hiyo na kwamba sasa azma hiyo imeanza kutimia.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Sophia Kumbuli, alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kuwahamasisha wadau katika kushiriki kuchangia ukarabati wa mabweni hayo.

Aliwaomba wananchi wa wilaya hiyo kuendelea kujitokeza kuchangia ukarabati huo ili ukamilike haraka na wanafunzi waendelee na masomo kama kawaida.

"Bado tuna uhitaji mkubwa hivyo tunawaomba ninyi mliojitokeza kwenye harambee hii mwendelee kusaidia kuhamasisha wengine huko mitaani ili nao waguswe," alisema Kumbuli.

Baadhi ya vifaa ambavyo vimeshatolewa vinaanza kufanya kazi mara moja ili kazi hiyo ikamilike na mhula wa masomo kwa wanafunzi usivurugike, alisema.

## Shirika lajitosa Ufanisi wa biashara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Maendeleo la Uholanzi (SNV), kupitia mradi wa kuboresha mfumo wa masoko ya maziwa na alizeti (TAM), linafanyakazi na mabaraza ya biashara mkoani Mbeya kuongeza ufanisi.

Mshauri wa masuala ya sera katika mradi wa TAM, Renatus Mbamilo, aliyasema hayo wakati wa mkutano wa wadau wa mabaraza ya biashara wa mkoa huo wakiwemo watendaji kutoka serikalini na wa sekta binafsi.

Baadhi ya wadau waliohudhuria mkutano huo ni pamoja na makatibu wa chemba za wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima (TCCIA) wa wilaya zote, maofisa biashara wa halmashauri na wawakilishi wa asasi ya wasindika mafuta ya alizeti Mbeya (Mbesopa).

Mbamilo alisema SNV inatekeleza mradi huo kwa kushirikiana Shirika la Msaada la Watu wa Uingereza (UkAID) na kwamba waliamua kuyasaidia mabaraza hayo kufuatia kuombwa na serikali ya mkoa.

Alisema wanayasaidia mabaraza katika maeneo ya ubora wa majadiliano, namna ya kuibua hoja na kuzitafutia majawabu pamoja na namna ya kupata fedha za kuendeshea mabaraza.

Ofisa Biashara wa Mkoa wa Mbeya, Stanley Kibakaya, alisema waliamua kuliomba shirika hilo kusaidia kuboresha utendaji kazi wa mabaraza hayo baada ya kubaini kuwa yanajishughulisha pia na uboreshaji wa mazingira ya kibiashara.

Alisema mabaraza yanakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinafanya yasiwe na ufanisi hasa katika kutatua changamoto zinazokwamisha kuboresha sekta ya biashara.

Alisema baadhi ya changamoto ni pamoja na kukosa bajeti za kuyaendeshea na kuwa na uwakilishi ambao si mzuri kwa pande zote mbili ambazo ni sekta binafsi na ya umma.

Vilevile alisema mabaraza hayo yamekuwa yakitekeleza majukumu yake kwa kushinikizwa badala ya kufanya kazi kwa mujibu wa sheria hali ambayo pia alisema inapunguza ufanisi.

"Baraza la biashara kwa mujibu wa sheria inatakiwa liwe ni majadiliano ambayo yanawapa wajumbe nafasi ya kuibua hoja na kutafuta ufumbuzi, lakini tulibaini kuwa wenzetu wa sekta binafsi wanakuja kulalamika hivyo tunaamini SNV watatusaidia kuwajengea wajumbe uwezo," alisema Kibakaya.

Ofisa Mtendaji wa TCCIA wa Mbeya, Emile Malinza, alisema changamoto kubwa inayoyakabili mabaraza hayo ya mikoa na wilaya ni fedha za uendeshaji kwa madai kuwa serikali haina bajeti kwa ajili ya shughuli hizo.

Alisema wamewahi kukubaliana kufanya zamu kugharimia mabaraza hayo kati ya sekta ya umma na binafsi lakini wakakwama kutokana na halmashauri kutokuwa na mtiririko mzuri wa fedha.

Alisema kama mabaraza hayafanyiki, changamoto zinazokwamisha sekta ya biashara hazitatuliwi kwa wakati na hivyo sekta hiyo kushindwa kukua kwa kasi inayostahili.





# Bil.943/- zatumika elimu bure

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, amesema katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano, Sh.bilioni 943 zimetumika kwa ajili ya mpango wa elimu bila malipo.

Ole Nasha alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akifunga mkutano mkuu wa kwanza wa wenyeviti wa walimu wakuu shule za msingi Tanzania Bara.

Alisema katika kipindi hicho kumekuwa na mabadiliko makubwa kwenye sekta ya elimu ambayo yamechochewa na mambo mbalimbali ikiwamo mpango wa elimu bure na ujenzi wa miundombinu.

"Kwa miaka minne sasa serikali inatekeleza mpango wa elimu bila malipo na Sh. bilioni 24 zinatolewa kwa mwezi na jumla ya Sh. Bilioni 943 zimeshatumika tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani.

"Wanaopelekewa fedha kusimamia ni walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari, isingekuwa nyie kuwa wasimamizi wazuri tusingepata mafanikio makubwa lakini tumepata kutokana na nyie kuwa wasimamizi wazuri,"alisema.

Sambamba na hilo, alisema kwa kipindi hicho nchi imepiga hatua kubwa katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari ili kuwa na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.

"Kuanzia mwaka 2016 hadi sasa zimetumika Sh. bilioni 308 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwa shule za sekondari na msingi, wasimamizi wakuu wa miundombinu hiyo katika ujenzi wake," alisema.

Aidha alisema kwa kipindi hicho viwango vya ufaulu vimekuwa vikipanda bila kushuka.

"Matokeo ya darasa la saba mwaka 2016 ufaulu ulikuwa wa asilimia 70.2 huku mwaka 2017 ulipanda na kuwa asilimia 72.8. mwaka jana (2018) imefikia asilimia 77.72 na sifa hizi zinakuja kwenu walimu kwa kushirikiana na wazazi kwa kuongeza ufaulu," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa kidato cha nne wastani wa ufaulu kwa mwaka 2016 ilikuwa asilimia 70.4 na mwaka 2017 ni asilimia 77.6 huku mwaka 2018 ikiwa asilimia 78.4.

Kadhalika, alisema kuanzia mwaka 2016 hadi sasa serikali imeshatoa Sh. trilioni 1.8 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu.

Ole Nasha alisema serikali inaendelea kushughulikia tatizo la upungufu wa walimu.

"Ombi la walimu wakuu kupatiwa pikipiki naomba nilibebe ni suala la kibajeti, ni kweli mngeweza kusaidia mafanikio makubwa ," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema serikali inajipanga kupitia sera ya elimu ili kuendana na mfumo wa ufundishaji wa karne ya 21.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Walimu hao (Tapsha), Rehema Ramole, alisema siku mbili za mkutano huo wamepata mafunzo mbalimbali ya uongozi, haki na wajibu wao na kukabiliana na rushwa.

Aliomba walimu wakuu hao wapatiwe pikipiki ili kurahisisha usafiri kutokana na kufanya kazi kwenye mazingira magumu.



Mkuu wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Mwanahamisi Mukunda (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Mpalanga, Merina Mwakipesile na Daudi Daniel ya jinsi walivyofundishwa somo la Sayansi na waalimu wao, alipotembelea shule hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TCRA yasogeza huduma kwa wananchi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Kati imeanza kutembelea wilaya zote za jijini Dodoma kurahisha huduma za usajili wa kadi za simu kwa alama za vidole kwa wananchi kabla ya Desemba 31, mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa TCRA Kanda ya Kati, Antonio Manyanda, alipokuwa akitoa taarifa juu ya mwenendo wa usajili kadi za simu jijini Dodoma na mikoa ya Singida,Tabora na Kigoma.

Manyanda alisema kila wilaya watakuwa na siku tatu za kuendesha usajili huo na wanaamini jambo hilo litasaidia kwa kiasi kikubwa kuwafikia raia wote vijijini na mijini ambao hawajakamilisha usajili huo.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kutaka wananchi wote kutekeleza kabla ya Desemba 31, mwaka huu, muda ambao utakuwa mwisho wa kusajili kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

"Nawaomba wakazi wa maeneo mbalimbali kutumia nafasi iliyotolewa na TCRA ya kutembelea maeneo mbalimbali kwa ajili ya usajili," alisema Manyanda. Alisema wameanzia wilaya za Singida na baada ya hapo watahamia Dodoma mjini na kufuatiwa na wilaya za Bahi, Chamwino, Kondoa, Chemba na Kongwa.

Mkuu huyo alisema mikakati huo umelenga kupita wilaya zote na vijiji vyake ili kuhakikisha wananchi wote wa eneo husika wanafikiwa na huduma hiyo.

"Naomba wakazi wa Dodoma na mikoa jirani mtumie fursa hii kusajili laini zenu za simu hii ni nafasi ya mwisho kwenu kabla ya kumalizika muda uliowekwa," alisema Manyanda.

Mkazi wa Dodoma, Veronica Joseph, alisema hivi sasa shughuli ya usajili imeboreshwa kiasi kikubwa kwa sababu hakuna usumbufu wowote.

# Mfumo elimu kwa wafugaji kikwazo

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa wafugaji wamekuwa hawafaidi mazao ya mifugo yao kutokana na kukabiliwa na changamoto ya mfumo wa elimu inayotolewa kwa wataalam kutokuwa rafiki kwao.

Makamu Mkuu wa Chuo Mstaafu katika chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Dominick Kambarage, alisema hayo jana katika warsha ya siku moja kwa wataalamu wa mifugo, wafugaji na wadau wa mazao ya mifugo.

Warsha hiyo iliandaliwa na taasisi za Zoetis na African Livestock Production And Health Advancement (ALPHA) kwa kushirikiana na Bill & Melinda Gates kwa ajili ya kuwajengea uwezo wafugaji na kuhamasisha matumizi ya madawa kwa wakati sahihi katika kuwakinga mifugo.

Prof. Kambarage alisema elimu inayotolewa kwa wataalam Tanzania inaangalia zaidi vitabu na ufaulu wa mtu katika vyeti badala ya kuangalia mafunzo kwa vitendo na kwamba elimu imekuwa si ya kuwapika wataalam ili kuwa msaada kwa wafugaji na wakulima.

"Nashangaa vyuo kujaza wanafunzi kuliko uwezo wa udahili kwa chuo husika kitu kinachoonyesha bora wapate mafunzo lakini hakuna uhalisia. Vyuo vinatoa GPA (wastani wa ufaulu) nzuri sana, lakini hazitafaa kitu kama hakuna vitendo ndani yake. Umefika wakati tuangalie idadi ya wanafunzi na ubora wa tunachokihitaji," alisema.

Mtaalam mwingine, Prof. Amandus Muhairwa, alisema elimu inayopaswa kutolewa kwa sasa ielekezwe zaidi katika matumizi ya dawa za mifugo kuanzia kwa wafugaji wenyewe na kubadii mitazamo.

Prof. Muhairwa alisisitiza vyuo kutoa elimu ya vitendo zaidi ya nadharia na kuwatoa mijini wataalamu wa mifugo ili wakaishi karibu na wafugaji vijijini.

Awali, Mwakilishi wa Zoetis, Dk. Gabriel Varga alisema yametolewa kwa ajili ya kuwakumbusha wataalam kuwafikia wafugaji na kuwapa elimu.

Dk. Varga alisema utafiti mbalimbali umeonyesha wafugaji hawapati faida ya mifugo yao kutokana na kushindwa kufuata taratibu za ufugaji bora wenye tija.



# Sababu uchelewaji vyeti kuzaliwa hizi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UKOSEFU wa magamba ya kuchapisha vyeti vya kuzaliwa kwa watoto umesababisha kuchelewa upatikanaji wa yeti hivyo katika Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanziar.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Shamata Khamis Shaame, alisema tayari tatizo hilo kwa sasa limeshapatiwa ufumbuzi.

Alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Paje, Jaku Hashim Ayoub, aliyetaka kujua lini tatizo la kuchelewa kwa vyeti vya kuzaliwa watoto litapatiwa ufumbuzi.

Naibu Waziri huyo alisema tatizo hilo limechangiwa na mambo mbalimbali ikiwamo ukosefu wa muda mrefu wa magamba ya kuchapisha vyeti hivyo.

Alisema tatizo hilo sasa limepatiwa ufumbuzi ndiyo maana vyeti vya kuzaliwa vimeanza kuchapishwa, hivyo kuwataka wazazi kufuatilia kuchukua vyeti vya watoto wao vilivyokuwa tayari vimechapishwa.

"Mheshimiwa Spika tayari tumeanza kuchapisha vyeti vya kuzaliwa watoto baada ya kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizojitokeza ikiwamo ukosefu wa magamba," alisema.

Waziri aliitaja changamoto nyingine ambayo ilikuwa moja ya chanzo cha kusababisha kuchelewa kuchapishwa kwa vyeti hivyo kuwa ni hitilafu za kiufundi katika mfumo wa kielektroniki.

Alisema tatizo hilo nalo limetatuliwa na mafundi na uchapishaji wa vyeti hivyo kwa kuzingatia mfumo wa kielektroniki umeanza rasmi.

Aliwataka wazazi wa mikoa mitano ya Unguja na Pemba ambao awali walikuwa wakikabiliwa na tatizo hilo la ucheleweshaji wa vyeti hivyo kwenda katika ofisi za wakala ziliopo karibu na sehemu zao.

Hata hivyo alisema kwa sasa liko tatizo moja kubwa la mlundikano wa vyeti hivyo huku vingine vikisubiri kuchapishwa.

Alisema vyeti hivyo ni vile ambavyo vilikaa muda mrefu vikisubiri kuhakikiwa na kuingizwa katika mfumo rasmi wa kielektroniki.

# Wataka marekebisho sheria ya bahari

**Na Rahima Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi (BLW) wametaka marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini Zanzibar yafanyike haraka ili Zanzibar iendelee na kusajili meli za kimataifa baada ya kuzuiwa na serikali ya Muungano.

Msimamo huo umetolewa na Kamati ya Kudumu ya Ardhi na Mawasiliano katika maagizo yake kwa serikali baada ya Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar (ZMA) kuzuiwa kusajili meli za kimataifa kutokana na meli tano kukamatwa na vilipuzi na mihadarati.

"Kamati yangu inaitaka serikali kupitia ZMA kutekeleza maagizo yote kwa haraka ya kurekebisha sheria. Tunaamini yakirekebishwa haya bila shaka serikali ya Muungano itairuhusu ZMA kusajili tena meli za nje bila wasiwasi wowote," alisema Mwenyekiti wa Kamati, Hamza Hassan Juma, katika ripoti yake.

Akijibu hoja za kamati hiyo, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano, na Uchukuzi, Dk. Sira Ubwa Mamboya, alisema serikali imeanza kuifanyia mapitio ya marekebisho sheria ya Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kabla ya kuanza tena kusajili meli za kimataifa.

Aliwaambia wajumbe kuwa mapitio ya sheria baada ya kukamilika, yatawasilishwa katika kamati maalum zilizoundwa baina ya pande mbili za Muungano kabla ya kuwasilishwa serikalini kwa ajili ya utekelezaji wake.

"Wizara imeunda kamati maalum ya wataalam inayosimamiwa na ZMA ambayo imepanga kukutana na Kamati ya Tanzania Bara ambayo itajumuisha na vikosi vya ulinzi na usalama vya pande mbili ili kumaliza suala la Zanzibar kusajili meli za nje," alisema.

Waziri alisema suala la ukaguzi wa meli ni la kisheria, mkaguzi wa ZMA anajulikana na Taasisi ya Usafiri wa Baharini Duniani (IMO) na bandari zote duniani, hivyo hakuna uhusiano wa mkaguzi wa Tasac (Shirika la Wakala wa Meli Tanzania) ajibu masuala ya ukaguzi ya mamlaka ya usafiri wa baharini Zanzibar.

Alisema kimsingi ZMA ni chombo kinachojitegemea na hakiombi ruhusa Tasac badala yake ni kushauriana tu katika utekelezaji wa majukumu kupitia vikao vya pamoja.

Dk. Sira alisema mfumo huo wa kisasa wa usajili wa meli kwa kutumia teknolojia ya kielectroniki utazinduliwa rasmi baada ya kukamilika kwa masuala ya kisheria kupitiwa na kamati maalum zilizoundwa baina ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (kulia), akizungumza na Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Muhamed Ramia, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Maandalizi daftari mali za serikali mbioni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia, amesema mchakato wa maandalizi ya daftari la kuhakiki mali za serikali uko katika hatua za mwisho. Alisema hayo jana wakati akitoa ufafanuzi na kujibu hoja za Kamati ya Fedha ya Baraza la Wawakilishi iliyotaka kujua maandalizi ya kuanzishwa kwa daftari hilo yamefikia wapi.

Balozi Ramia alisema daftari la kuhakiki mali za serikali ni muhimu na litasaidia kuzitambua kwa haraka mali za Serikali.

Alisema kwa muda mrefu utaratibu wa kuhakiki na kuhifadhi mali za Serikali ulikuwa ukiwekwa kwa kila wizara na taasisi kwa njia zake. "Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba mchakato wa kuunda daftari la kuhakiki mali za Serikali uko katika hatua za mwisho," alisema.

Pia Balozi Ramia aliwaambia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba mashamba ya serikali yaliyotambuliwa Pemba tayari yameingizwa katika daftari hilo. Alisema mashamba hayo yalikuwa hayamo katika madaftari ya uhakiki mali wa Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo, hivyo kupotea na kuingia katika mikono ya watu binafsi.

# Sababu serikali kutumbua bodi ya maji za bainishwa

**Na Romana Mallya**

BODI ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA), imevunjwa kwa kushindwa kusimamia majukumu yake.

Taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Maji ilieleza kuwa hatua hiyo imechukuliwa na Waziri wa Maji Prof. Makame Mbarawa kuanzia juzi.

Taarifa ya Katibu Mkuu, Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo imeainisha kuwa kuvunjwa kwa bodi hiyo unatokana na mamlaka aliyo nayo Waziri kwa mujibu wa kifungu namba 14 cha jedwali la kwanza la Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira namba 5 ya Mwaka 2019.

"Kifungu hicho kikisomwa pamoja na kanuni namba 14 ya Kanuni za Usambazaji wa Maji (Tangazo la Serikali namba 90 la Aprili 26, mwaka huu," taarifa hiyo ilieleza.

Aidha, taarifa hiyo ilifafanua kuwa bodi ya MORUWASA imevunjwa kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia mamlaka ya maji hivyo kuathiri utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika manispaa ya Morogoro.

Prof. Mbarawa ametaka kuanza kwa utaratibu utakaowezesha kuundwa kwa bodi mpy



Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Zipora Liana (wa tatu kushoto), akikabidhi zawadi ya cheti kwa Mteja wa Benki ya NMB, Lucas Bise, wakati wa sherehe ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa `Wateja, iliyofanyika katika Tawi la Benki hiyo, Mlimani City, jijini humo juzi. Kushoto ni Ofisa Mkuu wa Idara ya Fedha NMB, Ruth Zapuna na Meneja Tawi hilo, Irene Masaki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sagcot: Kipaumbele chetu ni mkulima mdogo kupata soko

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (Sagcot), kinaweka kipaumbele kwenye kuinua mnyororo wa thamani wa mazao ili wakulima wadogo katika ushoroba wa kusini mwa Tanzania wapate soko la uhakika la mazao yao.

Kauli hiyo imetolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Geoffrey Kirenga, katika mahojiano maalumu juu ya utendaji wa taasisi yao katika kipindi cha miezi tisa iliyopita. Amesema tasisi hiyo kwa sasa msukumo wake ni kutumia kongani zake kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao yanayozalishwa ili wakulima washiriki kwenye mapinduzi ya kilimo na kilimo kiwa na tija na wakulima washuhudie wenyewe kilimo kinavyowaletea maendeleo.

Aliyataja mazao hayo ni nyanya, chai, viazi mviringo, maziwa na soya na kusema kuwa baada ya mazao kuyaongezea thamani yamepata soko la uhakika ndani na nje ya Tanzania.

"Nguvu kubwa tumeielekeza katika kuongeza thamani mazao yanayozalishwa na wakulima katika ukanda tuliokabidhiwa na taifa, maana lengo ni kumnufaisha mkulima na shughuli zake za kilimo na kupata maendeleo yeye na taifa," alieleza Kirenga.

Alisema taasisi yake imeunganisha wakulima wadogo katika ushoroba wa kusini mwa Tanzania na wabia hao wamefikisha huduma mbali mbali kwa wakulima na kufanya uzalishaji ongezeke maradufu.

Hakutoa takwimu.

"Kwa hiyo kazi yetu ilikuwa ni kutambua wabia sahihi, wadau mbalimbali wa maendeleo na kuwashawishi tushirikiane nao kuinua wakulima katika ushoroba wetu; wakakubali," alisema.

Mkuu wa Kongani na Maendeleo ya Ubia, Maria Ijumba, alileza kuwa ongezeko la mazao katika ushoroba wa kusini kimsingi ni matokeo ya kutumia mbinu ya kongani.

Alieleza kuwa suala la kuwaunganisha wakulima wadogo na kuwafikishia huduma ili kilimo kiwe na tija kwao lilihitaji ubunifu ndiyo sababu taasisi yao ikabinu mbinu ya kongani.

## NMB yapiga jeki vifaa elimu, afya

**Na Mwandishi Wetu,** BAHI

MKUU wa Wilaya ya Bahi ,Mwanahamisi Mukunda amewataka wazazi nchini kujenga tabia ya kufuatilia maendeleo ya elimu ya watoto wao kila siku ili kubaini uwezo wao katika masomo.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akipokea msaada wa madawati 51 kwa ajili ya shule ya Msingi Mpalanga na vifaa tiba kwa ajili ya kituo cha afya Bahi vyote ikiwa ni msaada toka Benki ya NMB. Mukunda aliwataka wazazi kujenga tabia ya kufuatilia maendeleo ya elimu ya watoto wao ili kubaini uwezo walionao katika masomo .

"Tuache kulalamika na kuwanyooshea vidole waalimu kuwa hawafundishi, wakati mwingine ni vigumu kwa mwalimu kuweza kujua kama kila mwanafunzi ameelewa somo , lakini kama kila mzazi akijenga tabia ya kufuatilia maendeleo ya elimu ya mtoto atabaini uwezo wake," alisema. Alisema wakati mwingine wanafunzi wamekuwa watoro hawafiki shuleni lakini mzazi akikagua madaftari yake atabaini kuwa motto wake hakufika shule siku hiyo.

Pia aliwataka kuwahimiza watoto kwenda shule pamoja na kuwajengea mazingira mazuri kwa kuwanunulia mahitaji mhimu ya shule ili kuwavitia zaidia.

Hata hivyo aliwashukuru Benki ya NMB kwa kutoa msaada huo kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya hiyo kwani umeweza kuokoa fedha nyingi ambazo zingetumika kununulia vifaa hivyo. Aidha, alisema Wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa madawati zaidi ya madawati 6,000 na yaliyopo ni madawati 9000 kwa Wilaya yote.

Naye Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema benki hiyo ilikabidhi msaada wa sh milioni 10 kwa maeneo hayo mawili . Alisema katika Kituo cha Afya Bahi walikabidhi vitanda vitano pamoja na magodoro yake, mashuka 25, seti moja ya vifaa vya chumba cha akinamama kujifungulia na kitanda kimoja cha wajawazito kujifungulia vyote hivyo vikiwa na thamani ya Sh. milioni tano.

Mlozi aliongeza kuwa katika Shule ya Msingi Mpalanga NMB ilikabidhi msaada wa madawati 51 yenye thamani ya Sh. milioni tano hivyo vifaa vyote katika maeneo hayo mawili kufikia thamani ya Sh. milioni 10. Mbunge wa Bahi, Omari Baduwel, alichangia Sh. milioni moja kwa ajili ya kulipia gharama za kuunganisha umeme Shule ya Msingi Mpalanga.

## Waonywa rushwa wakati uchaguzi

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MKUU wa Dawati la Elimu kwa Umma wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kigoma, Leonida Mushema, amewataka wananchi wa mkoa huo kuacha tabia ya kurubuniwa na wagombea kwa kuwapa kanga, chumvi, fedha na vitenge kwa lengo la kuchagua viongozi ambao si waadilifu.

Mushema aliiambia Nipashe kuwa changamoto waliyonayo ni wananchi wengi kujenga utamaduni kuwa kipindi cha uchaguzi ni kipindi cha mavuno.

Alisema: "Sisi tunapata upinzani mkubwa sana kwa sababu kuna wananchi wengi wanakuwa wanapotosha wengine kwamba mimi nikipata mtu ananipa Sh. 2,000 na wakati nimelala na njaa.

"Kumbuka kwamba fedha hiyo ataitumia kwa siku moja tu inaisha, pamoja na kukumbana na changamto hiyo watu hawako tayari kubadilika kisaikolojia, bado hatujachoka tunaendelea kuifanyia kazi kwa maana ya kutoa hamasa kwa viongozi wa dini na viongozi wengine wa serikali watusaidie kuendelea kuhamasisha watu."

HABARI KIMATAIFA

## Kampeni urais Tunisia zafungwa

**TUNIS,** Tunisia

KAMPENI za uchaguzi nchini Tunisia zilifungwa jana kwa duru ya pili ya uchaguzi wa urais unaotarajia kufanyika Jumapili ijayo.

Katika uchaguzi huo utawakutanisha, Kais Saied na mfanyabiashara aliyezuiliwa jela, Nabil Karoui.

Wafuasi wa Karoui walisema kuwa hawatakubali kufanyika kwa uchaguzi huo ikiwa mmoja wa wagombea hao wawili atakuwa bado anazuiliwa jela.

Kufungwa kwa Karoui kumezua sintofahamu kwa uchaguzi wa urais ambao umepangwa kufanyika mwishoni mwa wiki ijayo.

Wajumbe kadhaa wa kamati kuu ya kisiasa ya chama chake cha Qalb Tounes walikutana juzi na wametilia mashaka duru ya pili ya uchaguzi wa urais ikiwa kiongozi wao atakuwa bado anazuiliwa jela ndani ya siku 11 zinazosalia.

Wameomba Tume huru ya uchaguzi, ISIE kutafuta suluhisho haraka.

"Ni juu yao leo kutafuta suluhu hali ambayo siyo ya kawaida inayomkabili mgombea wetu aliyechaguliwa akiwa jela. Wanapaswa kupata ufumbuzi, siyo sisi," Osama Khlifi, mjumbe wa kamati kuu ya kisiasa ya chama cha Qalb Tounes alisema.

Mwenyekiti wa tume huru ya uchaguzi, ISIE, ameomba mara kadhaa Nabil Karoui kuachiliwa huru ili kuhakikisha usawa kuwania na fursa kwa wagombea wote wawili. **RFI**

## Jaribio lingine la kombora

**SEOUL,** Korea

KOREA Kaskazini imethibitisha kufanya jaribio la kurusha aina mpya ya kombora lenye uwezo wa kuruka kwa kasi ya kilomita 450 na kufika urefu wa kilomita 910 kabla alijashuka baharini.

Jaribio hili nchini humo ni la 11 kwa mwaka huu likitanguliwa na lile la mwezi Mei lililokuwa la masafa mafupi.

Katika nchi hiyo makombora yenye uwezo wa kubeba silaha za nyuklia yanarushwa. Lakini utofauti wa jaribio hili ni kuwa, kombora halijarushwa kutoka ardhini, bali kwenye nyambizi chini ya bahari.

Kombora hili kuwa na uwezo wa kurushwa kutoka majini ni umuhimu zaidi kwa nchi hiyo kwa kuwa sasa wana uwezo wa kufanya mashambulizi mbali ya eneo lao.

Kwa mujibu wa maofisa wa Korea Kusini, kombora hilo lina uwezo wa kuruka kwa kasi ya km 450 na kufika urefu wa km.910 kabla alijashuka baharini.

Hii inamaanisha kuwa makombora hayo yana uwezo wa kuruka umbali mrefu mara mbili wa kiwango cha kimataifa ingawa ya awali ya Korea Kaskazini yalikuwa na uwezo wa kuruka mbali zaidi.

Kombora hilo liangukia baharini upande wa Japani, unaoitwa upande wa Mashariki wa bahari.

Japani imedai kuwa kombora hilo limetua katika umbali wa kilomita 200 kutoka ardhi yake.

Jaribio hilo linakuja muda mfupi baada ya Korea Kusini kusema kuwa mazungumzo ya nyuklia kati yao na Marekani yataendelea. **BBC**

# Trump auita uchunguzi dhidi yake ni 'mapinduzi'

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, anakosoa uchunguzi ulioanzishwa dhidi yake wa kumuondoa madarakani na kuuita ni "mapinduzi".

Wakuu wa kamati mbalimbali za Baraza la Wawakilishi wamemtuhumu Waziri wa Mambo ya Nje, Mike Pompeo, kwa hatua yake ya kuzuia juhudi zao za kukusanya nyaraka na kuwahoji mashahidi.

"Kadiri ninavyopata kufahamu mambo mengi zaidi kila siku, ninafikia kuhitimisha kuwa kile kinachofanyika siyo kuniondoa madarakani kisheria bali ni mapinduzi.

"Ni mapinduzi ya kuwanyang'anya wananchi nguvu zao, kura zao, uhuru wao, haki yao ya kikatiba, uhuru wao wa dini, jeshi lao, ukuta wa mpakani na haki yao waliopewa na Mungu kama Raia wa Marekani," Trump ameandika katika ukurasa wake wa Twitter.

Wademokrat waliowengi katika Baraza la Wawakilishi wanaendelea na uchunguzi wa kumuondoa Rais madarakani ili kuangalia iwapo wanataka kumfungulia mashtaka Trump chini ya amri ya kikatiba inayowalazimisha maofisa wanaojihusisha na "uhaini, rushwa, au jinai nyingine kubwa na makosa mengine kuondolewa madarakani.

**Kadiri ninavyopata kufahamu mambo mengi zaidi kila siku, ninafikia kuhitimisha kuwa kile kinachofanyika siyo kuniondoa madarakani kisheria bali ni mapinduzi.**

Mkaguzi Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje anatarajiwa kukutana Jumatano na wafanyakazi kutoka Baraza la Wawakilishi na kamati mbalimbali za Baraza la Seneti kuzungumzia nyaraka ambazo wabunge wameomba wapatiwe wakati wakichunguza mazungumzo ya simu yaliofanyika Julai, kati ya Trump na Rais wa Ukrain Volodymyr Zelenskiy.

Kamati za Usalama, usimamizi na masuala ya kigeni za Baraza la Wawakilishi zilikuwa zimeomba kusikiliza ushahidi utakaotolewa Jumatano kutoka kwa Balozi wa zamani wa Marekani Ukraine, Marie Yovanovitch, lakini kikao hicho kilikuwa kimeahirishwa mpaka wiki ijayo.

Balozi huyo wa zamani aliyekuwa anaiwakilisha Marekani Ukraine anatarajiwa kuzungumza na kamati hiyo Alhamisi.

Trump alisema hakufanya makosa yoyote katika mazungumzo yake na Zelenskiy.

Mtoa taarifa alifungua malalamiko akieleza wasiwasi wake juu ya Trump kuomba nchi ya kigeni kuingilia kati uchaguzi wa mwaka 2020 kwa kuitaka Ukraine kumchunguza mgombea wa chama cha Demokrat, Joe Biden.

Pompeo ametuma barua Jumanne kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Kigeni ya Baraza la Wawakilishi, Eliot Engel akisema maombi ya kupatiwa nyaraka za Wizara ya Mambo ya Nje na ushahidi wa maafisa wa zamani na wa hivi sasa "inaelewekа kama ni jaribio la kuwatishia, kuwanyanyasa na kuwaonea" wafanyakazi wa idara hiyo.

Alisema maombi hayo yanazua "Masuala muhimu ya kisheria na utaratibu," na tahadhari zinazopuuziwa kuwa kutotoa ushirikiano itapelekea kuzuia sheria isifuate mkondo wake.



Raia wa Congo akipatiwa chanjo ya ugonjwa wa Ebola. **PICHA: DW**

# 25 washtakiwa kwa usaliti Rwanda

**KIGALI,** Rwanda

WATU 25 wameshtakiwa kwa kuisaliti serikali ya Rwanda pamoja na uhalifu mwingine unaohusiana na madai ya shughuli zao katika kundi la waasi.

Waendesha Mashtaka nchini humo, walisema watu hao wameshtakiwa kwa kuisaliti serikali hiyo na uhalifu mwingine unaohusiana na madai ya shughuli zao katika kundi la waasi lililoanzishwa na mpinzani mwenye makao yake nchini, Afrika Kusini.

Wanaume hao walifikishwa mbele ya Mahakama ya Kijeshi mjini Kigali kwa mara ya kwanza tangu waliporejeshwa Rwanda, mwezi Juni kutoka nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) walikokamatwa.

Washukiwa hao ni pamoja na Habibu Mudathiru, aliyekuwa mwanajeshi nchini Rwanda ambaye waendesha mashataka wanasema alikuwa msimamizi wa mafunzo na shughuli za kundi la waasi la Rwanda National Congress (RNC) nchini Congo lililoanzishwa na Kayumba Nyamwasa.

Nyamwasa aliyekuwa mshirika wa Rais Paul Kagame, sasa ni mpinzani wa Rwanda mwenye makao yake nchini Afrika Kusini.

Upande wa mashtaka ulisema kuwa, baadhi ya washukiwa ni raia wa Burundi huku wengine wakiwa raia wa Uganda. **DW**

## Utekelezaji miradi wasitishwa

INATOKA UK. 2

wa fedha mpaka hapo yatakapotoka maelekezo mengine," alisema.

Mwaipaja alisema wizara hiyo haijakataa miradi hiyo ya maendeleo lakini imeona tatizo liko katika utekelezaji wake.

Kwa mujibu wa barua ya katibu Mkuu, miradi iliyositishwa kwa mkoa wa Dar es Salaam ni minne ambayo ni wa Coco Beach, machinjio ya Vingunguti unaogharimu Sh. bilioni 8.5 ambao wiki mbili zilizopita Rais Magufuli aliutembelea, mradi wa soko la Tandale unaogharimu Sh. bilioni 9.6 na Kibada Sh. bilioni 14.02.

Barua hiyo ilitaja miradi mingine na gharama za ujenzi kwenye mabano kuwa ni Kituo cha Mabasi Liwale ambacho kitajengwa Likongowele (Sh. bilioni 1.2) machinjio ya kisasa Ngelewala, Iringa (Sh. bilioni moja), kituo kipya cha mabasi Nzega (Sh. bilioni 2.8), kituo cha mabasi Katesh, Hanang (Sh. bilioni 5.6) na soko la kisasa Bomani Ward, Tarime (Sh. bilioni nane).

Mingine ni soko la kisasa Mlandizi (Sh. bilioni 7.7, soko la samaki Sanzale, Chemchem Bagamoyo (Sh. bilioni 1.6) na kituo kipya cha maegesho ya malori Nyamhongolo, Ilemela (Sh. bilioni tisa).

Katika barua huyo, Katibu mkuu huyo alifafanua kuwa katika kipindi cha kuanzia Desemba 2017 hadi Agosti, mwaka jana, serikali iliingia mikataba ya utekelezaji wa miradi 38 yenye thamani ya Sh. bilioni 288.06 kutoka halmashauri 29 za mikoa 17.

"Hadi kufikia Agosti 2019, miradi 18 iko katika hatua za ujenzi na miradi mingine 20 haijafikia hatua ya ujenzi kutokana na sababu mbalimbali," alisema.

Barua hiyo ilieleza kuwa pamoja na nia njema ya serikali katika utekelezaji wa miradi hiyo na kutenga fedha kwa madhumuni hayo, bado baadhi ya halmashauri zimekuwa na utekelezaji hafifu na usioridhisha hivyo kutotimiza malengo ya kimkataba.

"Kwa barua hii, nasitisha utekelezaji wa mikataba ya kugharamia miradi yote ambayo wakandarasi bado hawajaanza kazi za ujenzi na mitadi ambayo ipo kwenye hatua za ununuzi hadi maelekezo mengine yatakapotolewa," alisema.

## Mjadala kila kona RC kuchapa viboko

INATOKA UK. 2

kikatili na inayodhalilisha utu. Pia nakemea kitendo cha Mkuu wa Mkoa kutumia madaraka yake vibaya kwa kutenda kinyume cha taratibu za adhabu kwa wanafunzi. Mwenye mamlaka ya kumwadhibu mwanafunzi ni mwalimu mkuu."

Naye Mwanasheria Jebra Kambole, katika ukurasa wake aliandika: "Huyu Mkuu wa Mkoa kuna siku ataenda kituoni akachukue bunduki ili kukamata wezi maana atona wezi wanasumbua polisi kama wanafunzi wanavyosumbua walimu!!! Unawachapa wewe ndo mwalimu wa shule?"

Naye Daniel Marari aliiandika: "Katika karne ambayo simu na kompyuta ni nyezo muhimu ya kusomea. Sisi tunaadhibu watu kwa kumiliki (si kutumia)) simu. Na ule mpango wa laptop kila mwanafunzi ulilenga nini?"

Ole Mmari, aliandika 'Hii ya RC kupita shuleni na kupiga wanafunzi ni 'too low'(jambo lilolo chini ya uwezo wake) kwa kiongozi. Mambo kama haya ni aibu kufanywa na kiongozi wa umma. Ni ukatili wa hali ya juu." "Katika zama hizi, tusijikite kuwanyima watoto kuwa na simu au kompyuta. Tujikite katika kuwafundisha matumzi bora, mfano wapi na jinsi gani ya kufikia vitabu na kujifunza zaidi ya darasani na kadhalika," aliongeza.

Saidi Fundikira alihoji kama sheria inamruhusu kufanya hivyo, vinginevyo wawasaidie wazazi wa watoto kumpeleka mahakamani. Alisisitiza ukatili kama huo usivumiliwe.

Thomas Ludovick alisema anaamini wakuu wa mikoa wana shughuli nyingi za kufanya kama kukagua au kufuatilia miradi ya maendeleo badala ya kujishusha na kufanya jambo kama hilo.

"Mungu wangu kama Mkuu wa Mkoa anaweza kuchapa viboko wanafunzi kiasi hiki mbele ya umma. Nafikiria anachofanya kwa watoto wake na mkewe," aliandika Charles Onyango.

Naye mdau wa elimu na mwandishi wa vitabu, Richard Mabala alihoji: "Alichapa viboko vingapi? alifuata sheria ya elimu kweli?"

Tito Magoti aliandika: "Si ruhusa wanafunzi kumiliki simu shuleni lakini RC Mbeya ametoa adabu kwa sheria ipi? Mihemko tu, amevunja sheria za nchi, amedhalilisha watoto mbele ya vyombo vya habari. Amepiga na kujeruhi na amejichukulia sheria mkononi."

Taarifa kutoka mkoani Mbeya zilisema wanafunzi watano wa shule hiyo wanashikiliwa na polisi tuhuma za kuchoma moto mabweni mawili ya shule hiyo.

Tukio hilo la uchomaji moto mabweni ambalo lilitokea majira ya saa 2:00 usiku, linadaiwa kuhatarisha maisha ya wanafunzi 150 wanaolala ndani ya mabweni hayo.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kiwanja, Elly Mnyarape, alisema chanzo cha tukio hilo ni baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo kukamatwa na simu za mkononi jambo ambalo ni kinyume cha sheria za shule hiyo.

Alisema Septemba 30, mwaka huu, walifanya msako na kukamata simu za mkononi zaidi ya 26 ambazo zilikuwa zikimilikiwa na wanfunzi.

Alisema baada ya msako huo, walishaangaa majira ya saa 2:00 usiku kuona mabweni mawili yakiungua, hatua ambayo wanaamini kuwa ilitokana na wanafunzi kutoridhika na kunyang'anywa simu zao.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, alisema baada ya kufika shuleni hapo, walifanya uchunguzi ikiwa ni pamoja na kuendesha kura ya siri ambapo wanafunzi 19 walikamatwa na kufikishwa Polisi kwa ajili ya mahojiano zaidi.

Alisema kuwa baada ya mahojiano ambayo yalifanywa na Mkuu wa Upelelezi wa Polisi Wilaya ya Chunya, wanafunzi 14 walionekana hawahusiki na kurejeshwa shuleni na wenzao watano wanaendelea kushikiliwa na polisi wakihusishwa na tukio hilo.

Baada ya kutoa maelezo hayo, Mkuu wa Mkoa Chalamila aliagiza kengele kugongwa na wanafunzi wote wakakusanyika ili kumsikiliza.

Akizungumza na wanafunzi, hao, Chalamila alisema kitendo cha wanafunzi kutumia simu wakiwa shuleni ni utovu wa nidhamu na kinyume cha sheria za shule na kwamba ndicho chanzo cha tukio la mabweni ya shule hiyo kuchomwa moto.

**Salome Kitomari (Dar) na Nebart Msokwa, CHUNYA**

## Askari polisi kortini kwa tuhuma rushwa mil 60/-

INATOKA UK. 4

Jamhuri na Indra Ghandi.

Wankyo alidai katika shtaka la pili wanadaiwa Julai 3, mwaka huu maeneo ya Mtaa wa Jamhuri na Indra Ghandi walipokea rushwa ya Sh. milioni 48 kutoka kwa Aisha Gote kwa niaba ya dada yake Nazima Khambiye.

Shtaka la tatu linawakabili washtakiwa wote, kwa madai kuwa wanadaiwa Julai 5 mwaka huu katika maeneo hayo walipokea rushwa ya Sh. milioni mbili kutoka kwa Nazima ili wasimpeleke Kituo cha Polisi.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa shtaka la nne linamkabili Patrick, inadaiwa kuwa kati ya Julai 3 na 5 mwaka huu Mtaa wa Jamhuri na Indra Ghandi, kwa udanganyifu alijitambulisha kuwa ni Ofisa wa Benki Kuu Tanzania (BoT) huku akijua si kweli.

Katika shtaka la mwisho washtakiwa wanadaiwa kujipatia Sh. milioni 50 huku wakijua fedha hizo ni zao la makosa ya wizi.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu lolote sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri lao. Kesi iliahirishwa hadi Oktoba 17, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Katika kesi nyingine iliyosomwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rwizile, washtakiwa waliofikishwa kizimbani ni Askari wa Jeshi la Polisi Kitengo cha Upelelezi, Shaban Shillah, Emmanuel Njegele, Joyce Kitta na Ulimwengu Rashid.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Maghela Ndimbo, alidai kuwa washtakiwa wote Desemba 17, 2018 eneo la Klabu ya Raibow. Mbezi Beach jijini Dar es Salaam, walishawishi rushwa ya Sh. milioni 200 kutoka kwa Diana Navisha kama kishawishi cha kutomchukulia hatua kwa tuhuma za kufanya biashara ya nyara za serikali.

Ndimbo alidai kuwa katika shtaka la pili, Desemba 17, washtakiwa walipokea rushwa ya Sh. milioni sita, Desemba 18 walipokea rushwa ya Sh. milioni sita, Desemba 19, walipokea rushwa ya Sh. milioni mbili na Desemba 23, 2018 walipokea rushwa ya Sh milioni mbili, fedha hizo zote walipokea Kituo cha Polisi Kawe.

Katika shtaka lingine Januari 3, mwaka huu, eneo ya Mgahawa wa Tamarind walipokea rushwa ya Sh. milioni mbili, Aprili 13 walipokea rushwa ya Sh. milioni moja maeneo ya Tripple Seven Baa na Mgawaha.

Mshtakiwa Joyce anadaiwa kughushi maelezo ya Diana akidai kayatoa mwenyewe na kutia saini wakati akijua si kweli.

Katika shtaka la Mwisho, mshtakiwa Shaban na Emmanuel wanadaiwa Aprili 13 mwaka huu walikaidi amri halali iliyotolewa na Mchunguzi wa Takukuru, Colman Lubisi iliyowataka kuwaweka chini ya ulinzi.

Washtakiwa walikana mashtaka, upelelezi haujakamilika na upande wa mashtaka haukuwa na pingamizi la dhamana.

Washtakiwa walitakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye vitambulisho vya taifa, watie saini dhamana ya maandishi ya Sh. milioni 10 na kati ya wadhamini hao mmoja awe na hati ya mali isiyohamishika.

Mshtakiwa Shaban alitimiza masharti ya dhamana lakini washtakiwa wengine wote walishindwa kukamilisha.

Kesi itatajwa Oktoba 16, mwaka huu.

## Risiti EFD mfupa mgumu kwa mapambano ya rushwa

INATOKA UK. 3

Sh. 100,000 huo ni udanganyifu, unaidanganya TRA, serikali na unajaribu kukwepa kodi serikali isipate kodi yake," alibainisha.

Mbungo alisema watu wengi wamejenga mazoea kuwa rushwa ni nipe nikupe, kwa kutoa kitu upate huduma au kutoa kitu upate kitu unachokitaka.

"Dhana ya rushwa imekuwa pana sana, tuna makosa 24 ambayo mengine hayana nipe nikupe ya moja kwa moja, mfano matumizi mabaya ya ofisi, mtu katumia vibaya ofisi ya umma amefanya vitu vya kumnufaisha yeye huwezi kuona nipe nikupe pale," alifafanua.

## PP ashtukia janja ya mawakili msamaha JPM

INATOKA UK 2

Riaz Aziz Khan, Mohammad Tayyab, Ali Bakhash, Abdulrahman Mohammed, Martin Crasta, Imtiaz Feyaz, Arshad Muhammad, Hamza Sharif na Zulfiqar Ali.

Hakimu Ngoka alisema mahakama imewatia hatiani kwa kukiri kufanya kosa hilo nchini na kuamuru kila mmoja kulipa faini ya Sh.milioni 10 au kwenda jela miezi 12.

Ngoka mbali na kuwapa adhabu ya kulipa faini, pia aliwaonya washtakiwa hao na kuwataka kutii sheria, kanuni na taratibu za nchi pindi wanapoingia nchini.

Wakili Mkuu wa Serikali, Maritenus Marandu, alisema kabla ya jana, washtakiwa hao waliandika barua iliyowasilishwa na Wakili wao, Steven Mosha ikionyesha washtakiwa hao kukiri makosa yao.

Akiwakumbusha washitakiwa hao makosa yao Wakili Mwandamizi wa serikali Mkoa wa Arusha Abdallah Chavula akiwa na Wakili Idara ya Kazi Arusha, Emmanuel Mweta, alisema washitakiwa hao walifanya kosa la kufanya kazi nchini bila vibali vya kazi kati ya Novemba 2018 na Januari 2019.

Washtakiwa hao walifanikiwa kulipa faini hiyo na kuachiwa huru.

**IMEANDIKWA NA BEATRICE SHAYO, DAR NA CYNTHIA MWOLOLEZI, ARUSHA**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: **0713 525954 / 0787 822000.**

**VIWANJA/NYUMBA.** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Nyumba inauzwa Kaloleni Arusha ina frame za biashara,nyenye SQ 59 mil 800. Nyumba inauzwa Usariver ya bedroom4 mil 70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA VYETI



**AZIHADI ABDIRASHID** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo: cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1381-0053** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari MALIBWI, Cheti cha Certificate of General Agriculture chenye number **CGA/2013/07/1413** kilichotolewa na chuo cha MATI MTWARA pamoja na Transcript ya General Agriculture kilichotolewa na MATI MTWARA chenye namba **CGA/2013/07/61.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chcote cha Polisi. Polisi taarifa: **LUS/RB/1305/2017**

115444802

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHARLES M. CHIWALANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0716-0018** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1999 katika Shule ya Sekondari MALECELA,. Yeyote atakaekion ataoe taarifa kituo chochcote cha Polisi. Polisi taarifa/Control Number: **9910810116066**

115444902

## KUPOTEA KWA LEAVING CERTIFICATE



**MARY CHARLES LIWELI** anatangaza kupotelewa na Leaving Certificate yenye index namba **S/494/0043** kilichotolewa na ULEMBWE SEKONDARI MWAKA 2010. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/313937/19.**

115445002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

BOYS MECHANICS & INJECTION PUMPS anatangaza kupotelewa na kadi ya gari iliyokuwa na namba ya usajili T 631 AKU yenye chasis namba 3428776 injini namba 1816307.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: IR/TR/RB/2079/2019

215444502

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA
KILOSA
YAH: MAOMBI NA: 02/2019

JOHN J. DINYA (Suing as next friend) LISPAMETHOD KIKOTI AND ANTHONY METHOD KIKOTI........MLETA MAOMBI

VERSUS

MANYUSI ANTHONY KIKOTI................1 MJIBU MAOMBI
AYUBU METHODI KIKOTI.......................2 MJIBU MAOMBI
COSMAS CHUWA....................................3 MJIBU MAOMBI

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA AYUBU METHODI KIKOTI**

Popote Ulipo Unaarifiwa Ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Kilosa,Tarehe 23/10/2019 mwenyewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imesainiwa leo tarehe 27 Mwezi 09 Mwaka, 2019.

115445202

## KUPOTEA KWA CHETI



**CATHERINE LUCAS KANTAMBI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Sita chenye index namba **S1610/0502** kilichotolewa na CHIEF KIDULILE SEKONDARI MWAKA 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MBA/RB/353740/2019.**

115445902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ERMIYAS SAMUEL BEYENE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 357 CED NISSAN MARCH.** Chassis namba **AK12818208.** Engine namba **CR12316919.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **WMB/RB/8970/19.**

115445402

## KUPOTEA KWA KADI

**JM SERENGETI ESSENTIALS LIMITED** inatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaj yenye namba ya usajili MC 195 CAG aina ya BAJAJ BOXER Chasis namba MD2A21BY9JWB93395

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **CHA/BI/RB/189/2019**

215443002


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa

Tupigie 0767 223311

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe MWANGA WA JAMII



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# KLOPP: SINA HASIRA NA UKUTA WA LIVER

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amekataa kukishutumu kikosi chake cha Liverpool kwa kuruhusu kufungwa mabao matatu kwenye mchezo wao wa ushindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Salzburg - na akasisitiza "sasa tumeanza mashindano" kwenye Kundi E.

Mohamed Salah alifunga mara mbili huku Sadio Mane na Andrew Robertson kila mmoja akifunga bao moja kwa mabingwa hao watetezi wa kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuweza kupata ushindi wa mabao 4-3 kwenye Uwanja wa Anfield juzi Jumatano, wakiwa wametoka kufungwa 2-0 na Napoli kwenye mchezo wa kwanza.

Miamba hao wa Italia, Napoli walitoka sare ya bila kufungana na Genk kwenye mchezo wao wa pili.

Klopp aliiambia BT Sport: "Ni bora kujifunza soka wakati wa mchezo kuliko kuzungumza baadae.

"Nilifikiri tulikuwa kwenye kiwango cha juu katika kipindi cha dakika 30 za mwanzo, halafu Salzburg wakabadilisha mfumo na kuanza kutusababishia matatizo.

"Haraka walipobadilisha mchezo, ilikuwa ngumu kwetu kuweza kwenda nao sambamba.

# Arsenal yarejea kumwania Upamecano

**LONDON,** England

ARSENAL inatarajia ikafanikisha mchakato wa kumsajili mchezaji wa RB Leipzig, Dayot Upamecano, katika kipindi cha majira ya joto mwakani baada ya dau lake kupungua.

Kocha Unai Emery amemtaja beki huyo wa kati wa Ufaransa kuwa mmoja wa wachezaji anaowahitaji katika kipindi cha majira ya joto mwakani ili kuimarisha kikosi chake kwenye idara ya ufundi.

Ofa ya awali ya klabu hiyo maarufu kwa jina la The Gunners ya pauni milioni 55 ilikataliwa na vigogo hao wa Ujerumani, ambaye kwenye mkataba wake imetajwa kuwa ana thamani ya pauni milioni 82.

Hapo nyuma, Emery alifikiria kumsajili David Luiz kutoka Chelsea lakini mapema msimu huu alibaini kwamba Mbrazili huyo hataweza kumudu vema safu hiyo ya ulinzi ambayo anahitaji kuona imeimarika zaidi.

Huenda Arsenal ikapata nafasi ya kumsajili Upamecano kwa dau linalokaribia pauni milioni 55 katika kipindi cha majira ya joto mwakani.

Kwa mujibu wa gazeti la L'Equipe la nchini Ufaransa, kupitia jariba la The Sun, limeandika kuwa dau la mchezaji huyo litashuka na kufikia kiasi cha pauni milioni 53 labda beki huyo awe amesaini mkataba mpya kabla ya msimu huu haujamalizika.

RB Leipzig ilimsajili Mfaransa huyo kwa dau la pauni milioni 9 kutoka kwa ndugu zao Red Bull Salzburg mwaka 2017 na kiwango chake kimekuwa kikipanda kila siku na anatajwa kuwa mmoja wa mabeki bora vijana duniani.

Beki huyo amecheza mechi mbili tu msimu huu baada ya kukosa michezo minne ya kwanza kutokana na kuwa na majeraha ya mguu.





# Lampard aelezea furaha ya ushindi

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, alifurahia ushindi wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kama kocha, lakini ameionya timu yake: "Sasa kazi ngumu imeanza."

Ushindi wa 2-1 ugenini dhidi ya miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Lille ilinyanyua morali ya mashabiki wake baada ya mwezi uliopita kufungwa na Valencia, na Chelsea sasa ikiwa na pointi tatu mkononi inajiamini kuwa tayari kuwavaa Ajax kwenye mchezo judo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tammy Abraham katika kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa akitimiza umri wa miaka 22 na Willian akicheza mechi yake ya 300 kwa klabu hiyo, kila mmoja alifunga bao moja kuiwezesha Chelsea kupata ushindi kwenye uwanja wa Pierre-Mauroy.

Victor Osimhen alifunga bao la kusawazisha kwa Lille na kumfanya Lampard kuwa na hofu ya kupoteza mchezo huo.

Lakini baadae akaondoka uwanjani hapo akiwa na furaha baada ya ushindi huo nchini Ufaransa ambako Lampard, alikuwa nahodha wakati Blues wakilibeba taji hilo mwaka 2012.

Alisema baada ya mchezo huo: "Najisikia vizuri, kwa sababu hapa ndio palikuwa mahali pagumu zaidi kuja na presha ya kutowafunga Valencia kwenye mchezo wa kwanza, ilikuwa kubwa mno.

"Tulicheza na mabeki watatu nyuma na walipeleka mipira mbele mara kwa mara na kwa uhakika kabisa tulicheza vizuri na tulipata ushindi tuliostahili."

# Nice yamfukuza mchezaji mwizi

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Nice imemfukuza mchezaji wake, Lamine Diaby Fadiga baada ya kukiri kuiba saa yenye thamani ya pauni 62,000 (sawa na zaidi ya Shilingi milioni 120) kutoka kwa mchezaji mwenzake, Kasper Dolberg.

Mshambuliaji wa Denmark, Dolberg mwenye umri wa miaka 21, aliibiwa saa yake katika chumba cha kubadilishia nguo Septemba 16 na kuripoti kisa hicho kwa maofisa wa polisi.

Mshambuliaji Fadiga mwenye umri wa miaka 18 ameiwakilisha Ufaransa katika kikosi cha wachezaji chini ya umri wa miaka 18.

"Nice na Lamine Diaby Fadiga waliachana siku ya Jumanne," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

Kutokana na wizi huo wa saa ya Kasper Dolberg kutoka chumba cha kubadilishia nguo na kukiri kwa mchezaji huyo, klabu iliamua kufutilia mbali mkataba wake mara moja .

Mbali na masuala ya kifedha na michezo, Klabu ya Nice haiwezi na haitakubali tabia kama hiyo ambayo ni kinyume na lengo la kuwaunganisha wafanyakazi wote wa klabu hiyo.

Dolberg alijiunga na Nice kutoka klabu ya Ajax msimu huu, huku Diaby Fadiga akiwa katika klabu hiyo kwa muda wa miaka mitatu.

Nice ipo katika nafasi ya sita katika ligi hiyo, itacheza ugenini dhidi ya klabu ilio katika nafasi ya tatu Nantes siku ya Jumamosi.







# VAN DE BEEK AIKATAA MADRID

**AMSTERDAM,** Uholanzi

DONNY van de Beek mipango yake ni kuona anaondoka Ajax huku Mholanzi huyo akiondoa uwezekano wa kuhamia Real Madrid wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Van de Beek alithibitisha wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto kwamba, Madrid waliwasiliana na Ajax juu ya uwezekano wa uhamisho wake, lakini dili la kutua kwa miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, ulishindikana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 amekuwa akiendelea kuhusishwa na mpango wa kutua Madrid huku aking'ara na vinara wa Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, Ajax, lakini sasa anataka kuondoka hapo Amsterdam msimu huu 2019-20.

"Sitaki kuondoka wakati wa kipindi cha majira ya baridi Januari," amesema Van de Beek akiiambia Voetbal International.

"Nitacheza hapa msimu wote, nitamaliza hapa Ajax mwaka huu. Hiyo inanipa mimi nguvu na utulivu. Nitaangalia nini kitatokea.

"Pengine siku moja kwenye maisha yangu ya soka itatokea kwamba nitaondoka kwenye klabu kipindi cha majira ya baridi, lakini kwa sasa sitaki."

Van de Beek alifunga wakati Ajax wakiifumua Valencia mabao 3-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano.

Amefunga mabao matatu kwenye mashindano yote msimu huu, huku akitoa pasi za mwisho nne kwenye Ligi Kuu.

# *Man United yajitosa kumwania Odegaard*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuwa imeingia kwenye mbio za kumwania, Martin Odegaard ambaye anafurahia kipindi chake cha uchezaji pale Real Sociedad.

Akiwa anacheza hapo kwa mkopo akitokea Real Madrid, Odegaard ameonekana kuwa kwenye rada za klabu nyingine barani Ulaya kwa sasa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway sasa amehusishwa na mpango wa kujiunga na United na anaweza kutua pale Old Trafford katika kipindi cha majira ya baridi kijacho.

United imeripotiwa kuingia kwenye mbio za kuwania saini ya kiungo huyo ili imsajili kipindi cha majira ya baridi Januari, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Odegaard kwa sasa amekuwa na wakati mzuri zaidi kwa miamba hao wa La Liga, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 akiwa amefunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho mbili msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway, ambaye alijiunga na Madrid kutoka Stromsgodset mwaka 2015, lakini alicheza mechi mbili tu kwa miamba hao wa Hispania, huku pia akihusishwa na mpango wa kutakiwa na Manchester City, Liverpool na Arsenal.



# DONDOO Z KA MAGAZETI Y AYA




# VALVERDE: MESSI AMEIOKOA BARCA

●●● Kufunga mabao manne ni hisia ya kushangaza, nadhani mashabiki wote wa Gunners...

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde, amesifia kiwango cha Lionel Messi, wakati klabu hiyo ikitoka nyuma na kupata ushindi dhidi ya Inter Milan kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumatato.

**Messi alirudi uwanjani kutoka majeruhi na kuwasaidia mabingwa hao wa La Liga kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Inter kwenye dimba la Camp Nou.**

Nahodha huyo wa Barca alianza katika mchezo wake wa pili msimu huu, akiwa amekosa kuivaa Getafe kutokana na mumivu ya nyama za paja pamoja na Villarreal na alitengeneza bao la ushindi la Luis Suarez dakika ya 84.

Akizungumzia kuhusu kiwango cha Messi baada ya mchezo huo, Valverde aliwaambia waandishi wa habari: "Ni mchezo wa kwanza ambao amecheza kwa dakika zote, pia ni mchezo alioonyesha umuhimu wake na mzigo kwa timu pinzani.

"Kila anapocheza anaweza kutusaidia hata kama amechoka. Messi hakuwa kwenye maandalizi ya msimu kama wengine, hivyo anatakiwa kuzoeana nao."

Messi alikuwa katikati ya ushindi wa Barca, huku mshindi huyo wa mara tano wa Ballon d'Or, alipomtengenezea pande zuri Suarez ndani ya boxi la penalti ana akafunga bao la ushindi zikiwa zimesalia dakika sita mpira kumalizika.

Valverde aliongeza: "Kuelekea mwishoni alicheza soka la kuvutia, lakini alikuwa amechoka zaidi kuliko mwanzo."

Suarez aliwanyamazisha wale wanaoshutumu kiwango chake kwa kufunga mabao hayo mawili na kumfanya afikishe mabao matatu katika michezo miwili.

Lautaro Martinez alianza kwa kuwanyamazisha mashabiki wa Barcelona kwenye Uwanja wa Nou Camp dakika ya pili, lakini Suarez akasawazisha kabla ya kufunga la pili la na ushindi.

"Washambuliaji wanaishi kwenye eneo la hatari," alisema Valverde. "Wanacheza katika eneo hatari zaidi na mara zote wanakuwa wamezungukwa na walinzi na wanahitaji kuwa suluhisho la mabao.

"Wakati mwingine huwezi kufanikiwa, kama wiki moja iliyopita, lakini alifunga moja kwenye La Liga na mara mbili kwenye ligi ya mabingwa Ulaya.

"Luis ameshaonesha kwa muda mrefu kwamba tayari ana uwezo wa kufanya lolote uwanjani."

## ZISIKUPITE

### MADDISON YAMGANDA UNITED

MANCHESTER United bado inaendelea kuwinda saini ya kiungo mchezeshaji wa Leicester City, James Maddison mwenye umri wa miaka 22, kwa dau la pauni milioni 80. ***(Mail)***

### DEMBELE ATAKIWA UNITED

WINGA wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele (22), ni mmoja kati ya washambuliaji watatu wanaotakiwa na Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ili kukujenga imara kikosi chake. ***(Manchester Evening News)***

### ODEGAARD AGOMBEWA ENGLAND

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer, ameweka wazi kwamba anamhitaji nyota wa Norway, Martin Odegaard (20), katika kikosi chake kipya, lakini kiungo huyo wa Real Madrid pia anawindwa na Arsenal, Liverpool na Manchester City. ***(Sun)***

### KANE AIVURUGA SPURS

MABOSI wa Tottenham wanahofu kuwa straika wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane (26), atakuwa kwenye kundi moja la wachezaji wazoefu wa klabu hiyo ambao wanataka kuondoka katika kikosi hicho. ***(Times - subscription required)***

### POCHETTINO MAMBO SAFI

KIBARUA cha Kocha wa Spurs, Mauricio Pochettino, hakiko mashakani kufuatia kuanza vibaya katika msimu huu na bado anaendelea kupata ushirikiano kutoka kwa mwenyekiti wa klabu hiyo, Daniel Levy. ***(Telegraph)***

### BERBATOV AITABIRIA SPURS

STRAIKA wa zamani wa Tottenham na Manchester United, Dimitar Berbatov, anaamini bosi wa Spurs, Daniel Levy, atafanya mazungumzo na Pochettino hivi karibuni ili kufahamu ufumbuzi kuhusu hatima na mwelekeo wa timu hiyo. ***(Star)***

### ALLEGRI KUREJEA MZIGONI

KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri, amesema anajipanga kurejea kwenye kibarua cha kufundisha katika kipindi cha majira ya joto mwakani, baada ya kupata mapumziko ya mwaka mmoja, na hatakubali kurudi katikati ya msimu huu. ***(Sun)***

### SARRI AMFIKIRIA KANTE

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri, anamatumaini kuwa ataungana tena na kiungo, N'Golo Kante. Kocha huyo wa Juventus ameweka wazi kwamba yuko tayari kumsajili Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 28, kwa dau la pauni milioni 70. ***(Mail)***

### TOMORI KUITWA ENGLAND

KOCHA wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, anajiandaa kumwita beki wa kati wa Chelsea, Fikayo Tomori (21), katika kikosi chake kitakachocheza mechi ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Euro 2020 dhidi ya Jamhuri ya Czech na Bulgaria. ***(Telegraph)***

### STERLING AWATULIZA WENZAKE

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England na Manchester City, Raheem Sterling (24), amesema kuwa anaamini ni suala la muda tu haujafika kwa klabu yake kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini amewataka wachezaji wenzake kuwa na uvumilivu. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# AZAM FC KUENDELEZA 'DOZI' LIGI KUU BARA

Na Mwandishi Wetu

USHINDI! Kocha Mkuu wa Azam FC, Etienne Ndayiragije, amesema kuwa anakiimarisha kikosi chake ili kiendelee kupata ushindi katika mechi zinazofuata za Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Azam FC, mabingwa wa zamani wa Kombe la Kagame, juzi ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ndanda FC kutoka Mtwara na kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex inatarajia kuwakaribisha Namungo FC ya mkoani Lindi.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Ndayiragije, alisema kuwa licha ya kupata ushindi dhidi ya Ndanda, amekiri kwamba mchezo huo ulikuwa mgumu na anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kuhakikisha wamezibakiza pointi tatu nyumbani.

Ndayiragije alisema kuwa anaridhika na muunganiko ambao umeanza kuonekana katika kikosi hicho na hayo ni matunda ya kufanya maandalizi mazuri kabla ya msimu kuanza.

"Nina imani huko mbele mambo mazuri yatakuja, timu inaendelea kuimarika, mashindano tuliyoshiriki ya kimataifa, yamekuwa pia ni kama sehemu ya maandalizi, tunaomba mashabiki wetu wazidi kutuamini," alisema kocha huyo.

Naye Ofisa Habari wa timu hiyo, Jaffer Idd, alisema kuwa kikosi chao kinaendelea na mazoezi kwa sababu inataka wachezaji waimarike zaidi na kupata matokeo mazuri katika mechi ijayo dhidi ya Namungo.

Idd alisema kuwa mechi zote za ligi hiyo zina ushindani na wao watazikabili klabu zote kwa tahadhari.

"Tunawaheshimu Namungo, ni moja ya timu ngumu na imefika hatua ya kushiriki Ligi Kuu kwa uwezo wake, mchezo wa mpira ni ushindani, lengo letu ni kupata pointi tatu muhimu," alisema Iddi.

Aliongeza kuwa wanahitaji kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ili waweze kupata tiketi nyingine ya kushiriki mashindano ya kimataifa hapo mwakani.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya SportPesa, Tarimba Abbas (kulia), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 260.3 mshindi wa Jackpot ya SportPesa, Scolastika Ngwalueson kutoka Mbagala jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mlandege, Selem View dimbani leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI Mlandege inatarajiwa kuwavaa Selem View katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa kwenye Uwanja wa Amaan, jumla ya mabao 44 yameshafungwa katika michezo 23 ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye viwanja tofauti vilivyoko Unguja na Pemba, imefahamika.

Timu ya Zimamoto yenye mabao saba ndiyo inaongoza kwa kupachika idadi kubwa ya magoli ikiwa imejikusanyia pointi tisa baada ya kushuka uwanjani mara tatu.

Mabingwa watetezi wa ligi hiyo, KMKM yenye pointi tisa sawa na Zimamoto, inashika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha klabu 16 ikiwa na magoli manne.

Chipukizi kutoka kiswani Pemba ndiyo timu inayoburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo baada ya kupoteza michezo yake mitatu iliyocheza.

Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Ali Mohammed, aliliambia gazeti hili kuwa msimu huu timu zote za Ligi Kuu zitacheza mechi za nyumbani na ugenini kwa kuanza na Pemba na baadaye kumalizia Unguja kama ratiba inavyoeleza.

"Msimu huu ni tofauti, na ratiba hii itasaidia kwa kiasi kikubwa hata kuondosha upangaji wa matokeo, na ndio maana tukasema ligi zichezwe siku za mapumziko ili timu ziwe na muda wa kusafiri, mfano timu ya Unguja itaenda Pemba na timu ya Pemba itakuja Unguja, usafiri wa boti za kwenda Pemba kama zinavyojulikana haupo kila siku," alisema Mohammed.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan itakuwa ni kati ya Mwenge dhidi ya Zimamoto huku Mwenge wakiwakaribisha Gombani na JKU watavaana na Kipanga kwenye Uwanja wa Mao.

## Uchaguzi Moro mambo yameiva

Na Mwandishi Wetu

CHAMA cha Soka Mkoa wa Morogoro (MRFA), kinatarajia kufanya uchaguzi mkuu wake ifikapo Oktoba 22, mwaka huu, imeelezwa.

Katibu Mkuu wa Kamati ya Uchaguzi ya chama hicho, Robert Lamuo, aliliambia gazeti hili kuwa tayari wameshaanza kutoa fomu kwa wadau wanaotaka kuwania nafasi mbalimbali na mwisho wa mchakato huo ni leo.

Katibu huyo alisema kuwa huu ni wakati mwingine muhimu kwa wadau wa soka wa Morogoro kujitokeza kushiriki katika uchaguzi huo ili viongozi watakaopatikana washirikiane kuleta maendeleo ya mchezo huo mkoani Morogoro.

Alisema kuwa fomu kwa ajili ya kuwania nafasi ya Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Mjumbe Mwakilishi wa Vilabu zitatolewa kwa gharama ya Sh. 200,000 na nafasi nyingine zilizosalia ni Sh. 100,000.

"Tunaamini mchakato huu utakwenda vizuri kama ulivyotarajiwa, na zoezi limeanza baada ya wilaya zote zinazounda Mkoa wa Morogoro kupata viongozi wake kama katiba inavyosema," alisema Lamuo.

## Tanzania Bara yaifuata Kenya

Na Mwandishi Wetu

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Vijana ya umri chini ya miaka 20 (U-20), cha Tanzania Bara, jana jioni kiliwasili salama katika mji wa Jinja, Uganda ili kuwavaa wapinzani wao, Kenya katika mechi ya fainali ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati itakayochezwa kesho mjini humo.

Timu ya Tanzania Bara iliyokuwa katika mji wa Gulu, imesafiri umbali wa kilomita 400 ili kufika kwenye kituo hicho kitakachochezwa mechi ya fainali hizo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zuberi Katwila (pichani chini), alisema kuwa wanatarajia kufanya mazoezi mepesi leo asubuhi ili kujiweka tayari na mchezo huo ambao kwao itakuwa ni "kufa au kupona."

Katwila alisema kuwa timu hizo mbili zinafahamiana na kila upande utaingia uwanjani ukitaka kurekebisha makosa ambayo yalijitokeza katika mchezo wa hatua ya makundi ambao ulimalizika kwa sare ya mabao 2-2.



# Michezo

Ijumaa Oktoba 4, 2019

Nipashe





Valverde: Messi ameiokoa Barca UKURASA 30



Mshambuliaji wa Yanga, David Molinga, akiwatoka wachezaji wa Polisi Tanzania katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 3-3.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga chupuchupu*

## ●●● Ni baada ya kulazimishwa sare na Polisi Tanzania, Molinga akifanya...

**Na Adam Fungamwango**

MAGOLI matatu 'hat-trick', yaliyofungwa na mshambuliaji wa Polisi Tanzania, Ditram Nchimbi yaliifanya timu hiyo kupata sare ya mabao 3-3 dhidi ya wenyeji Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**Nchimbi ameweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga 'hat-trick' kwenye Ligi Kuu msimu huu, ambao ulishuhudiwa na bosi Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali, Simon Sirro.**

Hata hivyo, kwa upande wa Yanga, straika wake, David Molinga "Falcao", jana alifungua rasmi akaunti yake ya mabao kwenye ligi hiyo kwa kufunga mabao mawili ambayo yaliifanya timu yake iweze kujinusuru na kichapo kutoka kwa Maafande hao, kabla ya nyota huyo kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) hajafunga.

Kwa matokeo hayo, Yanga inapata pointi ya kwanza kwenye msimu huu baada ya kucheza mechi mbili na kukaa katika nafasi ya 19 kwenye msimamo wa ligi hiyo yenye timu 20, mchezo wa kwanza ilifungwa bao 1-0 kwenye uwanja huo huo dhidi ya Ruvu Shooting.

Yanga ililazimika kupigana kufa na kupona kupata sare hiyo, kwani mpaka dakika ya 63, ilikuwa nyuma kwa mabao 3-1. Awali ilionekana kama ingekuwa mechi nyepesi kwa Yanga, kwani dakika ya sita tu, ilipata bao lililofungwa na mchezaji wake mkongwe, Mrisho Ngasa.

Ilikuwa ni dakika ya 33, Polisi Tanzania iliposawazisha bao kupitia kwa straika wa zamani wa Njombe Mji, Majimaji, Mwadui FC na Azam FC, Nchimbi alipoufuma mpira uliokuwa ukizagaa kwenye eneo la hatari. Nchimbi tena aliipatia Polisi Tanzania bao la pili dakika ya 55, baada ya kuwazidi mbio mabeki wa Yanga na kumhadaa kipa, Metacha Mnata na kutupia shuti lililojaa wavuni.

Dakika mbili baadaye Polisi Tanzania inayonolewa na Selemani Matola iliandika bao la tatu, lililofungwa kwa kichwa baada ya mpira wa faulo kutoka mashariki mwa uwanja, iliyotokana na Lamine Moro kumchezea madhambi, Marcel Kaheza.

Mabao hayo yalionekana kuishtua Yanga, huku Polisi Tanzania yenye makao yake makuu Moshi, Kilimanjaro wakibadili mfumo na kucheza soka la kuzuia zaidi, hivyo kukaribisha mashambulizi mengi langoni mwao.

Hali hiyo iliwagharimu dakika ya 64, baada ya straika Mkongomani Molinga kupiga kichwa kilichojaa wavuni, licha ya kipa, Kulwa Manzi kupambana kuuondoa, lakini tayari ulikuwa umeshavuka mstari wa goli.

Faulo iliyopigwa na Molinga dakika ya 68, iliifanya Yanga kusawazisha bao na kufanya ubao wa matokeo usomeke 3-3, huku Molinga akionekana ameanza kazi ya kumsaka straika wa Simba, Meddie Kagere mwenye magoli sita mpaka sasa.

Hata hivyo, Polisi Tanzania ililazimisha kumaliza mchezo huo pungufu, baada ya mchezaji wake, Yasin Mustapha, kuonyeshwa kadi nyekundu baada ya kucheza faulo zikiwa zimebakia dakika mbili mchezo huo kumalizika.

Polisi Tanzania inayoshiriki Ligi Kuu Bara kwa mara ya kwanza imefikisha pointi nne na kwenye msimamo iko kwenye nafasi ya 14 wakati mabingwa watetezi Simba wenye pointi 12 na wameshuka dimbani mara nne wanaendelea kukaa kileleni.

# Stars, Rwanda kupimana nguvu Kigali

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kuivaa Rwanda (Amavubi) katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa Oktoba 14 mwaka huu jijini Kigali nchini humo.

Mechi hiyo itachezwa kwenye Uwanja wa Kigali, ulioko katika mji mdogo wa Nyamirambo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema kuwa maandalizi kuelekea mchezo huo yamekamilika na wanatarajia utawasaidia kuwaimarisha nyota wake.

Ndimbo alisema kuwa kuelekea mchezo huo, kikosi cha Taifa Stars kilichoko chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije, kitaanza mazoezi Jumatatu.

"Shirikisho la Soka la Rwanda (Ferwafa) pamoja na TFF zimefikia makubaliano yote muhimu ya mchezo huo," alisema Ndimbo.

Aliwataja wachezaji 28 walioitwa kwa ajili ya mchezo huo unaochezwa kwenye kalenda ya kimataifa ya Fifa ni pamoja na Juma Kaseja, Metacha Mnata, Said Kipao, Salum Kimenya, Shomary Kapombe, Gadiel Michael, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr", Kelvin Yondani, Erasto Nyoni, Bakari Nondo, Himid Mao, Jonas Mkude, Kelvin John na Farid Mussa.

Nyota wengine walioitwa ni pamoja na Adi Yusuph, Iddi Suleiman, Mudathir Yahya, Salum Aboubakar "Sure Boys",Frank Domayo, Mzamiru Yassin, Shaaban Chilunda, Ayoub Lyanga, Abdul- Aziz Makame, Andrew Simchimba, Miraji Athumani, Feisal Salum "Fei Toto, Simon Msuva na nahodha, Mbwana Samatta.

Wakati huo huo Shirikisho la Soka Afrika (Caf), limewateua waamuzi kutoka Burundi kuwa ndio watachezesha mchezo wa marudiano wa kuwania tiketi ya kucheza fainali za CHAN dhidi ya wenyeji Sudan.

Taarifa ya Caf iliwataja waamuzi hao kuwa ni Thiery Nkurunzinza ambaye atasaidiwa na Willy Habimana na Shabani Niyungeko huku mwamuzi wa akiba akiwa ni Georges Gatogato.

Mchezo huo wa marudiano unatarajiwa kuchezwa Oktoba 18 mwaka huu kwenye Uwanja wa El Merriekh, Omdurman na Stars itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 katika mechi ya kwanza iliyochezwa hapa nchini.

Stars ilisonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuiondoa Kenya (Harambee Stars) kwa penalti 4-2.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002